29 JANUARI, 2026

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA PILI

### Kikao cha Tatu – Tarehe 29 Januari, 2026

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Katibu, tunayo Kanuni ya wageni ambayo tumeshauriana na Katibu na *Chief Whip,* Kanuni hii kwa kweli siyo rafiki. Hili ni Bunge la wananchi na wananchi wana haki ya kutambulishwa na kuingia ndani ya Bunge hili. Kwenye Kamati ya Kanuni, kikao kitakapotangazwa kesho, tutakaa na kutazama namna ya kuboresha zaidi ili Wabunge watambulishe wananchi ndani ya Bunge lao wenyewe. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

### MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu. Tunaanza na Mheshimiwa Emmanuel Cherehani. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko makubwa sana hapa nchini kwa wananchi wetu wanaoenda kupata matibabu katika hospitali na

zahanati zetu, wakati mwingine hata zile hospitali za rufaa. Wakifika wanaambiwa kutoa fedha za kumwona Daktari, na maeneo mengine wanatozwa fedha, shilingi 5,000, au shilingi 10,000, mpaka shilingi 30,000 ilhali madaktari hawa ni waajiriwa wa Serikali, na wanalipwa mishahara na Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia Dkt. Samia Suluhu Hassan wengine amewapandisha mpaka madaraja vizuri kabisa na stahiki zao wanalipwa vizuri, bado kuna maeneo mengine unakuta hali ya mifumo mvua imenyesha, watu wengine hakuna umeme, maeneo mengine umeme umekatika, *solar* labda hali ya hewa ni mbaya, wanafika wagonjwa wanaambiwa mifumo imegoma mpaka hali ya mifumo utakapokaa vizuri. Unakuta watoto wadogo wanahangaika, wamechemka, wakinamama wanateseka.

Mheshimiwa Spika, nataka nijue, nini kauli ya Serikali juu ya suala hili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, utaratibu tuliojiwekea kama Taifa kwenye masuala ya afya ni kuchangiana kwenye vitita mbalimbali ambavyo vinatolewa kama ambavyo vimeainishwa katika bima mbalimbali. Kwa wale ambao wanakuwa nje ya utaratibu wa Bima ya Afya kwa Wote ndiyo ambao huwa wanakutana na changamoto ya kutakiwa kuchangia pale wanapofika katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Spika, niweke wazi kwamba hawa niliowataja wanaotakiwa kuchangia ni nje ya wale ambao wamesamehewa kisheria, wakiwemo watoto wa chini ya miaka mitano, wakinamama wajawazito, wazee pamoja na wale ambao wana magonjwa ya mlipuko.

Mheshimiwa Spika, nitoe tu maelekezo kwa Wizara ya Afya kuzingatia viwango vile ambavyo vimeainishwa na Serikali kwa mujibu wa kanuni zetu ambazo zinalinda viwango hivyo ili Watanzania waweze kupata matibabu na waweze kumudu matibabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kama mtakakumbuka Mheshimiwa Waziri wa Afya alielezea hivi karibuni kusudio la Serikali kutunga sheria itakayolinda hivi viwango ili kuepukana na kila Halmashauri ama kila Mkoa kuwa na viwango vyake.

Mheshimiwa Spika, nielekeze Wizara ya Afya kuharakisha utaratibu huo ili sheria iweze kutungwa ili kuweza kuwa na viwango ambavyo vinaeleweka na viko sambamba katika maeneo yote kuepukana na kila zahanati ama kila kituo cha afya ama kila hospitali kuwa na viwango vyake na pengine maeneo mengine, viwango kuwa vikubwa zaidi vinavyosababisha Watanzania washindwe kumudu matibabu kwa uharaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mifumo kama ni masuala ya uzembe uzembe, tutayafuatilia kwa ukaribu ili pasiwepo na visingizio ambavyo vinasababisha Watanzania wachelewe kupata matibabu kwa sababu ambazo zinaweza kuzuilika. Kwa yale ambayo ni *genuine* ya kimfumo naelekeza taasisi zinazohusika kufanyia kazi ili pasiwe na malalamiko haya ya mara kwa mara kwa sababu masuala ya matibabu hayapaswi kusubiri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nimuulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa ilitoa taarifa kwamba kutakuwa na upungufu wa mvua nchini kote kwenye msimu huu wa mvua za masika na vuli. Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba kama nchi tunakuwa na utoshelevu wa chakula na kuzuia mfumuko wa bei kuelekea kipindi cha miezi ya Ramadhan na Kwaresma? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mamlaka yetu ya hali ya hewa ilitoa tahadhari hiyo, na katika baadhi ya maeneo ni kweli tumeona mvua zikiwa na mtawanyiko usiozoeleka na baadhi ya maeneo mvua zikiwa zimechelewa.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie Bunge lako Tukufu kuwatoa hofu Watanzania kwamba, kwa sasa tunacho chakula cha kutosha. Mahitaji ya chakula cha akiba kwa nchi ni takribani tani 150,000, na sasa nchi ina zaidi ya tani 400,000 za akiba. Kwa maana hiyo, tuna tani 150,000 ambayo ni *standard* na tuna zaidi ya tani 200,000 ambazo ni za ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, rai ambayo niliitoa hata nilipokutana na Wakuu wa Mikoa ni kuendelea kuwahamasisha Watanzania katika maeneo ambayo yanaweza kuwa na mvua zisizoridhisha kuzingatia ushauri wa aina ya mazao ya kupanda ambayo yanaweza yakaiva kwa kuzingatia mvua hizo hizo ambazo zimetabiriwa kwamba huenda zisiwe na mtawanyiko mzuri.

Mheshimiwa Spika, tunajua maeneo ambayo huwa yana mvua chache, hivyo, wananchi wa maeneo hayo wazingatie kupanda mazao ambayo yanaweza yakamudu kukomaa kwa kutegemea mvua zenye mtawanyiko ambao unaweza usiwe wa kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nimeelekeza pia Wakuu wa Mikoa watoe elimu kwa wananchi wetu kuendelea kuwa na matumizi mazuri ya chakula kilichopo na kile kitakachovunwa, kwa sababu kwa tahadhari hiyo tuliyopewa, huenda kwenye siku za usoni ndiko tukaanza kupata matatizo ya upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Spika, kadhalika tumetoa rai kwa wananchi kutunza chakula na kuwa na matumizi ya lazima tu ili kuweza kujiandaa endapo katika baadhi ya maeneo ambayo kunaweza kukawa na tatizo zaidi la mtawanyo la mvua, basi tuwe na akiba ya chakula.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa tahadhari ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitoa ya kuelekea Kwaresma na mwezi Mtukufu wa Ramadhani, hatuna kisingizio cha kupandisha bei kwa sababu kwa sasa tuna akiba ya chakula ya kutosha. Kwa hiyo, nitoe rai kwa wafanyabiashara wasitumie vipindi hivyo vya Kwaresma na mwezi Mtukufu wa Ramadhani kutaka kujipatia faida iliyopitiliza viwango ambavyo vinaweza kuumiza Watanzania kwa kisingizio cha tahadhari iliyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hatuna upungufu wa chakula, na tuna ziada, na pale ambapo pana tatizo, Serikali kupitia wakala wa chakula imeendelea kupeleka chakula ili kuweza kuhakikisha wananchi hawapati shida na Watanzania wote waweze kumudu kupata chakula. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa na mwendelezo mzuri kwenye sekta za michezo kwa kuendeleza kufanya vizuri timu zetu za Taifa pamoja na vilabu. Je, ni upi mkakati wa kudumu kwa Serikali katika kutambua vipaji kuanzia ngazi za chini pamoja na kujenga miundombinu ya kisasa ambayo inaendana na hadhi ya Kimataifa kuanzia ngazi za shule? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kufuatia swali hili, kwanza niungane na Mheshimiwa Rais kwa kuipongeza timu yetu ya Taifa kwa kuweka rekodi ya kucheza kwenye timu 19 bora kwenye *AFCON,* na ilikuwa almanusura ifanye vizuri zaidi. Ama baada ya hapo na nitumie swali hili pia kuvitakia kila la heri vilabu vyetu ambavyo vinaendelea kwenye mashindano ya Kimataifa hatua ya makundi. *(MakofI)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imechukua hatua nyingi za kuwezesha nchi yetu kupanda kwenye masuala ya michezo, ikiwemo kutenga shule 56 kwa nchi nzima kuwa maalum kwa ajili ya masuala ya michezo ambako vijana wetu wataendelea kufundishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na hilo, Serikali imeongeza msisitizo kwenye mashindano ya vijana wa shule za msingi kupitia UMITASHUMTA, Mashindano ya shule za sekondari kupitia UMISETA, hata sasa tumeelekeza taasisi za Serikali zinazoweza kudhamini mashindano haya ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania wafanye hivyo ili watoto wanapocheza, waimbe na nyimbo za uzalendo za kuhamasisha watu kujua kwamba kodi ndiyo maendeleo yetu pamoja na taasisi nyingine za aina hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika, Serikali imeendelea na ujenzi wa miundombinu. Hivi sasa, mbali na viwanja vitakavyotumika na *AFCON,* Serikali pia imeendelea kujenga. Imetenga baadhi ya viwanja vitakavyoboreshwa kwa ajili ya mazoezi na viwanja hivi viko mikoani, viko kwenye Wilaya zetu ambavyo pia vitatumika kwa ajili ya maandalizi ya masuala ya kimichezo.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa Halmashauri zetu kote nchini kuendelea kutunza maeneo ya wazi yanayofaa kwa ajili ya michezo. Kumekuwepo na utaratibu wa kila eneo la wazi kuuzwa na hivyo kusababisha vijana, watoto kukosa maeneo ambayo wanaweza wakafanya mazoezi ama wakafanya masuala ya michezo.

Mheshimiwa Spika, leo hii tuna baadhi ya wachezaji wanaocheza timu ya Taifa aina Feisal, Dickson Job, Metacha, Shomari Kapombe ni mazao ya mazoezi yao yaliyoanza kwenye maeneo ya wazi. Kwa hiyo, nitoe rai kwa Halmashauri zetu, Mipango Miji wahakikishe kila wanapopanga, wasiuze maeneo ya wazi yanayotumiwa na vijana wetu kwa ajili ya mazoezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika tumekaa na Wizara ya kisekta kuangalia uwezekano wa kuwa na mashindano mengi ambayo yatafanya vijana wetu waweze kupata utimamu na kujiandaa kuweza kufanya vizuri zaidi katika michezo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante. Nilikuwa naona baadhi ya majina uliyoyataja ulikuwa unasema kwa hamasa, lakini mengine ulikuwa unayataja kwa…*(Kicheko)*

Mheshimiwa Thomas Maganga Kampala.

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, mwanamazingira namba moja Tanzania ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alianzisha *slogan* ya nishati safi ili kukabiliana na changamoto ya uharibifu wa mazingira, lakini kumekuwa na taasisi za Serikali ambazo zina mamlaka ya kisheria ya kutoa leseni ya uvunaji wa miti na magogo ya asili. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukuaji wa mti mmoja wa asili huchukua miaka 30 mpaka 60 kukomaa, leseni hizi zimepelekea uvunaji holela wa miti na magogo.

Mheshimiwa Spika, je, ni nini mkakati wa Serikali kupunguza uharibu huu wa mazingira? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna aina ya misitu ambayo ukuaji wake ni wa miaka 20 mpaka 30, lakini kwa kuzingatia Sheria ya Misitu Na. 14 ya Mwaka 2002, ipo sheria inayoipa Mamlaka Wakala wetu wa Misitu *(TFS)* na mwongozo wa namna uvunaji wa miti ambao kwa kawaida unazingatia mpango wa uvunaji wa miti na unazingatia aina ya miti ambayo inatakiwa kuvunwa, idadi ya miti na muda wake wa kuvuna. Kadhalika kuna mwongozo ambao unatoa utaratibu wa kupanda miti pale ambapo umefanyika uvunaji.

Mheshimiwa Spika, ninatoa maelekezo kwa Wakala wetu wa Misitu *(TFS)* kuzingatia miongozo ambayo imetolewa hasa kuzingatia uelekeo wa Serikali ambao umejikita kwenye kuvuna miti kwenye mashamba badala ya kuvuna miti ile ya asili ili kupunguza msukumo wa kupotea kwa miti ya asili ambayo kukua kwake ni kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa Watanzania wote ni kuendelea kupanda miti, tukiiga mfano wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliotumia katika siku yake ya kuzaliwa kupanda miti na maeneo mengine yote tuendelee na utaratibu wa kupanda miti na kuitunza. Kuna baadhi ya maeneo tukipanda miti tunapanda kwa sherehe, lakini hatuitunzi ili iweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika kama ambavyo katika baadhi ya maeneo, watu wamekuwa na utaratibu wa kukata miti hata kama hawana kazi nayo, wanakata tu. Nadhani ni wakati muafaka sasa kubadilika kwa sababu hili jambo la mabadiliko ya tabianchi ni halisi na madhara yake tumeendelea kuyaona.

Mheshimiwa Spika, mtaona mwaka 2025, na mwaka 2024 yaliyotupata pale Hanang', mmeona siku hizi chache zilizopita yalitupata pale Morogoro na madhara yakaenda mpaka Dar es Salaam kwa kukosekana kwa maji, na haya yote yataenda sambamba hata maeneo mengine ambayo tunayatumia kwa kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano mdogo ni eneo ambalo lilikuwa na nyasi nyingi kwa ajili ya malisho ya mifugo, mkifyeka miti baada ya muda fulani eneo hilo halifai tena kwa malisho ya mifugo. Kwa maana hiyo tutaendelea kutengeneza matatizo katika maeneo yetu ya uzalishaji kama hatutajali utunzaji wa miti, kupanda miti na kutunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, ninatoa rai tena kwa Wakala wetu wa Misitu *(TFS)* kuzingatia mwongozo uliotolewa na Serikali na sheria ambazo zilianzisha chombo hicho.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai tena kwa wakala wetu wa misitu *(TFS)* kuzingatia mwongozo uliotolewa na Serikali na sheria ambazo zilianzisha chombo hiki.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Esther Edwin Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba Serikali imefanya kazi kubwa sana ya kulinda afya za wanawake na makundi mengine yanayojihusisha na biashara zinazohusisha nishati kwa kuweka matumizi bora ya nishati safi. Je, Serikali ina mkakati wa kuhakikisha kuwa matumizi ya nishati safi yanawafikia wajasiriamali waliopo vijijini kwa wakati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imeweka mkazo katika suala la nishati safi ya kupikia, na kiongozi kielelezo wa Kimataifa *(global champion)* ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kuhakikisha nishati inawafikia Watanzania walio wengi ambao walimchagua Mheshimiwa Esther Malleko na amekuja kuwatetea hapa, Serikali imeendelea kutoa ruzuku katika baadhi ya vifaa vinavyohitajika pamoja na nishati yenyewe ili kuweza kuhakikisha kwamba inawafikia akina mama kwa unafuu.

Mheshimiwa Spika, kadhalika kumekuwepo na wito ambao Mheshimiwa Rais mwenyewe amekuwa akielekeza kuweka unafuu kwenye majiko, kwenye nishati yenyewe ya kwenye mitungi, kupitia unafuu kwenye masuala ya kodi kwenye nishati safi hiyo ya kupikia ili kila Mtanzania aweze kumudu.

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa Waheshimiwa Wabunge na viongozi wote Serikali wakiwemo wa kuchaguliwa;

Waheshimiwa Madiwani na wengine, tuendelee kutoa elimu kwa Watanzania, kwamba hili ni jambo ambalo linawezekana. Ukirudi miaka 20 nyuma, siyo kila mtu angeweza kudhani kwamba hata vijijini kutakuwa na umeme, kutakuwa na simu ya mkononi, kumeweza kuwa na television. Maana yake ni kwamba hata hili linawezekana kwa kila familia, kila kijiji kuwa na utaratibu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Serikali tutaendelea kuchukuwa hatua hizo zinazoleta unafuu ili kila Mtanzania aweze kumudu.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya tangu ameteuliwa kuwa Waziri wetu wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya kazi kubwa sana kupeleka huduma za afya katika ngazi zote mpaka vijijini, lakini pamoja na upatikanaji wa huduma hizo kumekuwa na uelewa mdogo wa matumizi ya bima ya afya. Je, Serikali imejipangaje kutoa elimu kuhusu Bima ya Afya kwa Wote kwa wananchi mpaka vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Bima ya Afya kwa Wote ni jambo ambalo limekuwa hitaji la wananchi wa Tanzania kwa muda mrefu; na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika uongozi wake wa awamu ya kwanza alielekeza taratibu zote za masuala ya kisheria ziweze kukamilika. Ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kwamba hatua iliyosalia sasa ni kutoa elimu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ambayo kwa asili yetu ni nchi ambayo tumejengwa kwenye misingi ya undugu, nianzie hapa hapa kutoa rai kwa Watanzania wote kujiunga na Bima ya Afya kwa Wote, ni jambo la msingi ambalo litatuwezesha Watanzania wote kumudu masuala ya matibabu, kuweza kuchangia matibabu ya wale wenye uhitaji mkubwa wa matibabu na pengine wanaweza kumudu kulipia matibabu yao.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa ambalo tunatakiwa kufanya ni kujiunga kwenye vitita hivyo ambavyo vitaelekezwa na Wizara ya Afya, na baada ya kujiunga, upande wa Serikali, tunafanya kila jitihada kuhakikisha kuwa huduma hizo za afya zinapatikana kwa ukaribu, na kwa uhakika ili kuweza kuhakikisha kwamba kwa yeyote ambaye amejiunga na bima ya afya anapata matibabu ya chochote kile kinachomsumbua; tena kwa uhakika bila usumbufu ili kuweza kuhakikisha kwamba wote wanapata kuvutiwa kujiunga na bima hiyo ya afya.

Mheshimiwa Spika, katika maandalizi hayo, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliahidi kwamba ndani ya siku 100 ataongeza wahudumu wa afya, ataajiri wataalamu wa afya 5,000. Hivi tunavyoongea tayari wataalamu hao 5,000 walishaajiriwa na wamepelekwa kwenye zahanati zetu, vituo vyetu vya afya, na hospitali zetu, ili kuweza kuhakikisha kwamba mbali na majengo mazuri aliyoyajenga Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, pia tunakuwa na wataalamu wa afya wa kutosheleza katika maeneo ya hospitali zetu. Jambo hili linakwenda sambamba na upatikanaji wa vifaa vya kisasa ambavyo kwa sasa vinapatikana kwenye hospitali zetu zote.

Mheshimiwa Spika, zamani baadhi ya vifaa vilikuwa vinapatikana tu hospitali zilizopo Dar es Salaam. Ukitaka *MRI,* Dar es Salaam; ukitaka *CT-Scan,* Dar es Salaam. Hivi tunavyoongea, kila hospitali ya mkoa ina vifaa hivyo vya *CT-Scan*, masuala ya *Ultra Sound* yameenda mpaka hospitali zetu za halmashauri na za Wilaya na masuala ya *MRI* sasa yanapatikana hata kwenye hospitali zetu za kanda na hospitali zetu za rufaa. Kwa hiyo, ni hatua kubwa ambayo Serikali imepiga.

Mheshimiwa Spika, na tuwahakikishie Watanzania kwamba, wakishajiunga na bima hiyo ya afya watakuwa wameweka utaratibu wetu wa undugu wa kuweza kujihakikishia kuwa tunapata matibabu.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Madiwani na viongozi wengine wote, tuendelee kuelimishana, tuendelee kuelimisha makundi mbalimbali, tuendelee kuelimisha Watanzania kuhusu jambo hili kubwa ambalo lina manufaa makubwa na litakuwa na manufaa mapana kwa jamii nzima ya Tanzania.

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Agnesta Kaiza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Serikali imefanya maboresho ya utoaji mikopo ya 10% kwa kuziwezesha benki ziweze kutoa mikopo hiyo ndani ya baadhi ya halmashauri.

Mheshimiwa Spika, dhana nzima au sababu kuu ya Serikali kuitoa hii mikopo ilikuwa ni kwa ajili ya wale wananchi wa Kitanzania, kwa maana ya wanawake, vijana na wenye ulemavu ambao kimsingi katika hali ya kawaida hawakuwa na sifa za kukopesheka katika benki kutokana na hali zao za kimaisha ambazo zinawakumba.

Mheshimiwa Spika, sasa, benki hizi zimeweka masharti ambayo ni magumu sana ambayo hatimaye walengwa ambao Serikali imewakusudia waweze kupata ile mikopo wanashindwa kupata kwa sababu vigezo vinawatoa nje. Benki hizi zimeweka mkazo mkubwa sana wa masharti magumu kana kwamba sasa ni biashara.

Mheshimiwa Spika, wakati akina mama, vijana na wenye ulemavu wakiwa wanasubiri tabasamu kutoka kwa Mheshimiwa Rais kupitia hii mikopo, fedha hizi zimelala ndani ya benki. Ninatolea mfano mmoja, katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, *as we speak now*, shilingi bilioni 91 zimelala ndani ya benki. Wale ambao wanapaswa kukopeshwa wapo mitaani

hawawezi kukopesheka kwa sababu ya hayo masharti ambayo yamekuwa ni magumu. Kimsingi, ni kana kwamba sasa siyo tena ile 10%, ni kana kwamba sasa mtu anakwenda kukopa katika benki kibiashara.

Mheshimiwa Spika, kabla sijauliza swali, wote tunafahamu kwamba wananchi hawa ambao tumewalenga, hayo makundi matatu wengi wao hawana hata dhamana, na ndiyo maana Serikali mkaja na mpango mzuri sana wa kumkomboa kijana wa Kitanzania, kumkomboa mwanamke pamoja na wale wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, swali langu ni kwamba, Serikali kwa nia yake njema ile ile, haioni kwamba ni vyema sasa, ukabadilishwa mfumo mzima wa namna ya kukopesha zile fedha na ikibidi wananchi hawa, walengwa hawa, yatumike masharti na mifumo inayofanana ili hatimaye ile dhana nzima ya Serikali kumkomboa kijana wa Kitanzania, wanawake na wenye ulemavu iweze kuonekana kwa tija? Kwa sababu mwisho wa siku hizi shilingi bilioni 91 ambazo nimekupa mfano kutoka katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, sasa hivi tunavyoongea wananchi wangekuwa wanatabasamu kubwa sana na wakimshangilia Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo ameweza kuwakomboa.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru sana ikiwa Mheshimiwa Waziri Mkuu atatupa majibu ambayo yatapelekea tabasamu kwa wananchi ambao kimsingi ni wanyonge na Mheshimiwa Rais anahitaji kuwapatia tabasamu, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii. Ni kweli Serikali ilibadilisha utaratibu na kupeleka utaratibu wa majaribio katika baadhi ya majiji na halmashauri fedha hizi za mikopo kuanza kutolewa kwa utaratibu wa kupitia benki; na baadhi ya halmashauri ziliendelea na utaratibu ule wa awali.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa ya kufanya hivyo ilikuwa ni kupeleka utaratibu huu kwa maafisa ambao wanashughulika

na masuala ya mikopo, hasa hasa kuthibiti tatizo ambalo lilikuwa linajitokeza la vikundi hewa. Watu wanakaa kwenye halmashauri pale, wanatengeneza vikundi, wanatengeneza *syndicate* kutoka baadhi ya watumishi wa ndani ya halmashauri na wale wanaopokea fedha hizo. Kimsingi watumishi wasio waaminifu nao wanakuwa sehemu ya vikundi, wamezitanguliza kule kwenye kikundi na wao wanakuwepo kule kwenye kikundi.

Mheshimiwa Spika, baada ya zoezi lote, lile lengo la Serikali linakuwa halijatimia lile la kuwasaidia wahusika, hasa wanaofanya shughuli hizo za uzalishaji. Lengo la pili, la kwamba kutakuwepo na marejesho ili na wengine waweze kupata, nalo linakuwa halitimii. Kwa hiyo, ndiyo ilikuwa sababu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupeleka kwa majaribio kwenye maeneo haya ya benki, nimekisikia Mheshimiwa Mbunge alichokisema. Nilipata fursa ya kukaa na wafanyabiashara hizi ndogo ndogo. Nilikaa na wamachinga, bodaboda, bajaji na mama lishe. Moja ya mambo waliyouliza na waliyoelezea yalikuwa yanafanana na hayo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyasema. Maelekezo niliyoyatoa ambayo ndiyo dira iliyotolewa na Mheshimiwa Rais ni kwenda kwenye uhalisia.

Mheshimiwa Spika, machinga hawezi kuwa na hati ya nyumba. Ukimwambia alete hati ya nyumba ndipo apate mkopo, ni dhahiri kwamba hatakuwa na hiyo hati ya nyumba. Katika maeneo mengine walielezea kwamba wanatakiwa watoe dhamana, *I mean,* barua ya udhamini wa watumishi walipo Serikalini. Nayo, machinga, au bodaboda ukiwaambia waanze kuhangaika kutafuta mtumishi aliye Serikalini amdhamini, nalo ni tatizo lingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitoa maelekezo kwamba waondoe masharti hayo yanayokwamisha walengwa hawa kuweza kupata manufaa ya fedha hizo ambazo Mheshimiwa Rais amekusudia ziweze kuwafikia. Tulikubaliana na benki, walikuwepo pale, kwamba hayo masharti ya hati ya nyumba, hayo masharti ya barua ya udhamini kwa wale ambao wanatambulika hayatakuwepo.

Mheshimiwa Spika, labda nitumie tu Bunge lako Tukufu kuweka wazi eneo moja. Kwa yule ambaye hana kitambulisho cha Taifa, ndiye anayetakiwa utambuzi. Wale ndio ambao wametakiwa watoe barua ambayo *at least* imtambulishe yeye ni Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi ninakumbuka kuwa kuna watu tumesoma wote sekondari tukiwa tunagombania chakula hapo na sahani, tumeenda chuo pale tunapanga foleni, baada ya miaka kadhaa tumeona wanashika nafasi katika nchi za jirani kule. Wamesoma kwa kodi za Watanzania, wameziba nafasi za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata huku kwenye mikopo nako, niwaombe Waheshimiwa Wabunge waridhie utaratibu wa kupekua, kwamba apate Mtanzania mwenyewe, ule uendelee, lakini kwa wale ambao wana vitambulisho vya Taifa hawataulizwa hati wala hawataulizwa barua ya mtumishi yeyote anayetoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anamaanisha kwenye jambo hili la kuwawezesha vijana wa Kitanzania, wanawake wa Kitanzania, na ndugu zetu wa kutoka makundi maalum, ndiyo maana mbali na zile asilimia 4:4:2 ameongeza shilingi bilioni 200 ndani ya siku 100 baada ya kuchaguliwa kwake, ili kuongeza wigo wa vijana hawa kuweza kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, tayari Mheshimiwa Rais ameshatoa maelekezo pia katika bajeti hii inayoandaliwa utafutwe utaratibu wa kuiongeza asilimia tano nyingine ya kujenga miundombinu watakapofanyia biashara hizo, ikiwemo masoko nadhifu yenye hadhi ya utu ili akina mama na vijana waweze kufanyia biashara katika maeneo ambayo ni nadhifu. Kwa hiyo, hili nalo Serikali tunaendelea kujiandaa nalo.

Mheshimiwa Spika, asilimia tano hii itatumika hata katika baadhi ya maeneo ambako *either* wamachinga, akina mama lishe ama wengine ambao wanakosa maeneo ya kufanyia

biashara yatatumika hata kutoa fidia ili machinga wafanyie biashara katika eneo ambalo watapata wateja, na akina mama lishe wafanyie biashara ambapo watapata wateja.

Mheshimiwa Spika, mke wangu aliwahi kuwa mama lishe, kwa hiyo, ninapoongelea watu hawa, ninaongea kwa *passion* kwa sababu nimewahi kuishi kwa kulishwa na fedha hii ya mama lishe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza ninakushukuru sana, na hasa kwa hili swali la mwisho ambalo lilikuwa lina utata sana na Wakurugenzi walikuwa hawana kauli ya Serikali. Kwa tamko lako leo, hili ni agizo la Serikali na lizingatiwe na lifuatwe ili kuhakikisha wananchi hasa wa kipato cha chini wapate hizi fedha za Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, leo tuna vijana wanafanya biashara za *online*. *Online* haihitaji ofisi wala haihitaji chumba, inahitaji uaminifu tu. Bodaboda sasa hazisubiri abiria, zinafanya *delivery.* Hawa wote wanahitaji mchango huu wa Mheshimiwa Rais ili na wao wawe sehemu ya hili.

Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana kwa majibu sahihi na ninakupongeza sana. *(Makofi)*

Waziri Mkuu aliyestaafu alikuwa upande huu, na Waziri huyu yupo upande huu. Kwa hiyo, tusubiri mengi kwenye ukumbi huu, na kiti kitadhibiti maneno mengi ambayo hayatokuwa na mpango, au sambamba na matakwa ya kiti. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninamwita Mwenyekiti Mheshimiwa Najma aje kuendelea na Shughuli za Bunge.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Muhtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu, tuendelee.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na maswali ya kawaida sasa tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo Mbunge wa Moshi Mjini aulize swali lake.

Na. 40

**Ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Moshi**

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka fedha za kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya inayojengwa Kata ya Ng'ambo Halmashauri ya Manispaa ya Moshi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo, Mbunge wa Moshi Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilianza ujenzi wa miundombinu ya Hospitali ya Manispaa ya Moshi Februari, 2023, ambapo jumla ya shilingi bilioni 1.96 zimetumika kujenga jengo la ghorofa kwa ajili ya huduma za wagonjwa wa nje *(OPD)*. Ujenzi wa miundombinu ya hospitali hiyo umefikia 55%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imetenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Moshi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo.

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nilishukuru Bunge hili Tukufu. Nami ni miongoni mwa Wabunge wapya wa kwanza kufika. Pia, nimshukuru Mheshimiwa Rais pamoja na chama changu. Vilevile, niwashukuru Wanamoshi wote kwa kuniamini na kunipa kura nyingi za kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu kwa sasa upo kwa 50% na mradi huu ulipaswa uishe kuanzia Machi, 2025 na mkandarasi ambaye yupo *site* ni mkandarasi mwenye uwezo, sina mashaka naye, lakini lugha na ushirikiano wa watendaji, siyo mzuri kwake. Kwa maana hiyo, je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kufika Moshi Mjini eneo la tukio ili kutatua changamoto hizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Ni lini Serikali itazipandisha hadhi Zahanati za Bondeni, Kaloleni, Njoro, na Kiboriloni kutokana na ongezeko kubwa la wagonjwa? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge hili Tukufu nitoe maelekezo kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa Wakurugenzi wote nchini, kwanza kuwapa taarifa Waheshimiwa Wabunge kuhusu fedha ambazo Serikali imezipeleka katika maeneo yao, kwa maana wao ndio wanaoziomba fedha hizi na Serikali inapeleka. Kwa hiyo, ni muhimu sana kuwapa taarifa ili kuona nguvu yao kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuhusu suala la kupandisha zahanati kuwa kituo cha afya, niendelee kuwaelekeza Wakurugenzi kujenga miundombinu wezeshi katika zahanati zetu hasa majengo ya maabara na majengo ya upasuaji, ili kuhakikisha tunapandisha zahanati zetu kote nchini kuwa vituo vya afya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nape Moses Nnauye.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na kazi nzuri sana ambayo imefanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuweka miundombinu ya afya na vifaa tiba kwenye maeneo mengi ya nchi yetu, ongezeko la maeneo haya ya huduma za afya ambayo hayajakamilika kama hospitali, zahanati na vituo vya afya kwa maana ya majengo, inaongezeka kwa kasi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni umefika wakati tukaweka nguvu kukamilisha maeneo haya ili yakamilike kabla ya kuendelea na maeneo mengine mapya, kwa sababu maeneo haya yanaongezeka kwa kasi nchini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuwekeza katika vituo vyetu vya afya hasa kwenye mashine za kuweza kutoa huduma za vipimo katika maeneo yote kote nchini. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kuongeza huduma katika vituo vyetu na kutangaza huduma mpya ambazo zinapatikana katika vituo vyetu, ili wananchi waweze kuwa ni wanufaika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Kituo cha Afya cha Bunda ambacho kipo Kata ya Bunda Mjini, kinatoa huduma kwa watu wengi, lakini kuna majengo ambayo hayajakamilika na ni muhimu; *OPD* tunahitaji shilingi milioni 184, wodi ya wanawake na wanaume shilingi milioni 342, vyote vina thamani ya shilingi milioni 524. Ni lini mtakamilisha na hasa ukizingatia kinatoa huduma kwa wananchi wengi hasa kwenye kata saba za mjini?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli Serikali imeendelea na utaratibu wa kuwezesha vituo vyetu vya afya hasa majengo ambayo ni muhimu kulingana na uhitaji. Kweli Bunda Mjini ina ongezeko la watu wanaohitaji huduma hizi na Serikali tunaendelea kutenga fedha hasa kupitia mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuwezesha kituo chetu cha afya cha Bunda Mjini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Pascal Lucas Lutandula, Mbunge wa Chato Kusini.

Na. 41

**Kupandisha Hadhi Kituo cha Afya Bwanga**

**MHE. PASCAL L. LUTANDULA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha mchakato wa kukipandisha Kituo cha Afya Bwanga kuwa Hospitali ya Wilaya?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya tathmini ya miundombinu katika Kituo cha Afya Bwanga na kubaini upungufu wa miundombinu muhimu ikiwemo jengo la huduma za nje *(OPD)* pamoja na wodi za kulaza wagonjwa, wodi ya wanaume, wodi ya wanawake, magonjwa mchanganyiko, wodi ya watoto na wodi za upasuaji kwa wanaume na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kipaumbele cha Serikali ni kuongeza na kuboresha huduma zinazotolewa katika Kituo cha Afya Bwanga, kwa kuongeza miundombinu inayopungua na

kukarabati miundombinu chakavu ili kuwezesha kituo hicho kutoa huduma bora. Serikali itakipandisha hadhi Kituo cha Afya Bwanga kwa kuzingatia miongozo ya Wizara ya Afya mara baada ya kuongeza na kuboresha miundombinu katika kituo hicho.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pascal Lucas Lutandula.

**MHE. PASCAL L. LUTANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, nimshukuru sana Mungu kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kufika kwenye jengo hili na ukumbi huu, mimi mtoto wa Mama Ntilie, siyo rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nianze kwa kumshukuru sana Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali kukipandisha hadhi Kituo chetu cha afya cha Bwanga. Hata hivyo, Bwanga tumekuwa na changamoto kituo hiki kinapata wangojwa wengi sana. Wagonjwa wa nje tu kwa siku ni takribani wagonjwa 160 mpaka 300, lakini katika majibu ya msingi ya Waziri sikusikia akieleza upungufu tulionayo hususan gari na uzio wa kuzunguka Kituo cha Afya cha Bwanga, kwa sababu tunapakana na soko ambalo tumekuwa na mwingiliano kati ya wagonjwa na wafanyabiashara kama wauza miwa, ndizi na mihogo. Kwa hiyo ni lini sasa Serikali itatenga bajeti ya kwenda kujenga uzio na kutupelekea gari la wagonjwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, ninamwomba Waziri kwa majibu mazuri na niwashukuru sana watu wa Busanda kwa kumchagua Naibu Waziri. Kwa kweli ninaridhika na majibu yake, lakini ninaomba kujua, ni lini ataongozana na mimi kwenda kwenye Jimbo la Chato Kusini kwa sababu Wanachato Kusini bado wanazo changamoto nyingi katika upande wa afya ukajionee ili tupate majibu ya Serikali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Pascal Lutandula Mbunge wa Chato Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunakumbuka Jimbo la Chato na Halmashauri ya Chato lilikuwa Jimbo moja na waliweza kunufaika na magari ya wagonjwa. Walipata magari mawili mwaka 2025, gari moja kutoka Wizara ya Afya na lingine kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI. Hivyo, kwa idadi ya ongezeko la wagonjwa, kulingana na idadi ya magari ambayo tunaenda kuyapokea kutoka Wizara ya Afya, tutaendelea kutenga magari ya wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Bwanga na vituo vingine vinavyohitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uzio, nimwelekeze Mkurugenzi kuendelea kutenga mapato ya ndani na kuanza kujenga uzio wa kituo chetu cha afya katika Halmashauri ya Chato. Pia, suala la ziara ni kazi yetu TAMISEMI na tumekuwa tukiifanya na tumeshazunguka halmashauri nyingi sana nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Pascal Lutandula kwamba, baada ya Bunge hili tutaongozana pamoja kwenda jimboni kukiona kituo chetu na kuweka msisitizo katika kutoa huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu.

**MHE. DOTTO J. BAHEMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo letu la Ngara kuna Kata ya Nyakisasa yenye zahanati ambayo inatoa huduma zinazokidhi kabisa kutolewa katika kituo cha afya. Sasa bado pia kuna maendeleo ya ujenzi ambayo yanafanyika kwa ajili ya kufikia ubora. Nilikuwa naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini Serikali itaipandisha hadhi Zahanati ya Nyakisasa kuwa kituo cha afya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka jana wa fedha zimejengwa jumla ya zahanati 1,100 kote nchini kupitia mpango wa Serikali. Katika zahanati hii tutaendelea kujenga miundombinu wezeshi hasa jengo la upasuaji, wodi ya wanawake na wanaume ili kifikie hatua

ya kukipandisha kwenda kituo cha afya. Tutawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Afya ili waweze kukipandisha kutoka zahanati na kwenda kituo cha afya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa Watumishi wa Umma Tarime Vijijini ni 42%. Tuna vituo vya afya sita havina madaktari wala wataalamu wa maabara. Ni linii Serikali itapeleka huduma hiyo muhimu katika maeneo hayo ili wananchi wapendwa wa Tarime Vijijini wapete huduma hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu kuajiri watumishi 5,000 wa kada ya afya na wamekwisha sambazwa nchini. Ninaomba kutoa maelekezo kwenye halmashauri anayotoka Mheshimiwa Waitara, Mkurugenzi aweze kuajiri kwa mkataba, na umekuwa utaratibu wa Serikali hasa kwenye maeneo ya upungufu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria. Kuna swali la Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Sara Msafiri Mbunge wa Mvomero.

Na. 42

**Upatikanaji wa Vyeti vya Kuzaliwa – Ifakara**

**MHE. SARA M. ALLY K.n.y. MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kila Mtoto anayezaliwa Halmashauri ya Mji Ifakara anapata Cheti cha kuzaliwa kwa wakati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge hili la Kumi na Tatu, ninaomba nichukue fursa hii adhimu kwanza kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniteua kutumikia dhamana hii ya Naibu Waziri, Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mwenyezi Mungu anisadie katika kutekeleza majukumu haya kwa ufanisi kwa moyo wangu wote na nguvu zangu zote. Sasa nijibu swali la Mheshimiwa Abubakar Asenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini imeweka mfumo wa kusajili watoto na kuwapa vyeti vya kuzaliwa pindi wanapozaliwa ndani ya siku 90 bila malipo katika Halmashauri zote za Tanzania Bara ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Ifakara. Aidha, Halmashauri ya Mji wa Ifakara ina jumla ya vituo 39 ikiwemo vituo vya tiba 20 na Ofisi za Watendaji Kata 19 ambavyo vinasajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, wawahamasishe wananchi katika majimbo yao wanapopata watoto kuhakikisha wanasajiliwa na kupewa vyeti katika vituo vya tiba walipozaliwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sara Msafiri.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nishukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Kwa kuwa vyeti hivi vinatolewa kwa kuandikwa, na mkono na mara nyingi inakuwa ni changamoto kubwa sana vyeti hivi kukubalika kwenye baadhi ya taasisi zikiwemo za Serikali, kama vile kwenye bima ya afya, je, Serikali sasa iko tayari kubadilisha mfumo wa utoaji wa vyeti hivi viwe vya kidijiti ili viweze kukubalika na taasisi nyingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa bado uhamasishaji wa kupata vyeti hivi uko chini sana, je, Mheshimiwa Naibu Waziri, uko tayari kuunda timu kwa ajili ya kwenda kufanya uhamasishaji hasa kwenye ngazi za tarafa, ili wananchi wale waweze kupata huduma hizi kwa ukaribu zaidi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Sara Msafiri, kwa maswali yake mazuri ambayo ameyauliza kwa niaba ya Mheshimiwa Abubakari Asenga. Ninaomba niyajibu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpe uhakika *(assurance)* Mheshimiwa Mbunge, kwamba vyeti hivi vya kuzaliwa vinavyotolewa katika vituo vya tiba, ni vyeti ambavyo vimesajiliwa katika mfumo wa *RITA* na vinakubalika na kutambulika katika taasisi mbalimbali za kiserikali ikiwemo Bima ya Afya ya Taifa *(NHIF)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, *RITA* inaboresha mfumo wake wa usajili ambapo sasa baada ya taarifa za mtoto kuingizwa katika mfumo, mzazi atakuwa anapokea namba mahususi *(notification number)* ambayo ataitumia kupata cheti cha kimtandao bila malipo yoyote *(online certification)*. Hii ni utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambapo ameiagiza Serikali kutumia mifumo ya kidijiti kutoa huduma za muhimu kabisa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili, kampeni za uhamasishaji na kampeni za usajili wa vizazi na vifo. Ni kweli *RITA* imekuwa ikifanya kampeni hizi kwa kufika maeneo mbalimbali ya nchi na katika kipindi cha Julai mpaka Disemba mwaka 2025, tayari *RITA* imeweza kufika katika Wilaya mbalimbali ikiwemo Singida, Sengerema, Ukerewe, Longido, Arusha, na Mbarali kwa ajili ya kutoa huduma hizo za kuhamasisha wananchi ili waweze kuwaandikisha watoto waweze kupata vyeti vya kuzaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika Maonesho ya Saba Saba, Maonesho ya Nane Nane, na hata kwenye Kampeni ya Huduma ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, huduma hizi za uhamasishaji zinatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali kupitia wakala huu wa *RITA* utaendelea kufanya kampeni hizo kufika maeneo mbalimbali ili wananchi waweze kufahamu na wapate huduma ya usajili wa vizazi na vifo. Aidha, Serikali katika kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, *RITA* kupitia mfumo wa *(e-RITA)* ambao ni mfumo wa kidijiti, sasa inatoa huduma hizi za upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa na vyeti vya vifo ndani ya masaa 48 kwenye mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mtanzania popote alipo anaweza kuingia katika mfumo wa *e-RITA* akaomba cheti cha kuzaliwa, ama akaomba cheti cha kifo na ndani ya masaa 48 akawa amekipata kidijiti. Serikali itaendelea na jitihada za kuboresha huduma zinazotolewa na *RITA* ili wananchi waweze kupata manufaa na hasa kwa kutumia mifumo ya kidijiti. *(Mkofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Kombani.

**MHE. LUCY D. S. KOMBANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Hoja yangu ilikuwa hivi, huu mfumo uliopo sasa hivi wa kupata vyeti vya kuzaliwa uko *complicated* sana hasa kwa watu wa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni sasa ni muda wa kutumia mfumo kama ule wanaotumia *NECTA* wa kupata vyeti, kwamba watu wanamaliza shuleni kwao, vyeti vyao wanakuja kuvikuta kwenye shule zao; hivyo hivyo tunaweza tukafanya kwenye vyeti vya kuzaliwa kwamba, mtu amejifungua sehemu fulani ni rahisi sana kwake kukifuata cheti cha kuzaliwa ile sehemu aliyojifungulia kuliko utaratibu huu ulipo sasa hivi ambao hauko *friendly* kwa watumiaji wengi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, usajili na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa na hasa kwa watoto na makundi mengine, unafanyika siyo tu kidijiti peke yake lakini pia kuna vituo 11,718 ambavyo vinatoa huduma hiyo. Vituo hivyo ni 7,761 vituo vya tiba, kuna vituo 3,957 ambazo ni Ofisi za Watendaji Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mtanzania anaweza kwenda kupata usajili na kupata cheti cha kuzaliwa kupitia Ofisi za Watendaji wa Kata, na katika vituo vyetu vya tiba, hata pale mtoto anapopelekwa kliniki, taarifa zake zinachukuliwa na mtoto anaweza kupatiwa cheti cha kuzaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa wakati huu tunatumia mifumo yote, tunatumia mifumo ya vituo vyetu hivi, na pia tunatumia mifumo ya kidijiti kwa ajili ya kurahisisha huduma hizi za msingi za upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Kafiti William Kafiti, Mbunge wa Ilemela aulize swali lake.

Na. 43

**Mgogoro wa *Airport* na Wananchi wa Kata ya Shibula - Ilemela**

**MHE. KAFITI W. KAFITI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kulipa fidia au kuruhusu wananchi kuendeleza maeneo yao baada ya mgogoro wa muda mrefu na *Airport* – Mwanza?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba uridhie kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Kafiti, niweze kutoa maelezo kidogo. Kwa kuwa tuna habari njema sana asubuhi ya leo ambapo Ndege yetu ya *Air Tanzania* imeanza safari zake rasmi Nchini Ghana kwenye Jiji la Accra.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndege yetu iliondoka jana hapa ikiongozwa na ujumbe wa Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa Mnyaa, Waziri wetu wa Uchukuzi, pamoja na timu ya wataalamu ikiongezwa na Mkurugenzi Engineer Peter Ulanga, wamekwenda na wamefika salama kupitia Lagos. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kinakuwa kituo cha 17 kikiwa kimeanzishwa ndani ya siku 100, ndege yenye ukubwa wa kubeba abiria 180 ambayo ni *Boeing B 737 – MAX* 9. Nimeona niseme hili kwa sababu ni habari kubwa na nzuri, hivyo Watanzania wanaweza kwenda moja kwa moja mpaka Accra, Ghana siku za Jumatatu, Jumatano na Ijumaa. Kwa hiyo, tumpongeze Rais wetu mpendwa kwa maono makubwa yanayotekelezeka na yanayoonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa uridhie kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi nimjibu Mheshimiwa Kafiti William Kafiti Mbunge wa Ilemela kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua mgogoro wa muda mrefu wa ardhi katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Serikali inaendelea kulishughulikia suala hilo kupitia timu ya wataalamu iliyoundwa na Ofisi ya Waziri Mkuu itakayofanya

uchambuzi wa kina wa suala hilo. Timu hiyo pamoja na mambo mengine itatoa mapendekezo kwa ajili ya maamuzi ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kafiti William Kafiti.

**MHE. KAFITI W. KAFITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ninaomba niulize swali la nyongeza. Sote tunatambua mgogoro huu wa wakazi wa Shibula na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege umechukua muda mrefu yapata zaidi ya miaka 10 sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imekiri uwepo wa mgogoro huu wa muda mrefu, vilevile ninapenda kuishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuweza kuteua tume hii ya kitaalamu kuweza kushughulikia mgogoro huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua, kwa sababu mgogoro huu umekuwa ni wa muda mrefu na unakadiriwa kuwa na wakazi zaidi ya 1,440 ambao wanaishi katika kata hizi tano kwa maana ya Mtaa wa Shibula, Mtaa wa Semba A, Mtaa wa Bulyanhulu, Mtaa wa Nyamwilolelwa, pamoja na Kihili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitaa hii mitano imekuwa katika mgogoro mkubwa ambapo wakazi hawa sasa wanashindwa kuendeleza makazi yao. Sasa ni nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba Kamati hii iliyoundwa, lini itakwenda kukamilisha suala hili, ili wananchi wangu wa kata hizi waweze kupata muafaka wa suala hili? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nipokee shukrani zake, yeye mwenyewe amekiri mgogoro huu umedumu kwa miaka zaidi ya 10. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutambua uzito na umuhimu ameamua kuunda tume au timu ishughulikie na hatimaye tufike mahali pazuri ili wananchi wetu wa Shibula na mitaa mitano na wananchi wa Ilemela na Mwanza kwa ujumla

tufike hatima ya mgogoro huu. Ni dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita kuhakikisha kwamba, Uwanja wa Mwanza unaboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ambaye kimsingi ni mpenda maendeleo na amekuwa mfuatiliaji mzuri kwamba, dhamira ya Serikali kwenye uwanja huo ni kubwa, na kwenye jimbo lake ni kubwa na ndiyo maana hapo hapo Shibula barabara inajengwa ya lami. Hapo hapo Ilemela tumezindua meli na hapo hapo Uwanja wa Ndege wa Mwanza tunajenga jengo kubwa la abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho na muhimu kuliko yote, tunataka tuufanye uwanja wa Mwanza kuwa wa Kimataifa. Hivyo ili ufanikishe hilo, lazima uhakikishe kwamba, usalama unazingatiwa na hauwezi kuwa na usalama kama wananchi watakuwa wamevamia kwenye maeneo ya uwanja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Bananga, nimekuona.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ni lini Serikali italipa fidia kwa wananchi wa Jimbo la Tabora Mjini waliopisha ujenzi wa Reli ya *SGR* hususani kwenye Kata za Uyui na Kata ya Ikomwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ametupeleka kwenye *SGR*. Nimshukuru Mheshimiwa Hawa kwa swali lake la ziada. Serikali inatekeleza miradi ya *SGR* ya zaidi ya dola bilioni 10 nchi nzima ikijenga kilomita zaidi ya 4,000 na kuifanya nchi yetu kuwa nchi ya tano duniani kwa kujenga reli ndefu ya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza tayari Mheshimiwa Rais ameshaidhinisha fedha za kujenga reli kutoka Dar es Salaam – Dodoma, reli inafanya kazi, Dodoma – Mwanza Wakandarasi wako *site*, Tabora – Kigoma Wakandarasi wako *site*, hatuishii hapo tunakwenda mpaka sehemu ya pili ya nchi yetu kwa maana ya nchi jirani kwa wenzetu wa Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie wananchi wote wanaodai fidia nchi nzima kwenye miradi ya reli wakiwemo wananchi wa Mheshimiwa Hawa Bananga kwamba, tutakwenda kuwafikia watupe muda kidogo wakati tunafanya chambuzi mbalimbali ili tuweze kuwafikia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu haya ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa Mbunge wa Kibaha Vijijini aulize swali lake.

Na. 44

**Ujenzi wa Barabara ya Chalinze – Rufiji – Soga**

**MHE. ABUU J. HAMOUD** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya Chalinze – Gwata – Magindu – Mpalu – Utete – Rufiji – Tumbi – Boko – Soga na Kongowe – Soga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za manunuzi ya kumpata Mhandisi Mshauri atakayefanya kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara mpya ya Chalinze hadi Utete yenye urefu wa kilometa 354.9 kupitia Bwawa la Julius Nyerere zipo katika hatua za mwisho. Usanifu huu unajumuisha barabara ya Chalinze hadi Magindu yenye urefu wa kilometa 22.61. Baada ya kazi za usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa.

**MHE. ABUU J. HAMOUD:** Mheshimimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mara nyingine. Magari

mengi ambayo yanatoka Mtwara yanakwenda Lindi mpaka Dar es Salaam yanakuja mpaka Morogoro na sehemu nyingine magari yote haya yakipita njia ya Dar es Salaam yanasababisha foleni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nisisitize tu barabara hii ya Magindu – Chalinze – Utete ikijengwa kwa kiwango cha lami itapunguza kiwango kikubwa cha foleni ambayo inatokea Kibaha mpaka Mlandizi. Serikali ina mpango gani wa haraka kuhakikisha kwamba, barabara hii inajengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu nimjulishe Mbunge, Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa Mbunge wa Kibaha Vijijini kwamba, hii barabara kimsingi ni maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na aliyatoa rasmi wakati Bwawa la Mwalimu Nyerere linaanza kujazwa maji. Tulichofanya kama Wizara, kwanza, tumefanya upembuzi wa awali na ndiyo maana tumefikisha hizi kilometa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo makubwa kwenye hii barabara, yaani barabara haipo kabisa. Kwa hiyo tunakwenda kuanza barabara, sehemu kubwa ambapo tutakwenda mpaka Mloka hadi kwenda Utete. Kwa hiyo, tumlichukulia kama ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, na kikubwa ni kupunguza safari ya watu wanaotoka hasa Mikoa ya Ruvuma kule Tunduru – Mtwara – Lindi badala ya kuja Dar es Salaam waweze kupita hiyo njia ambayo itakuwa ni ya mkato na kulifungua hilo eneo la katikati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juma Mustafa.

**MHE. JUMA R. MUSTAFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kupata nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza kwenye Wizara hii ya Ujenzi. Swali langu, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya kutoka Tura, Jimbo la Igalula mpaka Mkoa wa Singida Iyumbu yenye kilometa 164? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge wa Igalula ni barabara ambayo inaunganisha mikoa miwili, lakini iko kwenye kiwango ambacho tunasema ni barabara za mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii kwa kuwa inaunganisha mikoa miwili itafanyiwa, na iko kwenye mpango kutokea Singida kwa sababu ndiyo kwenye ukubwa wa barabara kilometa 41, ziko Mkoa wa Tabora na hizo zinazobaki ziko Singida. Tumeweka kwenye mpango wa kuanza kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwenye bajeti inayokuja kama itapitishwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paschal Chinyele na Mheshimiwa Mecktridis Mdaku nimewaona.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Wakazi wa Dodoma wanafurahi sana kuona ujenzi wa barabara kutoka Dodoma Mjini kupitia Ntyuka hadi Mvumi. Je, ni lini Serikali itawalipa fidia wakazi wa Ntyuka ambao walipisha ujenzi wabarabara hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimwombe Mheshimiwa Mbunge Chinyele, baada ya hapa tuweze kuonana. Kwa utaratibu uliopo, tunapokuwa tunajenga barabara mara nyingi tunakuwa tumewalipa fidia. Tutaomba tupate hao wananchi ambao bado wana madai tuone kama walikuwa ndani ya hifadhi ya barabara iliyokuwepo ama walikuwa nje ama barabara imewafuata ili tuweze kuainisha vizuri na tuweze kuchukua hatua za kuweza kuwapatia hiyo fidia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mecktridis Mdaku, Mheshimiwa Selemani Jafo nimekuona.

**MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wangu wa Malinyi wamekuwa wakipata adha kubwa sana ya barabara kutoka Kivukoni – Lupilo kwenda Malinyi. Je, nini kauli ya Serikali kuhusu ujenzi wa barabara hii ili wananchi waweze kuondokana na adha hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamsikia vizuri barabara aliyoitaja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mecktridis rudia hilo swali kidogo.

**MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Malinyi wamekuwa wakipata adha kubwa sana ya barabara kutoka Kivukoni pale Ifakara, Kivukoni – Lupilo, Lupilo – Malinyi. Hii barabara Serikali ilisema itaijenga kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Swali langu. Nini kauli ya Serikali kuhusu ujenzi wa barabara hii, ili hawa wananchi waweze kuondokana na adha wanayoipata kipindi cha masika na kipindi cha kiangazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Ifakara – Lupilo – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Lumecha ipo kwenye mpango wa kuijenga, na ni zile tunazosema *Trunk Roads* (Babaraba Kuu). Tayari tuna Mkandarasi katika hiyo barabara ambayo ataanza kuijenga kwa kiwango cha lami kilometa 112, tukianzia Ifakara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selemani Jafo.

**MHE. DKT. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujua kwamba tuna barabara yetu na ndugu yangu Hamoud hapa ya kilometa 70.2 inayoanzia pale Mlandizi – Mnzenga – Manelumango. Sasa Upembuzi Yakinifu

umeshafanyika na hivi sasa Mkandarasi ameanza kazi katika eneo la Mnzenga kipande cha mita 300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini mpango wa Serikali katika bajeti ya mwaka huu 2026/2027 kuhakikisha tunaongeza fedha ili barabara hiyo sasa, kipande cha Mlandizi – Mnzenga kiweze kufunguka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Serikali imeshaonyesha nia ya kuijenga hiyo barabara na kwenye barabara hizi kubwa ni kuhakikisha kwamba tunazijenga kwa kiwango cha lami kadiri fedha inavyopatikana. Kwa kuwa tumeshaanza, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuongeza fedha kadiri inavyopatikana ili hatimaye tuweze kuikamilisha hiyo barabara yote kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Ujenzi ina maswali mengi, nimepokea vi-*memo* zaidi ya 50. Kwa hiyo, ninaomba tuvumiliane, taratibu taratibu tutapata kujibiwa maswali yetu.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Anne Kilango Malecela Mbunge wa Same Mashariki aulize swali lake.

Na. 45

**Ukarabati wa Mto Saseni Unaotumika kwa Umwagiliaji**

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza: -

Je, Serikali inawasaidiaje Wananchi wa Kata ya Kihurio wanaotegemea Mto Saseni kwa umwagiliaji ambao kwa sasa umeharibika sana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilifanya tathmini ya awali ya hali ya Mto Saseni mwaka 2024 ili kubaini miundombinu ya umwagiliaji inayohitajika kujengwa kwa manufaa ya wananchi wa eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya tathmini hiyo, yalionesha uwepo wa umuhimu wa ujenzi wa mabanio mawili kwa ajili ya kupeleka maji kwenye mfereji mkuu unaopeleka maji mashambani. Hadi kufikia Disemba, 2025, Mkandarasi anaendelea na kazi ya kuchimba mfereji na kujenga karavati kwa ajili ya kupeleka maji mashambani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nipate nafasi ya kuuliza swali moja, lakini pia nitoe ombi moja. Kwanza, ninaomba ku-*declare interest* Mheshimiwa Waziri kwamba ninatoka kata hii, na Mto Saseni ndiyo Mto ulionilea mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mto Saseni unajumuisha mifereji 12 ambayo ni mfereji wa Mzambo, Mkameni, Ndurumo, Mapenzi, Makalavati, Sekingere, Kimunyu, Mahanyu, Semrinde, Migombani, Lukuta, na Kitambi. Zoezi linalofanywa na Mkandarasi huyu litasaidia mifereji miwili tu na mifereji 10 itabaki haitumiki. Je, Serikali mnasema nini katika hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu baada ya swali moja ni kuomba jambo moja. Kwa kuwa Kata ya Kihurio na Kata ya Bendera ambazo zote zinatumia mto huu, takribani wananchi 15,000 wanaishi hapa wana hali mbaya sana. Serikali haioni ni vyema sasa kabla ya Bunge la Bajeti Mheshimiwa Waziri

mwenyewe pamoja na wataalamu tukaandamana kwenda Kata ya Kihurio ili mkaone Mto Saseni ambavyo una hali mbaya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Same Mashariki, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela anafanya kazi nzuri katika jimbo lake, nami ninalitambua hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie tu kwamba, nikianza na swali la pili, kabla ya Bunge la Bajeti, mimi pamoja na timu ya wataalamu tutafika katika jimbo lake na tutatembelea maeneo yote aliyoyaainisha ili tuhakikishe kwamba tunayapatia ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la nyongeza ambalo ametaka kujua kauli ya Serikali baada ya kwamba kazi hii inaendelea kule, mimi nimthibitishie tu kwamba, kupitia Tume ya Umwagiliaji Mkoa na Tume ya Umwagiliaji Taifa, ninawaelekeza sasa wafanye tathmini kwa ajili ya kuongeza *(ku-expand)* hii kazi ambayo inafanywa na Mkandarasi ili wasogeze katika hiyo mifereji mingine 10. Kazi hiyo tukishamaliza tathmini, ninaamini tutatafuta na fedha na tutaitekeleza kama ambavyo nimeahidi hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Daniel Surati.

**MHE. MARY D. SURATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii. Ni ukweli usiopingika Wizara ya Kilimo chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inafanya kazi nzuri ya kuleta maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wangu wa Serengeti ninaomba kumwuliza Naibu Waziri wetu, ni lini Serikali itatatua changamoto ya Mto Mara hasa hasa eneo la Kata ya Kisaka? Kwa maana changamoto hii imekuwa ni ya kudumu na maji yanaacha njia yake na kwenda kuvamia maeneo ya kilimo na makazi ya wananchi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**MHE. MARY D. SURATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na nitashukuru kama Naibu Waziri ataungana nami kwenda Jimbo la Serengeti ili akayashuhudie mambo haya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane vilevile kumpongeza Mbunge wa Jimbo la Serengeti ameanza vizuri. Nimthibishie tu kwamba Wizara ya Kilimo sisi ni watu ambao tuna uwezo wa kutembea na kufika maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitafika katika eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliainisha, lakini tutatuma wataalamu waende wakafanye tathmini ili tuhakikishe hiyo adha ambayo ameianisha hapa tuiondoe mara moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuberi Mfaume.

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza katika Wizara ya Kilimo. Wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini tunauliza, ni kwa kiasi gani sasa Wizara ya Kilimo itaboresha Mfumo wa Stakabadhi katika Ghala au kuwapelekea mfumo mbadala? Kwani mfumo huu kwao umekuwa hauna tija, unachelewesha malipo yao, lakini hata bei ya mazao yao imekuwa chini ukilinganisha na gharama wanazoingia katika uzalishaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimemsikia Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini na nimweleze tu kwamba Mfumo wa Stakabadhi ya Ghala ni moja ya Mfumo ambao umewasaidia sana wakulima. Tunakiri kwamba zipo baadhi ya changamoto na sisi kama Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara tumekuwa tukihakikisha kwamba hizi changamoto tunazitoa ikiwemo kufika katika hayo maeneo na kutoa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na mahitaji ya dharura, niseme tu kwamba, nitawatuma Wataalamu wa Stakabadhi ya Ghala wafike katika eneo lako, waweze kuzungumza na wakulima na vyama vya ushirika, na waweze kubainisha zile changamoto ili tuhakikishe kwamba tunazipatia ufumbuzi. Ninaamini katika mazungumzo tunaweza tukafikia katika makubaliano ambayo yatakuwa na masilahi kwa pande zote mbili.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Morris Joseph Makoi, Mbunge wa Moshi Vijijini.

Na. 46

**Pembejeo za Ruzuku kwa Wakulima wa Kahawa Moshi Vijijini**

**MHE. MORRIS J. MAKOI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatimiza ahadi ya kutoa pembejeo za ruzuku kwa wakulima wa kahawa Moshi Vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kuanzia msimu wa mwaka 2022/2023, Serikali imekuwa ikisambaza mbolea kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku kwa mazao yote nchini ikiwemo zao la kahawa. Aidha, katika msimu wa mwaka 2025/2026 wakulima 125 wa Moshi Vijijini wamenufaika kwa kununua tani 1,685.85 za mbolea kwa mpango wa ruzuku. Vilevile, Serikali kupitia Bodi ya Kahawa Tanzania na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania inatekeleza mpango wa kuzalisha na kusambaza miche bora ya kahawa kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2022/2023, 2023/2024 na 2024/2025, Serikali imesambaza bure miche 735,313

yenye ukinzani wa magonjwa ya Chule buni na Kutu ya Majani kwa wakulima wa zao la kahawa Moshi Vijijini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Morris Joseph.

**MHE. MORRIS J. MAKOI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Serikali, na kwa kuwa muda huu wananchi wote wa Jimbo la Moshi Vijijini wapo pembeni ya luninga zao wakifuatilia mjadala huu, hasa kwa sababu suala la ruzuku ya pembejeo ya kahawa, ni suala muhimu sana kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kwamba Naibu Waziri aliwahi kufanya ziara katika jimbo lile na kuzindua mpango wa kugawa miche bora ya kahawa milioni moja ambapo wananchi wale wa kata za *Old Moshi* Magharibi*, Old Moshi* Mashariki, Kibosho Magharibi, na kata nyingine za Tarafa ya Kibosho pamoja na Uru wanasubiri usambazaji wa miche ile ambayo mpaka sasa hivi bado haijapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali, je, Waziri anatuambia ni lini Serikali itakamilisha ahadi hiyo ya kusambaza hiyo miche milioni moja ili wananchi wa Jimbo la Moshi Vijijini waweze kuotesha miche hiyo hasa wakati huu wa msimu wa masika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Kiwanda cha Sukari cha *TPC* ni miongozi mwa viwanda ambavyo vinaendesha vizuri kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari katika kiwango cha Kimataifa. Kiwanda hicho kwa sasa kinajenga viwanda ndani ya mradi ule kama viwanda vitano ikiwemo kiwanda cha mbolea *soft,* umeme na viwanda vingine vya *spirit* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa Waziri atuambie Serikali ina mpango gani kuanza kujenga skimu ya umwagiliaji katika Kata ya Arusha Chini, kata ambayo wananchi wake wanazunguka kiwanda ili wananchi wale waweze kulima miwa

waweze kuuzia kiwanda kama wakulima wa nje waweze kujipatia mapato na kupunguza umaskini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Vilevile, nimpongeze Mheshimiwa Morris Makoi, Mbunge wa Moshi Vijijini, kwa maswali yake mawili ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza ni kweli mwaka 2024 Julai, mimi mwenyewe nilikwenda katika Jimbo la Moshi Vijijini na tulizindua mpango wa kugawa miche bora ya kahawa ya milioni moja. Mpaka sasa tumeshatoa miche 735,000 kama ambavyo nimejibu katika swali la msingi na zilizobaki ni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara tunakiri kumekuwa na mwamko mkubwa sana wa wakulima kuhitaji miche ya kahawa ambayo inatolewa kwa ruzuku, yaani kwa maana ni bure kwa wananchi wote. Nimwahidi tu kwamba tumekubaliana kwamba katika mwaka unaokuja tutaongeza uzalishaji wa miche ili tuhakikishe kwamba tunafikia yale malengo yote ambayo tumeahidi katika maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ni kuhusiana na kujenga mradi wa umwagiliaji katika Kata ya Arusha Chini. Nimwambie tu kwamba tulishafanya tathmini katika eneo hilo, sasa hivi tunachokifanya ni kutafuta fedha ili tuanze ujenzi wa mradi wa umwagiliaji katika hilo eneo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimwia Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kuniona.

Mheshimwia Mwenyekiti, nimshukuru sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri, kupitia Wizara ya Kilimo, kuweka ustawi mzuri wa kuinua zao la kahawa

katika Wilaya ya Karagwe na Mkoa wa Kagera kwa ujumla. Tumeona bei zikiongezeka kwa msimu mfululizo, na jambo hili jema limetoa hamasa kubwa kwa wakulima wa kahawa kutaka kulima kahawa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini mpango wa Wizara ya Kilimo kuhakikisha wakulima wa kahawa wanapata miche kwa wakati ili kuinua zao la kahawa, ikiwemo kuwapelekea vitalu angalau kila kata ili kupunguza foleni kubwa ya kugombania miche ya kahawa kipindi cha kilimo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimpongeze vilevile Mheshimiwa Bashungwa, Mbunge wa Karagwe kwa kufuatilia zao la kahawa ambalo ni miongoni mwa mazao yanayojenga uchumi wake katika jimbo lake na halmashauri yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo ninaweza nikawaambia watu wote ama maeneo yote wanaotokea katika zao la kahawa, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshamwelekeza Waziri wa Kilimo, Comrade Daniel Chongolo kwamba kuanzia msimu unaokuja katika fedha zinazotokana na mfuko wa maendeleo ya kilimo ambao tulipitisha hapa mwaka juzi 2024 kwa sheria yako ya Bunge sehemu ya fedha zile zitengwe kwa ajili ya kuzalisha miche bora ya kahawa na miche hiyo igawiwe bure kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kahawa sasa imekuwa moja ya zao ambalo linaleta fedha nyingi za kigeni. Kwa hiyo, kutokana na maelekezo hayo ya Mheshimiwa Rais, sisi tunakwenda kulitekeleza na tutaongeza uzalishaji kutoka miche ambayo tunazalisha sasa 20,000,000 kwa mwaka. Ninafikiri tuta-*double* ama tutakwenda mara tatu zaidi katika msimu unaokuja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, nimekuona.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kuniona. Mheshimiwa Naibu Waziri, Wilaya ya Lushoto inalima mahindi na ndiyo zao linalotegemewa kwa chakula mara moja tu kwa mwaka na hulimwa tu kipindi cha vuli. Mwaka huu hawajapata mvua kabisa kiasi ambacho hawategemei kupata mavuno yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa na utaratibu wa kupeleka mbegu za muda mfupi hasa kwa kipindi cha masika. Je, umeandaliwa mkakati au mpango maalumu kwa ajili ya kuongeza mbegu za kupeleka kama ngano kwa ajili ya ku-*rescue* kipindi cha masika wananchi waweze kuepuka na njaa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Vilevile, ninampongeza dada yangu, Mheshimiwa Husna Sekiboko kwa swali lake zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja la uhakika, sisi kama Wizara tunafanya tathmini na kuangalia mwenendo wa mvua na hali ya hewa yote kwa ujumla. Lengo letu kubwa ni kuhakikisha tu kwamba hatuwezi kukutana na majanga ambayo tunaweza tukakabiliana nayo sasa hivi. Miongoni mwa hatua ambazo tumekuwa tukizifanya ni pamoja na kujiandaa na kuwa na mbegu za muda mfupi ambazo zitawasaidia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana katika moja ya maelekezo ambayo Mheshimiwa Rais ameyatoa ni kuhakikisha kwa kwamba tunakamilisha miradi yote ya umwagiliaji ili kilimo chetu hapa nchini kisiwe kinategemea mvua peke yake, bali kitegemee maji. Kwa sababu, kwa kutumia mifumo ya umwagiliaji, maana yake tutakuwa na uhakika wa chakula muda wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuwathibitishie watu katika maeneo yote ambayo wana upungufu wa mvua, sisi kama Serikali tumejipanga na tunaamini tuna uwezo wa kukabiliana na

janga la aina yoyote ambalo linaweza kuja mbele yetu. Kwa hiyo, tuko tayari na mpango tunao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yohana Msita.

**MHE. YOHANA S. MSITA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kwanza ninampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini ninaomba niulize swali dogo la nyongeza kwa niaba ya Wanajimbo la Itigi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Itigi ni miongoni mwa majimbo ambayo yanalima sana zao la dengu na mwaka 2025 tumeona kuporomoka kwa kasi sana kwa bei ya dengu. Je, nini mkakati wa Serikali kuondoa adha hii ya bei ya dengu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni kweli anachokisema Mheshimiwa Mbunge wa Itigi, bei ya dengu imeshuka na sisi kama Wizara mwaka jana 2025 tulisaini mikataba na watu wa India kwa ajili ya kuendelea kuwauzia dengum na vilevile, na baadhi ya nchi za Asia ikiwemo China kutokana na mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kufunguka kwa soko hili kutasaidia kuongezeka kwa bei katika maeneo yote yanayolima dengu ikiwemo katika jimbo lake. Kwa hiyo, sisi jukumu letu ni kuendelea kulifuatilia ili tuhakikishe kwamba tunanyanyua kipato cha mkulima wa dengu, lakini na mazao mengine ambayo yanalimwa hapa nchini. Kwa hiyo, nimthibitishie tu hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deodatus Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Njombe na Mkoa wa Njombe kwa ujumla ni wazalishaji wakubwa sana wa zao la parachichi katika nchi hii, lakini uhimilivu wa zao hili

utategemea sana mpango wa Serikali kutoa dawa kwa njia ya ruzuku, yale yanayohusiana na masuala ya fangasi na dawa zinazohusiana na zao la parachichi kwa ujumla. Nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba inatoa ruzuku kwenye dawa hizi kwenye mpango wa bajeti unaokuja sasa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimpongeze Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini kwa kazi nzuri anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, moja ya mazao ambayo Wizara imekuwa ikitoa ruzuku ni pamoja na zao la parachichi na kuna aina kama tano ya viuatilifu ambavyo tumekuwa tukivitoa. Kwa mfano, *Copper Sulfate*, *Nichino*, Vuruga, *ZinMet* pamoja na *Neem*. Ni baadhi tu viuatilifu ambavyo tumekuwa tukitoa ruzuku, na vipo ambavyo bado hatujavitolea ruzuku kwa sababu vipo katika tathmini, na tukishamaliza hiyo tathmini maana yake tutaviingiza katika mpango wa ruzuku kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameliainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutajitahidi tu tuharakishe ili katika msimu unaokuja na viuatilifu hivyo viingie katika huo mfumo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakushukuru sana kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, aulize swali lake.

Na. 47

**Kuendeleza Mnada wa Magena**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza Mnada wa Mifugo wa Magena.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, ninaomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mnada wa Magena ni miongoni mwa minada 10 ya mpakani inayosimamiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambayo ilianzishwa kwa lengo la kurahisisha biashara ya mifugo kwenda nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza Mnada wa mpakani wa Magena, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inaendelea na hatua mbalimbali za kuboresha miundombinu katika mnada huo ambapo kwa mwaka 2021/2022 kiasi cha shilingi milioni 175.65 kilitengwa na kutumika kwa ajili ya ujenzi wa mazizi, kipakilio, birika la maji na vyoo na ujenzi huo ulikamilika. Aidha, ujenzi wa miundombinu muhimu iliyobaki ya ofisi ya mnada na uzio utafanyika kadiri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uwepo wa miundombinu hiyo, Mnada huu kwa sasa bado haufanyi vizuri kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo utoroshaji wa mifugo kwenda nchi jirani unaofanywa na wafanyabiashara wasio waaminifu, hivyo kusababisha mifugo michache kuingia katika mnada huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukuza biashara ya mifugo na kujenga uwezo wa kimapato kwa ajili ya kuendeleza minada ukiwemo Mnada huu wa Magena, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI, tunaendelea kuhamasisha na kutoa elimu kwa wadau kuhusu kuendelea kutumia Mnada wa Magena katika kununua na kuuza mifugo

kama ilivyokusudiwa wakati wa kuanzishwa kwa mnada huo ikiwa ni pamoja na kuendelea kudhibiti utoroshaji wa mifugo.

Mheshimiwa mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninashukuru kwa majibu ya Serikali. Ninapenda tu iingie kwenye *Hansard* kwamba Mnada wa Magena ni Mnada muhimu sana kwa sababu una *multiply effect* kwa uchumi wa wananchi wa Tarime na Mkoa wa Mara kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sababu ambazo Waziri amezitaja hapa zinazofanya mnada usifanye vizuri, sababu kuu mojawapo ni mnada ule upo mpakani. Kama alivyosema, ni mnada wa kuuza mifugo nchini Kenya ambao umewekwa siku moja ya Alhamisi ambapo *at the same time* kuna Mnada wa Mabera nchini Kenya. Kwa hiyo, wafanyabiashara wote wa mifugo wanapeleka moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kujua, ni kwa nini sasa Serikali isibadilishe ratiba ya Mnada huu uwe kama awali, uwe siku ya Jumatano ili ile minada mingine ya awali ambayo iko Mkoa wa Mara iende Jumanne na Jumatatu, ili kuhakikisha kwamba mifugo inaenda Magena halafu inaenda nchi ya Kenya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kama Naibu Waziri alivyosema kwenye majibu yake, kwamba minada yote ya mipakani imeanzishwa kwa lengo la kupeleka mifugo nchi jirani. Kwa Mkoa wa Mara na Kanda ya Ziwa, mnada wa mpakani ni Mnada wa Magena ambao unapeleka mifugo nchi ya Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini sasa Wizara yake ambayo ndiyo ina mamlaka ya kutoa vibali vya kupeleka mifugo Kenya, isihakikishe kwamba mifugo yote ambayo inaenda huko inaanzia kwanza kwenye Mnada wa Magena ndiyo kwenda nchini Kenya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Esther Matiko kwa juhudi zake za kuendelea kuwapambania wafugaji katika jimbo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza kuhusiana na siku ambayo mnada huo unafanyika, ni kweli hapo awali mnada huo ulikuwa unafanyika siku ya Jumatano ili kupisha au kufanya wafanyabiashara waweze kuuza mifugo yao siku ya Alhamisi katika Mnada wa Mabera nchini Kenya. Ni kweli kwa sasa Mnada huu unafanyika siku ya Alhamisi na hivyo umekuwa ni kikwazo kwa wadau wetu kufanya biashara kama ilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, na tutashirikiana na halmshauri husika ili kuhakikisha tunaangalia namna ya kurekebisha siku hizi. Kwa vile yeye pia ni Mjumbe wa Baraza la Madiwani katika halmashauri yake, tunaamini atatusaidia kusukuma ili kuweza kubadilisha tarehe hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la pili kuhusiana na vibali vya usafirishaji wa mifugo, Serikali kwa sasa inatumia Mfumo wa *MIMIS* (Mfumo wa Kidijiti) katika kutoa vibali vya usafirishaji wa mifugo kwa wadau wetu. Mfumo huu umekuwa rahisi kwa sababu umefanya wadau wetu waweze kuomba na kupata vibali popote walipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo huu umetusaidia sisi kuongeza mapato, lakini kupunguza utoroshaji wa mifugo. Tunaamini kwamba mfumo huu kuwepo kwake kumesaidia wafanyabiashara na wadau popote pale walipo wanaweza kupata kibali cha kusafirisha mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunatambua kama Serikali, kiu ya Mheshimiwa Mbunge ni kuhakikisha kwamba mnada huu unafanya kazi kwa tija kama ilivyokusudiwa, na ndiyo hasa hiyo

kiu yetu sisi Serikali. Kwa hiyo, nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote kwamba sisi kama Serikali tutaendelea kufanya kazi kwa bidii ikiwemo kutenga fedha ili kuhakikisha minada yote hasa iliyoko mipakani inafanya kazi kwa tija kama iliyokusudiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suleiman Arif Premji.

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa ni Wizara ya Uvuvi na kwa bahati nzuri nimepata nafasi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri ataniwia radhi, huwa tunapata nafasi chache sana za kuuliza maswali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kata ya Naumbu, Kata ya Nalingu, Msimbati na Msanga Mkuu huwa wanajihusisha na kilimo cha mwani na ndiyo tegemeo lao kubwa sana hasa akina mama. Kwa sasa, bei wanayolipwa ni shilingi 800/= kwa kilo. Je, Serikali ina mkakati wowote kwa kusaidiana na sekta binafsi ili kuboresha bei hiyo na kuwanyanyua kwenye kipato chao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Mtwara Vijijini kwa namna ambavyo anaendelea kuhakikisha kwamba wakulima wa zao la mwani wanapata tija kutokana na kilimo chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba kilimo hiki cha mwani kimekuwa ni mkombozi mkubwa sana kwa wananchi wetu hasa katika maeneo haya yanayozunguka bahari kuu, na sisi kama Serikali kwa kutambua hivyo tunaendelea kufanya bidii mbalimbali kuhakikisha kwamba wakulima wetu wa zao hili la mwani wanapata tija kama iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumechukua hatua mbalimbali ya kwanza ikiwa ni kuendelea kuwapa elimu na uelewa wakulima wetu wa zao la mwani la kuongeza thamani ya zao hili ikiwemo

kutengeneza sabuni, mafuta au unga wa mwani ambao una bei nzuri na kubwa zaidi katika soko la ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuendelea kuwahamashisha kutengeneza vikundi ambavyo kwenye soko vinakuwa na *bargaining power* kubwa zaidi kuliko mtu mmoja mmoja. Sisi kama Serikali kwa kushirikiana na wadau, tumeshaanza kuandaa mwongozo wa kuhakikisha kwamba zao hili la mwani ambalo ni zao la kibishara, tunaliingiza katika mfumo wa stakabadhi ghalani ambao utasaidia kupata tija na kupata bei nzuri kwa wakulima wetu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Injinia Ramadhani Hamza Singano, Injinia Ramadhani.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Lushoto ni miongoni mwa wilaya ambazo zinafanya ufugaji sana hasa katika Kata za Mng'alo, Makanya na Milingano, lakini kwa bahati mbaya bado hakuna mnada ambao unaweza ukawasaidia kwa ajili ya mazao yao ya mifugo je, ni lini sasa Serikali itaona umuhimu wa kutengeneza mnada wa kimkakati kwa ajili ya kuwasaidia wananchi hao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Wizara ya Mifugo na Uvuvi tutaendelea kuboresha na kuunda miundombinu mipya kila sehemu na katika majimbo yote nchi nzima kadri ya uhitaji na kadri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haiderali Gulamali.

**MHE. HAIDERALI H. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile mara ya kwanza nazungumza, niwashukuru Wanailongero

kunichagua ili niwawakilishe hapa. Pia nikushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sana Wanailongero Kata ya Makuru wanalilia mnada na josho kwa ajili ya wafugaji; na kata yetu ipo mpakani na Manyara, tupo kilomita sita tu. Kwa hiyo, tukipata huduma hiyo, wananchi wa wilaya zote watakuwa wamenufaika, naomba majibu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali zuri. Mheshimiwa Mbunge naomba tu niwahakikishie wananchi wa Ilongero kwamba tunatambua uhitaji au upungufu wa majosho na uhitaji wa uwepo wa mnada katika Jimbo la Ilongero na nikuhakikishie tu kwamba kadri ya upatikanaji wa fedha tutaendelea kuleta miundombinu hii ili kuwahudumia kwa urahisi zaidi wafugaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa majibu hayo kwa Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Saidi Salim Hamad, Mheshimiwa Mbunge wa Ole, aulize swali lake.

Na. 48

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi Jimbo la Ole**

**MHE. SALIM HAMAD SAIDI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi Jimbo la Ole kwa kuwa jimbo zima halina kituo cha Polisi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla ya kujibu swali, kwa ruhusa yako naomba uniridhie kwa vile ni mara ya kwanza kusimama na kuzungumza mbele ya Bunge hili nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kutupa uhai na uzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa namna maalum nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa heshima kubwa aliyonipa ya kuniteua kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Ninamwomba Mwenyezi Mungu aniwezeshe kuitekeleza vyema jukumu hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, sasa kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Salim Hamad Mheshimiwa Mbunge wa Ole kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatarajia kujenga Kituo cha Polisi cha Daraja B katika eneo la vitongoji Jimbo la Ole. Baraza la Manispaa ya Wilaya ya Chake Chake limetoa kiwanja Na. 61 chenye ukubwa wa mita za mraba 1429 pamoja na hatimiliki. Serikali inatarajia kutenga fedha ya ujenzi wa kituo cha Polisi toka kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Said Salim Hamad.

**MHE. SALIM HAMAD SAIDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninaomba kumwuliza swali la nyongeza kama lifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kiwanja tulichonacho kina *total square metre* 1,400 na kituo ambacho kinatarajiwa kujengwa kina ubora wa *class B, it means* kinahitajia *square metre* 250 mpaka *square metre* 300 na ardhi nyingine kubwa itabakia. Je, Serikali haioni haja ya kujenga kituo cha Polisi pamoja na nyumba za kukalia askari kwa wakati mmoja wa kwa sababu kiwanja tunacho cha kutosha? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Said Salim Hamad Mbunge wa Jimbo la Ole kwa swali lake la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali katika ujenzi wa nyumba za makazi ya askari upo katika utaratibu mwingine kinyume na mpango uliopo kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya Polisi na hilo ni mpango wa nchi nzima ambapo kwa sasa kazi ya ujenzi wa nyumba za askari inaendelea nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Pemba tumeanza pale Chakechake kwa ujenzi wa nyumba za ghorofa, lakini tunataraji kuendelea na kazi hiyo katika maeneo mengine kadri ya hali ya fedha itakapopatikana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salma nimekuona na Mheshimiwa Esther.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nichukue nafasi hii kukupongeza kwa kupata hiyo nafasi kwa kurejea tena kukalia hicho Kiti. Mwenyezi Mungu akujalie sana. Baada ya hapo, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini kituo cha afya kitajengwa katika Jimbo la Mchinga na hasa *Mchinga One* na ukizingatia kwamba kituo hiki tumehaidiwa muda mrefu kitajengwa, na hata Mheshimiwa Sagini nilikwenda naye pale Mchinga na wakaniahidi lakini mpaka leo bado. Nini kauli ya Serikali? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Salma Kikwete ambaye ameuliza swali la kituo cha Polisi, lakini nadhani nilisikia kituo cha Afya, lakini alikusudia cha Polisi. Kwa hiyo, nataka niseme tu kwamba Serikali ina mpango mkubwa wa ujenzi wa

vituo vya Polisi nchi nzima, na kwa sasa uhitaji wa vituo vya Polisi nchini ni mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna uhitaji wa vituo vya Polisi nchini vipatavyo 3,956 ambapo hadi sasa kata ambazo zina vituo vya Polisi ni 485. Kwa hiyo, tuna wastani wa kata 3,471 sawa na 88% hazina vituo vya Polisi. Mpango tulionao katika jambo hilo la kwanza, Jeshi la Polisi lilifanya tathmini ya kina kuweza kufahamu hali halisi ya uhitaji, lakini pia na matishio ya uhalifu kwa nchi nzima na hadi sasa tumebaini maeneo au kata 698 ambazo zina uhitaji wa haraka wa upatikanaji wa vituo vya Polisi, ninaamini ikiwemo na kata ambayo Mheshimiwa Salma atakuwa ameitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kata hizo 698 yapo maeneo ambayo wananchi tayari wameanza kazi hiyo kwa kujenga maboma 77, ambapo jukumu letu Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Jeshi la Polisi ni kuhakikisha kwamba tunayamaliza maboma hayo na kukamilisha vituo hivyo, na hivyo tukiweza kukamilisha maboma hayo 77 tutabakiwa na kata 621 ambazo zitahitaji ujenzi mpya wa vituo vya Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango tulionao kama Serikali katika eneo hilo, mpango wetu ni kuhakikisha kwamba tunagawa kazi hii katika hatua tatu au awamu tatu. Awamu ya kwanza tutaanza na vituo 196 ambavyo kati ya hiyo 77 ni kwa wale ambao wameshaanza hatua za awali za maboma 77 na 119 tuaanza ujenzi upya. Katika ujenzi huo, wastani wa shilingi 27,936,404,740.72 zinahitajika kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kwamba tukianza awamu hii ya kwanza, kituo ambacho kimeshatembelewa na Wizara, basi tutatahakikisha nacho kinaingia katika mpango huu wa awamu ya kwanza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Midimu nimekuona, Mheshimiwa Nabil Abdallah na Mheshimiwa Pondeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Maswa ni wilaya kongwe katika Mkoa wa Simiyu, lakini haina kituo cha Polisi. Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi Wilaya ya Maswa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge wa Maswa kwa swali lake la msingi na nimpongeze kwa kuainisha changamoto katika Wilaya ya Maswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimjibu tu kwamba Serikali ni kweli inafahamu kwamba kati ya wilaya zilizopo nchi nzima hadi sasa tuna wilaya 75 ambazo hazina vituo vya Polisi, na hili linatokana na kwamba ujenzi wa vituo vya Polisi unakwenda sambamba na kasi ya ukuaji wa uchumi na upelekaji wa maendeleo kwa wananchi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili kwa kweli Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya kazi kubwa mno na ya maendeleo katika maeneo mbalimbali ya kuhakikisha kwamba barabara zinasogea karibu na wananchi, vituo vya afya, shule na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, maana yake ukuaji wa uchumi wa watu, na pia uhitaji wa ulinzi karibu maeneo ya watu unazidi kukua. Katika hali hiyo, mpango uliopo wa Wizara kupitia Jeshi la Polisi ni kuhakikisha kwamba tunakamilisha ujenzi wa vituo vya Polisi vya Daraja A, kwa maana vile vya mkoa ambapo kwa sasa tuna mikoa mitano iliyobaki ambayo ni Mkoa wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kinondoni, Tanga, Morogoro na Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika tutakamilisha ujenzi wa vituo vya Polisi katika ngazi ya wilaya kikiwemo na hicho cha Wilaya ya Maswa ambavyo ni 75 kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikutoe hofu Mheshimiwa Mbunge, kadri ya hali ya fedha itakavyoruhusu tutahakikisha kwamba Wilaya ya Maswa nayo tunaijengea Kituo cha Polisi cha Daraja B.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nabil na Mheshimiwa Pondeza niliwataja.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nami naomba nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa nafasi ya uteuzi, lakini kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kuuliza swali moja tu dogo la nyongeza ambalo nilikuwa nataka nimwambie kuhusu vitendea kazi kwa Jeshi la Polisi kwa upande wa Zanzibar. Tumekuwa tuna upungufu wa zile *speed meter* kwa sababu kaskazini na kusini hakina, ni *only one* iliyokuwepo watu watoke mjini waende upande mmoja, lakini upande mwingine hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile alama za barabarani katika barabara nyingi za Zanzibar zimekuwa hazionekani, au sijui ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo lipo ni kuwa vitendea kazi, hata ile ya kupima *alcohol* tunaita *alcohol meter* ambapo wasababishaji wengi wa ajali wamekuwa ni walevi, lakini Polisi wanakosa ushahidi wa kumshitaki kwa kosa la kuwa huyu alikuwa kalewa; watasema tu alikuwa kalewa, lakini vipimo hamna. Je, Wizara na Serikali kwa ujumla inachukuliaje na italifanyia kazi kiasi gani? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba kwa ruhusa yako nimshukuru sana Mheshimiwa Pondeza almaarufu Amjadi, wa Jimbo la Mwembe Makumbi kwa kazi kubwa anayoifanya kwenye jimbo lake, na kwa kweli wale wananchi Mwembe Makumbi wakiwemo rafiki zangu wale wachunga punda wote wanamuunga mkono sana, hongera sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nikija kwenye hoja yake ya msingi ambayo ilikuwa inazungumzia utendaji kazi wa Jeshi la Polisi hasa kwa upande wa Zanzibar, nataka nimwambie tu kwamba Mheshimiwa Mbunge utendaji kazi wa Jeshi la Polisi kwa Tanzania nzima unafuata taratibu za Sheria, Katiba, Kanuni mbalimbali na hivyo hakuna utendaji kazi wa Jeshi la Polisi kwa Jeshi kwa Zanzibar uliotofautiana na upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kando na hilo kuhusiana na hoja ya alama za barabarani, jambo hili kwa namna fulani lina utofauti kwa sababu uwekaji wa alama za barabarani ni jukumu la Wizara ya Mawasiliano au Wizara ya Ujenzi kwa upande wa Zanzibar na Jeshi la Polisi lina wajibu wa moja kwa moja kuhakikisha kwamba alama hizo zilizowekwa barabarani zinafuatwa ili kuepusha ajali na makosa mengine ya barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vitendea kazi, nataka nitumie fursa hii kwa dhati kabisa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, hakuna wakati ambapo Jeshi la Polisi nchini limewezeshwa kwa kiasi kikubwa sana kwa vitendea kazi kuliko hii Awamu ya Sita ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Zaidi ya dola milioni 100 zilitengwa kwa ajili ya vifaa yakiwemo magari, helikopta, pikipiki na vitendea kazi vingine mbalimbali kwa ajili ya kuliweka kisasa zaidi Jeshi letu la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninaamini kwamba muda siyo mrefu tutaendelea kuona ukuaji zaidi wa utendaji au weledi wa kiutendaji katika Jeshi la Polisi unazidi kuimarika na kuhakikisha kwamba wananchi wanafurahia upatikanaji wa huduma hiyo ya usalama kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nabil nilikutaja.

**MHE. AHMED ABDALLAH NABIL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii kuchangia kuuliza swali la nyongeza kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imewekeza kwa kiasi kikubwa katika viwanja vya michezo na kiwanja kimoja kinajengwa katika jimbo langu la Dimani uwanja wa *AFCON*. Sasa je, Serikali ina mpango gani kuboresha Kituo kidogo cha Polisi Fumba ili kiweze kukidhi matajario ya uwanja huu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Pia nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Nabil, Mbunge wa Dimani kwa kuzungumzia suala la Kituo cha Polisi cha Fumba ambapo kituo kile cha Polisi kipo kwenye Daraja *2C1*, kwa maana Daraja C ni kile kituo ambacho kinasimamiwa na *OCS* kwa maana ya Mkuu wa Kituo cha Polisi na *C1* ni ile *Police Post* kama ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwamba mwaka 2027 tunatarajia nchi yetu itakuwa mwenyeji wa mashindano ya *AFCON*, na upande wa Zanzibar tunatarajia moja ya eneo litakalojengwa uwanja au linaloendelea kujengwa uwanja ambao utatumika kwa ajili ya *AFCON* ni kule Fumba, na vilevile tunafahamu kwamba wakati kutakuwa na shughuli za michezo mikubwa ya namna hiyo, kwa hiyo, ipo haja ya kuhakikisha kwamba tunakuza shughuli za kiusalama katika eneo hilo ikiwemo uimarishaji wa kituo hicho cha Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilielezea vituo 196 ambavyo tulisema tutajenga kwa upande wa Tanzania Bara vile vya kata kwa upande wa Zanzibar, mara nyingi ujenzi wa vituo vya polisi hauendani na kata, inategemeana na mahitaji. Hivyo kwa mahitaji hayo nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tunalichukua jambo hili na tutalitengea fedha mwaka wa fedha ujao ili kusudi tuweze kuweka Kituo cha Polisi chenye Daraja B ili wakati wa michezo ya AFCON tuwahakikishie wananchi usalama wao pamoja na mali zao katika eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa majibu hayo kwa Waheshimiwa Wabunge. Tunamalizia Wizara ya Afya, Mheshimiwa Naomy Duncan Mwaipopo, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 49

**Elimu kuhusu Homa ya Ini – Kigoma**

**MHE. NAOMY D. MWAIPOPO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kuhusu Homa ya Ini kwa wananchi wa Kigoma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatoa elimu kwa umma kuhusu kujikinga na Homa ya Ini kupitia Vituo vya Kutolea Huduma za Afya, Vyombo vya Habari na mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza Mpango wa kutoa elimu kuhusu Homa ya Ini katika Mkoa wa Kigoma kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kutoa elimu kwa jamii kuhusu upimaji, kujikinga, matibabu kupitia wahamasishaji wa ngazi ya jamii

(ii) Kuendela kuwajengea uwezo watoa huduma ili watoe elimu kwa jamii. Hadi sasa watoa huduma 102 wa Mkoa wa Kigoma wamepata mafunzo.

(iii) Kutoa elimu ya homa ya ini kupitia vyombo vya Habari na mitandao ya Kijamii: *Instagram, TikTok, Facebook* katika Mkoa wa Kigoma na nchi nzima.

(iv) Wizara imesambaza vipeperushi na mabango yanayolenga makundi mbalimbali katika jamii kama vijana, watu

wazima, akina mama wajawazito, viongozi wa dini, wanahabari, viongozi wa ngazi ya jamii, madereva wa magari ya masafa marefu, wajidunga, wachimba madini, wavuvi, wenzi wenye majibu pishani na watoa huduma za afya.

(v) Kutoa elimu kwa kupitia namba za bila malipo 117 na 199 ambapo washauri nasaha wamepatiwa mafunzo kuhusu homa ya ini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naomy Mwaipopo.

**MHE. NAOMY D. MWAIPOPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya pumzi, lakini pia nishukuru Halmashauri Kuu ya Chama changu cha Mapinduzi kwa kuniamini kuwa miongoni mwa wachache kuwawakilisha wanawake wa Mkoa wa Kigoma katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Kigoma kwa kunipa imani yao kuniamni kuwa mwakilishi wao katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali kuhusu ugonjwa wa ini katika Mkoa wa Kigoma. Kigoma tumepakana na nchi tatu za Jirani; Burundi, *Congo* na Rwanda, hivyo maambukizi Mkoa ule ni makubwa ukilinganisha na Mikoa mingine. Pia ninaishukuru Serikali kwa jitihada kubwa inayoifanya kwenye Mkoa wetu hasa kwenye Wizara hii ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Mkoa una hospitali ya Mkoa ambayo kiukweli imekamilika. Sasa hivi tunapima kila kitu Kigoma, hatuendi tena Muhimbili wala Bugando. Kwa hiyo, pongezi kwa Serikali, lakini pia pongezi kwa Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Serikali kwenye ugonjwa huu, niombe waongeze juhudi kwa sababu ugonjwa huu unaambukizwa sawa kabisa na maambukizi ya VVU, kwa maana ya kwamba unaambukizwa kwa kutumia vitu vyenye ncha kali, unaambukizwa kwa kupitia ngono, zile sababu zinazosababisha kupata ugonjwa wa UKIMWI ndiyo sababu zinazosababisha kupatikana kwa ugonjwa wa homa ya ini. Pamoja na elimu yanayoitoa, lakini maambukizi kwa Mkoa wetu wa Kigoma bado yako juu.

Je, Serikali ina mpango mkakati gani wa kuhakikisha ugonjwa huu unatokomezwa kabisa kwenye Mkoa wa Kigoma? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninampongeza Mheshimiwa Mbunge Naomy, Mbunge kutoka Mkoa wa Kigoma kwa kujali maisha ya wananchi wa Mkoa wa Kigoma ili wasiendelee kuathirika na ugonjwa huu wa homa ya Ini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye kwa juhudi za makusudi kabisa amewekeza kwa kiasi kikubwa sana kupambana na ugonjwa huu wa ini. Kwa sasa hivi ugonjwa huu wa ini una chanjo kwa watoto wadogo ambayo inatolewa bure. Watoto tu wanapozaliwa wanapewa chanjo hii wiki nne, wiki 10 na wiki 14 bure. Mama akijifungua tu anaingizwa kwenye mpango wa kupata chanjo.

Mheshimiwa Mwnyekiti, siyo hiyo tu, lakini ipo chanjo kwa ajili ya watu wazima. Tunafahamu chanjo hii ina miaka 25, kwa hiyo, tuko sisi ambao hatukupata chanjo ile ya utotoni, tunayo *chance* ya kuchanja tukiwa watu wazima ambao tunapata chanjo kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa huu wa homa ya ini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, kwa jitihada za makusudi kabisa za kutokomeza ugonjwa huu wa homa ya ini,

Serikali imeanzisha tiba kwa ajili ya wagonjwa hao wa ugonjwa wa homa ya ini Disemba mwaka 2025. Mpaka sasa tiba hii ya ugonjwa wa homa ya ini inatolewa kwenye hospitali zote za Rufaa za Mikoa nchi nzima hospitali 28, lakini inatolewa kwenye hospitali zote sita za kanda nchi nzima na inatolewa kwenye hospitali ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, niwahimize Watanzania wote kwamba sasa chanjo kwa ajili ya ugonjwa wa homa ya ini ipo, tiba kwa ajili ya ugonjwa wa homa ya ini ipo waende hospitalini, hospitali za rufaa na watapata matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa ugonjwa huu wa homa ya ini unaambukizwa sawa sawa na ugonjwa wa UKIMWI unavyoambukizwa. Kwa hiyo, sisi kama Wizara tutaongeza juhudi kwanza, kwa kufanya usimamizi shirikishi wa miongozo yote ya kusimamia magonjwa hayo yasiambukize na hasa kwa Mikoa ambayo imeathirika zaidi ambayo iko juu ya kiasi cha Kitaifa. *Hepatitis* Kitaifa ni asilimia 3.5 lakini iko mikoa ambayo iko juu ya asilimia 3.5 ikiwemo Rukwa, Katavi, Geita, Kigoma, Morogoro, Mara, Songwe, Tanga na Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, kwa juhudi za maksudi kabisa, tutafanya *supportive supervision* ili kutokomeza ugonjwa huu wa homa ya ini kwenye mikoa hii iliyoathirika zaidi. Nitoe rai sasa kwa Watanzania wote tujitokeze kupimwa kwa sababu wengi wetu hatujui hali zetu za *hepatitis* na imekuwa ni desturi kwamba mtu akijipima UKIMWI, basi anajua yuko salama kuendelea na ngono zembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie kwamba *hepatitis* ipo na inaambukiza sawa sawa na ugonjwa wa UKIMWI unavyoambukizwa, hivyo tuchukue tahadhari za makusudi ili tuweze kujikinga na ugonjwa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge katika maeneo yenu husika mshirikiane na Serikali kuendelea kutoa elimu kwa ajili ya wananchi wetu kwanza, wakapime ili waweze kuendelea kupata chanzo na matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho siyo kwa umuhimu, kwa jitihada za makusudi kabisa, Serikali imejumuisha huduma hizi za ugonjwa wa ini pamoja na UKIMWI, hivyo mwaka 2023 tulibadilisha kutoka *NACP* kwa maana ya *National AIDS Control Program* kwenda *(NASHCoP)* kwa maana ya *National AIDS, STIs and Hepatitis Control Programme* ili kuweka huduma hizi ziwe jumuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo suala hili ni mtambuka, Wizara zote za Serikali zimeshapata mwongozo wa kuendelea kuwaelimisha watumishi wao na kuwahudumia. Hivyo, ninatoa rai kwa taasisi zote kama ambavyo tulikuwa tukiwahudumia wagonjwa wa UKIMWI, lakini kuendelea kuwapima watumishi wetu, basi tuendelee kutumia mpango huu jumuishi ili pia watumishi wote katika taasisi zote wanufaike na huduma hii ya kupimwa, kuchanjwa na kupata matibabu kwa ajili ya ugonjwa huu wa ini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nakushukuru sana kwa majibu hayo na hilo swali ni moja tu, sijatoa ziada kwa sababu maelezo ni marefu na ni muhimu kwa Taifa letu kulijua. Kwa hiyo, naamini wananchi watakuwa wameelewa pamoja na Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umekwisha kwa leo, ninawapongeza wote ambao wameuliza maswali mafupi ya Kibunge na ndivyo ambavyo tunatakiwa humu ndani ili Wabunge wengi waweze kupate fursa ya kuuliza maswali ya Majimbo yetu. Najua tutaelewa tu taratibu wala tusiwe na haraka.

Nafahamu wengi wanatamani kuuliza maswali ya nyongeza lakini muda ni mfupi. Mtakapojitahidi kuuliza maswali mafupi ya nyongeza na Waheshimiwa Mawaziri wakaweza kujibu moja kwa moja kwenye *point* kwa ufupi, basi tutapata fursa ya kuuliza maswali mengi na tutapata majibu mengi. Naamini tutaendelea kujifunza taratibu na wala tusikate tamaa.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni wakati wa matangazo; naomba niwatangaze wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Spika ambao ni wageni watatu kutoka Jukwaa la Mabunge ya Nchi za Maziwa Makuu ambao ni Mheshimiwa Balozi Dkt. Deo Mwapinga, Katibu Mkuu Jukwaa la Mabunge ya Nchi za Maziwa Makuu. Karibu sana Katibu wetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Flaviana Charles, Mkurugenzi wa Jinsia, Wanawake na Watoto kutoka Sekretarieti ya Nchi za Maziwa Makuu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Emmanuel Ngisa, Mtumishi kutoka Sekretarieti ya Nchi za Maziwa Makuu, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni waliokaa Jukwaa la Spika, wengine ni mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge na Waziri Mkuu wetu ambaye ni Ndugu Saidi Mrisho Mpoto, msanii kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibu sana Ndugu Saidi Mrisho Mpoto. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Mbunge kutoka Bunda Mjini pamoja na wageni wengine wote ambao wamekuja.

Wageni kutoka Bunda Mjini karibuni sana katika Bunge letu, pia wageni wengine wote ambao mmekuja leo hii kwa ajili ya mafunzo, karibuni sana katika Bunge letu.

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hotuba ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa Ufunguzi Rasmi wa Bunge la Kumi na Tatu, Tarehe 14 Novemba, 2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu kwa hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, atafuatiwa Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo na Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya jiandae. Karibu Mheshimiwa Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Kama tulivyosikiliza hotuba ya Mheshimiwa Rais Tarehe 14 mwaka 2025, utagundua kwamba alikuwa anatoa Dira na Mwelekeo wa Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. Hilo ndiyo liko kwenye hotuba yake. Jambo la pili alikuwa anaeleza miaka mitano ya kwanza ya kutekeleza Dira yetu ya Maendeleo ya mwaka 2025 - 2050. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi, yaliyomo humo yanagusa sehemu tatu: kwanza, Uchumi; pili, ni ajira; na tatu, ni ustawi wa jamii au ustawi wa Taifa letu. Tokea tuanze mjadala huu imethibitika kwamba kila Mbunge anakiri kwamba Mheshimiwa Rais na Serikali yake wamefanya mengi sana kwenye majimbo yetu. Tunampa hongera na pongezi nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata wakati wa kampeni zetu, kila kitu kina umuhimu kwa wananchi wetu, lakini kwa miaka mitano ijayo yenye umuhimu zaidi ni vitatu: maji, umeme, na barabara. Sisi Musoma Vijijini, Mheshimiwa Rais tunamshukuru, tulimpelekea maombi na akaanza kuyashughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya kilomita 92 tumeshajengewa kilomita tano. Kuna miradi miwili pale, mmoja wa tenda ya kilomita 40 na nyingine ya Daraja la Mto Suguti, bado tunaendelea kufuatilia ndani ya Serikali na tunaomba fedha zipatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu, nitakuja kueleza umuhimu wa kutafuta vyanzo vipya vya fedha vya miradi mikubwa kama hii. Wakati Waziri wa Ujenzi akijibu karibu kila Mbunge hapa ana mradi ambao anaomba utekelezwe, lakini fedha hazitoshi. Kwa mfano, mimi barabara yangu kilomita 40 yaani nusu halafu na Daraja la Mto Suguti tunahitaji shilingi bilioni 80 litekelezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili tulichomwomba Mheshimiwa Rais akakubali ni bwawa la umwagiliaji kubwa la Bugwema na mkandarasi amepatikana, tunaomba tu Serikali iendelee kutafuta fedha ili mkandarasi aanze kazi, gharama yake ni karibu shilingi bilioni 42.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tukijadili hapa tunapaswa vilevile kuja na mawazo ya kutafuta fedha za miradi mikubwa kama hii. Miradi miwili tu ya Jimbo la Musoma Vijijini naiomba Serikali ipate shilingi bilioni 120. Kwa hiyo, tuwe wavumilivu wakati tunaomba maombi haya Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea ya Jimbo, nije ambayo ni makubwa kidogo ya Kitaifa, maana yake ukweli ni kwamba hotuba ya Mheshimiwa Rais ni vizuri kuongelea Jimbo lako tu, lakini nadhani nia hapa ni kutoa ushauri wa miaka mitano na miaka 25 inayokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, dira yetu tunaanza kuitekeleza toka hii bajeti ili tutoe mapendekezo mazuri kwa Serikali, lazima kwanza tujue hali halisi ya nchi yetu na kuwa tunashughulikia wananchi. Waheshimiwa Wabunge tunavyojadili, lazima tuweke maanani wingi wa Watanzania kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tuko Watanzania milioni 71, mwaka 2030 tutakuwa Watanzania milioni 80, mwaka 2050 tutakuwa Watanzania milioni 140. Hii ni muhimu sana kwenye mipango hata ambayo tutaanza kujadili wiki ijayo, lazima ujue *population* ya Taifa lako.

Pili, ambacho tunapaswa kukijua na mara nyingi hatukijadili ni *population density,* ni watu wangapi wanakaa kwenye *square* kilomita moja? Sasa hivi ni watu 80 *per square kilometre,* 2030 watakuwa ni watu 85.4 kwa *square kilometre* moja. Mwaka 2050 watakuwa 146 kwa kila *square* kilometre.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni muhimu kuifahamu kwa sababu ardhi haipanuki, lakini tunaongelea kupanua mashamba. Kwa hiyo, ardhi inapungua, watu wanaongezeka, ina maanisha hata mipango yetu ya mashamba lazima ibadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine cha muhimu cha kuweka maanani ni jinsi ambavyo watu wanahamia mijini, *urbanisation rate* kwa Tanzania ni kubwa sana hata duniani, ni asilimia tano. Makadilio ni kwamba tukifika 2050 Watanzania wengi watakuwa wanakaa mijini, kwa hiyo, 50% mijini na 50% vijijini panahitaji mipango mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kwenye dira hii ambayo Mheshimiwa Rais ameieleza kwa uzuri, lazima tujue pato letu la Taifa. Kwa leo hii karibu pato la Taifa ni shilingi bilioni 90. Makisio mwaka 2030 itakuwa shilingi bilioni 140 na mwaka 2050 dira yetu inasema tutakuwa na uchumi wa *dollar* trilioni moja. Hapo lazima tukune kichwa kwa miaka 20 kutoka *dollar* bilioni 140 kwenda trilioni moja, inawezekana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kigezo kingine cha muhimu kwenye hii dira yetu tunayoijadili miaka mitano na miaka 25 ijayo, ni pato la mtu mmoja mmoja *GDP Per Capita.* Sasa hivi kwa Tanzania tumeshuka kidogo ni 1,305 *dollars per person per annum;* kugawa kwa 12 ni pato dogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2030 itakuwa *dola* 1,780 na dira inasema tukifika mwaka 2050 pato letu la mtu mmoja mmoja liwe *dola* 7,000 lakini tukiongea bila kujilinganisha na wengine tutaona tunafanya vibaya, kumbe tunafanya vizuri au tunafanya vibaya. Tunasema tunafanya vizuri, kwa kulinganisha tu, Kisiwa cha Shelisheli *GBP Per Capita* yao kwa sasa ni dola zaidi ya 21,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vipimo vingine vya maendeleo ambavyo lazima tuvitumie wakati tunatekeleza hii miaka mitano. Jambo la pili ni kigezo cha Umoja wa Mataifa *(Human Development Index),* hii ni muhimu sana, inazidi hiyo *GDP Per Capita* kwa sababu inachukua maisha ya kila mtu kwa kila siku, inachukua mambo ya afya, elimu, kipato chako na hadhi yako ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti na ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, hii nikienda haraka, mwaka 1990 kwenye hiki kipimo tulikuwa 0.368, sasa hivi *HDI value* yetu tuko 0.555. Kwa hiyo, tuko katikati hatujafanya vibaya. Wenzetu Wakenya wanatuzidi. Mwaka 1990 walikuwa 0.463 na sasa wako 0.628.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipimo kingine wakati tunajadili hii dira ya miaka mitano na ya mpaka 2050 kinaitwa *Quality of Life Index*. Hivi vipimo viwili ni muhimu sana, vinazidi vya fedha. Hii matokeo ya mwaka huu Afrika haijafanya vizuri, isipokuwa *South Africa* ndiyo iliyopata *point* 150, lakini ukilinganisha na Uholanzi ina zaidi ya *point* 200. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuko kwenye *plan of action*. Mapendekeo yangu sasa kama hali halisi ni hii. La kwanza, kwenye elimu, ni lazima tuwe na elimu iliyo bora kwenye ngazi zote, *(quality education at all levels*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili,…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia, mengine nitaongea wiki ijayo, nipe muda kidogo nimalizie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kuweka mkazo kwenye masomo ya *STEM (Science, Technology Engineering* na *Mathematics)*. Hii *STEM* ndiyo imechukua kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine tukitaka kufanikiwa ni lazima tuwe na vyuo vya aina tatu: cha kwanza ni chuo kikuu ambacho kinafundisha nadharia, halafu na *practical's, na research*. Sasa sisi tunalalamika chuo chetu, nadhani katika haya matatu vyuo vyetu vinang'ang'ania nadharia, hakuna *practicals,* wala *research. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chuo cha pili ambacho tunapaswa kuwa nacho ni ambavyo vinaitwa *polytechnics,* kama ilivyokuwa Dar es Salaam *Technical College* ya zamani. Hivyo vyuo ni lazima uwe navyo. Cha tatu, ni hivi *vocational* kama tulivyonavyo vya *VETA*. Hii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la mwisho kwa upande wa elimu, kwa sababu sasa wanafunzi watasoma hadi kidato cha nne, ni lazima tuwapeleke wengi *high school,* yaani kidato cha tano na sita. Kwa hiyo, Wizara lazima ianzishe *high school,* izishushe hadi nyingine ziwe za halmashauri. Hivyo ndivyo tutakakavyowasomesha vijana wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la pili ni la kilimo, kwa sababu ndiyo ajira. Pia tutumie mbolea nyingi. Sasa hivi tunatumia takribani kilogramu 20 kwa hekta moja ya kilimo, lakini mapendekezo tutumie kilo 50 kwa hekta moja inayolimwa. Tuboreshe kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni *irrigation.* Ninashukuru jana tumeona yale magari, tupate maji kutoka kwenye visima, tupate maji kutoka kwenye maziwa na kwenye mito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakaribia kumalizia. Kwa mfano, hili Bwawa ninaloliongelea la Bugwema litatumia maji ya Ziwa Victoria, na sisi ambao tuko karibu na Ziwa Victoria tunachukua vipimo. Sasa hivi ujazo wa Ziwa Victoria ni *cubic meter* 2,000,007,060; na mwaka 2050 tumeshapiga mahesabu itafika takribani 3,000,000,300. Kwa hiyo tutumie kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni uchumi wa kijani *(green economy)*. *Green economy* itaendana na utumiaji wa umeme. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge tunaongelea umeme, lakini matumizi yetu ya umeme ni madogo kweli kweli. Inabidi kufanya mapinduzi ya uchumi mkubwa. Kwa sababu *electricity consumption per capita,* umeme tunaoutumia mtu mmoja mmoja kwa mwaka ni *units* 170. Ukizigawa kwa 12 hatutumii umeme Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya wako *units* 300. Linganisha na China ambao wako zaidi ya *units* 7,000 na india zaidi ya *units* 1,500. Kwa hiyo, siyo ajabu sisi kwenda China na India kununua vitu. Wao wanatumia umeme mwingi, sisi hatujatumia umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nitawaelekeza, hili ninaomba niache mpaka wiki ijayo. Vyanzo vipya vya kupata fedha za kutekeleza miradi mikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie hii ni *point* muhimu kweli kweli. Wabunge tutazunguka tutawalaumu Mawaziri, tutamlaumu kila mtu, lakini utekelezaji wa miradi mkubwa unahitaji mpangilio mwingine kabisa wa kifedha. Nitaongea wiki ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe nimetoa mfano, kwamba ninahitaji shilingi bilioni 140, jimbo moja, miradi mwili, fedha zitatoka wapi? Huo utakuwa mchango wangu wa wiki ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo. Nilimtaja Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya na Mheshimiwa *Engineer* Fadhili Sandali, wajiandae.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha leo hii kuwepo hapa katika Bunge hili Tukufu. Pili, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia hapa, niwashukuru sana wapiga kura wangu wote wa Jimbo la Chamazi kwa kunichagua kwa kura nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ushindi mkubwa alioupata katika ule uchaguzi wa mwezi Oktoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kushukuru, kwa sababu tunaambiwa; *Man lam yashkurin-naas, lam yashkurillaah* (asiyemshukuru mwanadamu mwenziwe hata Mwenyezi Mungu hawezi kumshukuru). Tumshukuru sana Rais wetu, Mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan, kwani ndani ya miaka minne yake iliyopita kazi kubwa zimefanyika katika lililokuwa Jimbo la Mbagala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia na katika kipande kilichobaki ambacho mimi nakiongoza cha Jimbo la Chamazi, tunamshukuru sana. Mambo makubwa aliyoyafanya ndani ya Jimbo la Chamazi ndiyo ambayo yamenifanya mimi kama Mbunge kupata kura nyingi za kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi majimbo yanapoanzishwa jimbo jipya linakuwa na uhaba wa miradi ya maendeleo, lakini niendelee kumshukuru wakati ninaingia katika jimbo jipya hili la chamazi miradi ya kutosha ya maendeleo

Mheshimiwa Rais, ametuandalia kitu ambacho kwa kweli Wanachamazi wanaendelea kutoa shukrani za dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muhtasari tu, katika elimu msingi tumejenga shule mpya tano za msingi, na kati ya shule hizo shule mbili za ghorofa. Shule moja sasa hivi inajengwa ya ghorofa tano ambayo itakuwa na madarasa zaidi ya 52. Shule ambayo inaenda kuweka historia katika nchi yetu ambayo hakuna shule mpya iliyojengwa kwa kuanza kuwa na madarasa mapya 52. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Katika elimu sekondari tuna shule nne mpya za sekondari. Kati ya hizo, tunazo shule mbili za ghorofa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa upande wa afya jimbo letu sasa la Chamazi jimbo jipya linayo hospitali ya wilaya ambayo ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Ninaamini kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Rais hospitali ile ya wilaya sasa inaenda kumalizika kwa haraka iwezekanavyo. Zahanati mpya tatu na vituo vya afya vitatu vimejengwa, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa barabara., barabara zimejengwa zile za *TANROADS* na zile za *TARURA*. Katika upande wa *TANROADS,* barabara ile ambayo inatoka Mbande Kisewe Namsongola, tumshukuru Mheshimiwa Rais, juzi mkandarasi amerudi *site* na anaendelea na ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada hizi zote za Mheshimiwa Rais alizozifanya na mipango yake ambayo ameieleza katika hotuba aliyoitoa hapa Bungeni ni dhahiri na sisi kama Wabunge tunao mchango mkubwa wa kuhakikisha hotuba hii sasa inatafsirika kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amezungumzia suala la Bima ya Afya kwa Wote katika hotuba hii. Bima ya Afya kwa Wote ni jambo jema sana, na Waziri wa Afya juzi amezindua na ametutangazia vitita. Ni jukumu letu sasa Waheshimiwa Wabunge kwenda kuwaelimisha wapiga kura wetu wote wajiunge na hii Bima za Afya kwa Wote, kitu ambacho kitasaidia

kupunguza gharama na kuondoa malalamiko ambayo yamekuwa hayana msingi ambayo yamekuwa yakizikumba hospitali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amezungumza na ana nia ya dhati ya kujenga miradi mikubwa katika maeneo yetu. Moja ya jukumu ambalo tunalo kama Wabunge na Mawaziri ni kuongeza vyanzo vipya vya mapato. Kipo chanzo kimoja cha mapato, ninaamini hatujakikusanya vizuri na hatujakisimamia vizuri. Tukikisimamia vizuri, tutaziwezesha halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna chanzo cha *City Service Levy*. Halmashauri kupitia *TARURA* zinapotangaza barabara, wakandarasi wanaojenga zile barabara wanalipa kodi hii kwa halmashauri. *TANROADS* chini ya Wizara ya Ujenzi, wakandarasi wote wanaojenga barabara kubwa wakimaliza, hawalipi kodi. Pia na Wizara ya Uchukuzi kwa upande wa T*ANROADS* tumeshuhudia mwendokasi umejengwa, halmashauri zilizo karibuni na ulipopita mwendokasi hawajalipwa kodi hii. Niombe sana Mawaziri, moja ya jukumu la Waziri wa TAMISEMI ni kuzitafutia fedha halmashauri. Hizi fedha zimezungumzwa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumwombe sana Waziri wa TAMISEMI katika kumuunga mkono Mheshimiwa Rais kuhakikisha miradi hii inatekelezwa, basi na jambo hili la ulipaji wa *City Service Levy* ufanyike kama vile sheria inavyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika kuhakikisha kwamba miradi hii ya maendeleo inatekelezeka, tayari tumeshaona mwarobaini mkubwa ni kupata fedha za kutosha. Kwa hiyo, kila mahali ambapo panahitajika pawe na mchango wa kuiwezesha Serikali kupata fedha, niwaombe Waheshimiwa Wabunge tutolee macho ili kuhakikisha kuwa fedha zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala zima la kodi ya pango la ardhi. Tunaendelea kupima maeneo, lakini yale yaliyopimwa asilimia kubwa hayalipi kodi ya pango ya ardhi. Ninamwomba sana Waziri wa Ardhi pamoja na sisi Wabunge na halmashauri

zetu tuhamasishe na kuwaelimisha wananchi wetu ili waweze kulipia kodi hizi za pango ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, pia halmashauri zetu tuzihamasishe, zitafute namna bora ya kuwawezesha wananchi waweze kupima maeneo yao ili mwisho tuendelee kupata kodi ya pango la ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwa kufanya hayo yote, ni matarajio yangu miradi mikubwa ya maendeleo itaenda kutekelezeka na miradi ambayo ipo chini ya halmashauri ikiwepo kujenga madarasa, kujenga vyumba vya walimu nayo itatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini ile changamoto kubwa ya upatikanaji wa majisafi na salama katika Jimbo la Chamazi, kama tutaongeza nguvu za kutosha katika kutafuta fedha naamini na changamoto ya upatikanaji majisafi na salama itakwenda kuwa historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Prof. Muhongo amesema kwamba tutajadili kwa kina namna bora ya Serikali yetu kuendelea kupata mapato katika hotuba mbalimbali zinazokuja, ikiwepo ile ya mpango. Katika Bunge la Bajeti niwaombe sana Wabunge wenzangu, pamoja na kuomba miradi ya maendeleo, lakini pia tujikite kuainisha vyanzo vipya vya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vya mapato vipo vingi. Tukijikita katika kuviainisha na viongozi wetu wa halmashauri na Mawaziri wakajikita katika kuvikusanya, ninaamini huko tunapokwenda tutaweza kutatua tatizo kubwa la utekelezaji wa miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, nikushukuru na wewe mwenyewe kwa kuchaguliwa, na pia nakupongeza. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo. Nilimtaja Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, Mheshimiwa *Engineer* Fadhili Sandali Chilombe, na Mheshimiwa Selemani Jafo, wajiandae.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kupata fursa ya kuchangia hotuba nzuri sana ya Mheshimiwa Rais wetu mpendwa. Kwanza ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kunipa uhai, afya njema na kutugawia wote humu ndani afya njema pamoja na Watanzania wote. Zaidi ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa kurudi tena katika Bunge hili kwa awamu ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninamshukuru Mheshimiwa Rais pamoja na Kamati Kuu na chama changu pendwa Chama cha Mapinduzi kwa kuona ni namna gani nina uwezo tena kurudi tena kuwa sehemu ya mchango wa kujenga Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni fursa ya kipekee sana sana kwangu, na ninaomba nishukuru sana kwa sababu nikisema sana, ninaweza nikatoa machozi, lakini sina namna nyingine zaidi ya kushukuru na kumwombea Mheshimiwa Rais. Mungu ampe maisha marefu, Mungu ampe afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo ambayo leo nimesimama hapa mbele, nizungumze, nitazungumza kutoka moyoni mwangu. Kwa namna ambavyo Mheshimiwa Rais amefanya kampeni zake, amezunguka Tanzania nzima na mambo aliyoyahubiri katika kampeni zake yamenifanya nisimame hapa leo. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba siyo hotuba pekee iliyonifanya nisimame hapa, lakini kwa namna ambavyo aliendesha kampeni zake zile, kwa namna ambavyo aliguswa na matatizo ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akili kubwa inazungumza matatizo ya watu, akili za kawaida zinazungumza matatizo ya mtu binafsi. Mheshimiwa Rais amethibitisha hilo kwa namna alivyokuwa

anaguswa na maeneo yanayohusu watu zaidi katika kampeni zake. Amegusa maeneo ya elimu, afya, madini, kilimo, nishati, maji, na maeneo mengine mengi kwa mifano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa ninapenda zaidi, kwa namna ambavyo nilipata fursa ya kuzunguka kidogo katika zile kampeni, niliona namna gani Wabunge walikuwa wakinadi sera na kushukuru miradi waliyopelekewa katika maeneo yao kwa kuitaja kwa takwimu na kuizungumza kwa mifano. Wale watu walikuwa wakishangilia namna gani ambavyo zile fedha ambazo tulikuwa tunazipitisha hapa zimekwenda kufanya kazi kule chini. Eeeh, Mheshimiwa Rais ahsante sana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo moja ambalo Mheshimiwa Rais amezungumza katika hotuba hii, ameguswa sana na eneo la wanawake na vijana, amezungumza mazuri mengi katika wanawake na vijana. Mimi kama kijana nikasema, mimi bado ni kijana jamani, na ndiyo kwanza nina miaka 39. Pamoja na kwamba ni Mbunge wa Wazazi, lakini bado ni kijana. Nina uwezo wa kuzungumza mambo ya vijana kwa sababu ni mzazi, ninakwenda kuelezea maeneo ya vijana pamoja na wanawake kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake amegusia namna gani anaenda kuboresha eneo la kilimo kwamba ni namna gani anavyotamani kilimo biashara na mkulima awe mwekezaji kwa kwenda kuongeza thamani au mnyororo wa thamani. Maana yake hii kwa vijana na wanawake ni fursa, tuikimbilie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni fursa nzuri kwa sababu tutaenda kulima kwa kutegemea pembejeo safi, kwa kutegemea mbegu nzuri za kisasa na kwa kutegemea umwagiliaji mzuri kwa sababu mwaka jana 2025 Bunge lililopita tulipitisha bajeti hapa kwa ajili ya kutengeneza mabwawa ya kumwagilia maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kuona namna gani Mheshimiwa Rais ana maono ya kuijenga Tanzania yetu. Hata hivyo, hii siyo tu kwa ajili ya biashara, itatupa utoshelezi wa

chakula katika Taifa letu na vilevile tutaweza kuwa na fursa ya kuuza nje zaidi kama kilimo kitaboreshwa zaidi na zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona eneo lingine ambalo amegusia ni utalii. Mheshimiwa Rais ameonesha nia ya dhati hata katika filamu yake ya *Royal Tour,* ameonesha namna gani anatamani utalii ukue katika hii nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona fursa katika eneo hili, na zaidi amezungumza kwamba atawezesha vyuo vya utalii ili viende ku-*produce* watu ambao wataenda kusomea masuala ya ukarimu. Maana yake ni nini? Hoteli nyingi zinaenda kujengwa. Watalii watakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, wanaenda kuweka vile vivutio kuvitaja kwa pamoja ili watu wakija Tanzania watumie muda mwingi au siku nyingi waweze kutembea Tanzania yetu na kufurahia utalii wetu. Hii nayo ni fursa kwa vijana. Maana yake kama utalii unakua, maana yake fursa za kazi za madereva, lakini fursa za wale wanaokarimu wale wageni ni fursa nzuri sana kwa vijana leo hii ambao wanalalamika ukosefu wa ajira, maana yake hii ni ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Rais ameendelea kusema mikopo ya 10%. Maana yake ni nini? Ametengeneza shule za amali na vituo vya *VETA*. Namna gani ule ujenzi ambavyo unaendelea katika hizo wilaya zetu unaenda kutengeneza *product* nzuri sana kwa vijana. Hii ni fursa ya kwenda kuchukua mikopo na kuwezesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kamati iliyopita au Bunge lililopita ninakumbuka nilienda eneo moja linaitwa Arumeru. Nilikuta vijana kadhaa pale wameungana kwa *professionals* tofauti tofauti wameweza kutengeneza kikundi ambacho ni kizuri sana kwa ajili ya kuongeza kipato chao binafsi. Hii ni fursa nzuri sana kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ina maana tukiwa na vituo au vikundi kama hivi tunaenda kuboresha matokeo mazuri ya kipato

chetu na tunaweza kuishi vizuri kwa namna ambayo inapendeza na nchi yetu inazidi kwenda kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, aligusia suala la wasanii. Tunaenda kutengeneza mambo mazuri kwa wasanii. Bunge hili twende tuka-*focus* tunyanyue vipaji kwa sababu kuna fursa kubwa ya ajira katika eneo la wasanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kizuri zaidi amemteua kaka yangu Mheshimiwa Makonda, wote mnamfahamu ari na nguvu yake, uwezo wake, namna yake ya kufanya kazi na namna anavyotamani matokeo ya haraka. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake habari, sanaa na michezo inaenda kukua kwa kasi na kwa haraka zaidi kwa sababu Mheshimiwa Rais ameonesha namna gani anapenda wasanii katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameonesha namna gani anapenda wanamichezo katika dunia hii, anawapenda sana wanamichezo, na tumeona mifano mingi kwa wanamichezo. Kwa hiyo, hii ni fursa sana kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka pia Bunge lililopita tulipitisha hapa ujenzi wa viwanja kwa ajili ya *AFCON.* Jamani hii ni fursa nzuri ambayo tunaenda kuitengeneza Tanzania yetu kuwa na historia ambayo haikuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake leo hii mtoto wangu ametamani kuwa mcheza mpira na anaamini mpira unaenda unalipa. Anasema mama mimi ninaenda kuwa Tajiri, ninaenda kukujengea nyumba na kukununulia gari kwa ajili ya mpira. Kwa nini mtoto wangu mdogo ameweza kuzungumza namna hiyo? Kwa sababu anaona namna gani watu walivyohamasika katika michezo *especially* mpira wa miguu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi Mwanayanga kwa kweli ninaheshimu sana mapenzi ya Mheshimiwa Rais. Kwa namna ya kipekee ninaomba nimsitiri na kumshukuru sana. Mheshimiwa Rais

ni mfano wa kipekee, sio kiongozi mbinafsi, ni kiongozi ambaye ameachiwa miradi ya kimkakati na ameiendeleza bila kuangalia alama yake ipi ataiacha katika nchi hii? Huu ni mfano mzuri sana kwa uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwingine angeweza kuanzisha mambo mengine kabisa, lakini amesema nitahakikisha miradi niliyoikutakuta kwa asilimia chache nitaimaliza. Nitatengeneza heshima ya aliyenitangulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni heshima ya kipekee sana katika nchi hii. Kukuta mtu ambaye anaamini katika kazi za wengine, kwa sababu angeweza kusema labda mimi ninatamani kujenga kitu fulani ili na mimi nijitengenezee alama, ili huko mbele waseme fulani alivyokuja alianzisha hiki na akafanya hiki, lakini aliyeanzisha ni mwingine na yeye ameweza kuendeleza kwa asilimia kubwa zaidi. Hii ni heshima kubwa. Ni mapenzi makubwa ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mbunge humu ndani sitaacha kusema. Sitaacha kusimama naye, ameonesha ume-*focus* pamoja na yote, lakini *focusing* yake imekuwa kubwa sana kwenye matatizo ya wananchi. Bunge hili Tukufu ninaliomba sana katika bajeti inayokuja tu-*focus* sana kwenye maeneo ambayo wananchi wanaguswa. Sana sana eneo la watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumza sana kwenye Bunge la Bajeti. Ninaomba nishukuru kwa fursa hii, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya. Nilimtaja Mheshimiwa *Eng.* Fadhili Sandali Chilombe, Mheshimiwa Selemani Jafo na Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas wajiandae.

**MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Ninaomba niungane na wenzangu walionitangulia kwamba kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama kwenye Bunge hili, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu

kwa kunipa fursa ya kuwepo hapa kwenye sehemu muhimu ndani ya hii nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwa namna ya pekee kabisa nikishukuru Chama cha Mapinduzi kwa kuniamini na ninaomba niwahakikishie kwamba nitafanya kwa kadiri Mungu atakavyoniwezesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwasahau mabosi wangu wapigakura wa Jimbo la Tunduru Kusini walioanza kunichagua kwenye kura za maoni na hatimaye kwenye Uchaguzi Mkuu nikaweza kuingia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninaomba moja kwa moja niungane na Wabunge wenzangu kwenye kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya toka huko ameanza kuchaguliwa au kupewa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 22 Septemba, 2025 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alikuwa Tunduru, alikuja kwenye kampeni kuomba kura zake na kutuombea kura sisi. Akiwa pale nilisema maneno. Nilimwambia nitayarudia hapa. Sisi watu wa Tunduru Kusini tumeguswa naye. Tulimuahidi kwamba tutampa kura za kishindo na tulifanya hivyo na ahadi hiyo ilitokana na ukweli kwamba yapo mambo tuliyaona yakitokea kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amefanya mambo makubwa ya kihistorioa katika lile jimbo. Nitayasema machache. Sisi ni wakulima, tunalima mazao mengi, lakini moja ya zao kubwa tunalolima ni korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha uongozi wake tulipokea pembejeo za aina mbili ambazo zilisaidia ku-*boost* zao la korosho kwenye eneo lile. Tulipokea pembejeo ya *sulphur* tani 28,809 sawasawa na mifuko 992,360 yenye thamani ya shilingi bilioni 44.656.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, Mheshimiwa Rais alituletea dawa za maji zenye ujazo wa lita 1,384,101 zenye thamani ya shilingi bilioni 20.716 na kufanya jumla ya fedha zilizoingia mifukoni mwa wakulima kwenye eneo lile kufikia shilingi bilioni 65.117.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uwezeshaji huo, zao la korosho kwenye eneo letu lilipanda kutoka tani 15,000 hadi tani elfu 39.9 na kuwafanya wananchi wa eneo lile wapate fedha zisizopungua shilingi bilioni 262.063. Hiki ni kiwango kikubwa cha fedha ambacho tumekishuhudia ndani ya utawala huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilimwambia na ambalo wananchi wa Tunduru Kusini, bado wanalikumbuka na kuliona ni uwepo wa mradi mkubwa wa umeme kwenye eneo lile. Mimi nina pacha wangu anaitwa Ado Shaibu, Mheshimiwa Mbunge, tunatoka wilaya moja; yeye yuko Kaskazini mimi niko Kusini. Jana alisema hapa, alijaribu kuchangia na kueleza juu ya uwepo wa mradi huu, lakini akatoa na changamoto ya umeme kwenye eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa maelezo ya mradi huu, ninaomba kidogo nitoe maelezo kuhusiana na maelezo ya jana ya Mheshimiwa Ado. Ni kweli kwamba Tunduru kuna changamoto ya umeme, lakini siyo kwa kiwango kile, na ninaomba niipongeze Serikali kwa namna ambavyo imekuwa ikishughulikia changamoto za umeme kwenye eneo na siyo Tunduru peke yake, bali nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za kuipongeza Serikali, pamoja na uwepo wa changamoto hizi ni kama zifuatazo: Kwa mujibu wa taratibu za kisayansi, umeme ninafikiri, kama tunavyofahamu, kwanza unazalishwa, unasafirishwa, unasambazwa, halafu unagawanywa. Sasa *line* zinazotumika kusafirishia umeme ni *line* kubwa zinaitwa *transmission line* ambazo zenyewe umeme unaosafiri kule ni wa msongo wa kuanzia *kilovolt* 66 kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyopo kwa Tunduru na maeneo mengine ni kwamba tunatumia *line* za *distribution* zile za *MV line* ambazo zina *kilovolt* 33 badala ya kutumia *transmission,* na hii mimi siilaumu Serikali. Ninafikiri sote tunafahamu kwamba Serikali imekuwa ikipiga hatua na imepiga hatua kubwa sana. Hii nchi mwanzo mikoa ilikuwa haina umeme, leo tunaongelea habari za vitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mujibu wa sheria za kisayansi, zinataka hivi, *MV line,* ile *line* ya *kilovolt 33* inatakiwa isizidi urefu wa kilometa 100 ili kumfanya mtumiaji apate umeme mzuri. Sasa changamoto ambayo tukonayo kwenye eneo na maeneo mengine ni kwamba, kwa sababu tunaendelea taratibu na maendeleo hayawezi kuja siku moja, Serikali ilianza kutengeneza gridi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasingeweza kusema kwamba tusipeleke umeme kwenye maeneo yote, tusubiri gridi. Hiki kitu hakiwezekani. Kwa hiyo, wakaamua kutumia *distribution line* kupeleka umeme kwenye maeneo, na kwa sababu hiyo basi, tumejikuta kwa mfano kwa Tunduru, sisi watu wa Tunduru tunapata umeme kutoka Songea kwenye Kituo cha Unangwa kilometa 261.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *line* ile haikomei Tunduru, ikitoka Unangwa inaenda kuishia Nanyumbu, kilometa 405 kutoka umeme unapotokea. Hii maana yake ni nini? *Line* ile badala ya kupeleka kilometa 100 wamepeleka hiyo kilometa 400. Hata hivyo, siyo 400 peke yake kwa sababu ile *line* inapokwenda haitembei kwenye *axis;* inatembea kwenye *axis* lakini kuna matawi yamejitokeza pembeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta kwa mfano, ukienda Mtwara Pachani pale kuna tawi limeenda huko mpaka ndani karibu kilometa 150. Yako matawi mengine ukifika Nanyumbu yanaingia kule Mtamba Swala. Kwa hiyo, ukijumlisha urefu wa ile *line* unapata karibu kilometa 1,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na urefu wa *line* hii, Serikali imefanya kazi kubwa sana kuhakikisha kwamba wananchi wa maeneo yale wanapata umeme. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba changamoto ya umeme Tunduru ni kubwa kwa kiwango hicho, lakini kutokana na hali ilivyo ndiyo maana Serikali imekuja na mradi ambao wenyewe kazi yake ni kuweka vituo vya kupozea umeme kwenye kila wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alisema juzi hapa, mradi huu upo, unakuja kwa *phases.* Kuna *phase* namba moja ambayo ina miradi 27. Serikali imetenga jumla ya shilingi trilioni 1.97 kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika. Kwa hiyo, baada ya maelezo haya, ninaomba nirudi kwenye nini ametufanyia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye eneo letu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwenye eneo letu sisi tumeletewa maajabu. Kwa nini ninasema ni maajabu? Kuna mradi katika hii miradi ya gridi imara. Tunduru tumeletewa ule mradi, kunajengwa *line* yenye urefu wa kilometa 214 kutoka Songea ya *transmission line.* Kama hiyo haitoshi, kinajengwa kituo pale cha *megawatts 120.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ninavyoongea, Mji wa Morogoro, kile Kituo cha Msamvu kinalisha Morogoro yote ikiwa pamoja na viwanda vya Mtibwa na maeneo mengine yote, lakini matumizi ya umeme pale ni *megawatts* 71 pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi Tunduru tuna matumizi ya *megawatts* nne na *projection rate* ya ukuaji wa matumizi kwenye eneo lile kwa sasa ni 0.5 *megawatts* kila mwaka. Tunakwenda kuwekewa kituo cha *megawatts* 120.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake ni nini? Kama ukuaji wa umeme utaendelea kubaki vile ulivyo, tunategemea kuwa na zaidi ya miaka 100 bila kufikiria ongezeko lolote la umeme kwenye eneo lile, lakini kwa kuwa umeme unaenda kuwekwa pale, tunaamini matumizi yataongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *projection* tunayoifikiria pamoja na kuongezeka na kwa mji ulivyo, haiwezi kuzidi *megawatts* mbili. Tafsiri yake ni kwamba kituo kile kikijengwa kinaenda kuishi pale kwa zaidi ya miaka 50 bila kufikiria nyongeza yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa muktadha huo, unaweza ukaona ni kwa namna gani Rais huyu alivyokuwa na dhamira ya kumaliza matatizo moja kwa moja kwenye maeneo. Ndiyo maana tunampongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, ninaiomba Serikali kwenye jimbo langu ninafikiri ni moja kati ya majimbo machache ya nchi hii ambayo hayana lami hata sentimita moja.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ado, taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza mwasilisha hoja, Mhandisi huyu mzoefu kwenye mambo ya umeme kwa jinsi anavyotujengea uelewa kwenye mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu mjadala huu unaendelea juu ya changamoto za umeme Tunduru, nitoe tu taarifa kwamba, nimeshakutana na Waziri mwenye dhamana sasa hivi na ametupa taarifa sahihi kwamba fedha zimeshalipwa kwa mkandarasi pale Tunduru na tunaipongeza Serikali kwa jambo hilo, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* umepokea hiyo taarifa?

**MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea kwa sababu nilikuwa ninaenda kuomba kwamba Serikali itusaidie kuleta fedha kule tumalizie mradi ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa idhini yako. Ombi langu kubwa kwa Serikali itusaidie kujenga ile barabara. Tuna barabara pale inaanzia Tunduru Mjini inazunguka mpaka kwenye Jimbo la Mheshimiwa Waziri, na jana tulikuwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumemweleza juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ile ni ya kimkakati, ilianza kutolewa ahadi na Mheshimiwa Kikwete, ikatolewa ahadi na Mheshimiwa Dkt. Magufuli, Mheshimiwa Rais tuliyenaye ameitolea ahadi na ipo kwenye ilani kila mwaka inaingizwa. Ninaomba mwaka huu isiwe historia. Mtusaidie kutujengea ile barabara. Tunashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Eng.* Fadhili Chilombe. Nilimtaja Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Dkt. Emanuel Qambaji na Mheshimiwa Kangi Lugola wajiandae.

**MHE. DKT. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mola ambaye ametupa afya na kutuwezesha kuingia katika Bunge hili la Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi yake kubwa anayoendelea kuifanya katika Taifa letu hili kwa maslahi mapana ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaomba nikupongeze wewe na timu tukianzia Spika, kwa baraka mlizozipata kutuongoza na hakika sisi tunafarijika sana. Nikupongeze Waziri Mkuu ndugu yangu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba na timu yako. Mheshimiwa Rais hajafanya makosa; amechagua watu ambao tuna imani kwamba tutasonga mbele vizuri katika miaka hii mitano kuhakikisha kwamba Ilani ya Chama cha Mapinduzi kama tulivyoinadi inaweza kufanikiwa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wazaramo tuna lugha tunasema, *zilongwa mbali zitendwa mbali,* kwamba unaweza

ukasema jambo hili na ukafanya tofauti. Ndiyo maana yake, lakini Mama Samia amedhihirisha lugha hiyo hiyo kwa upande wa pili unasema, *zilongwa zitendwa. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunajadili hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo ameitoa mwishoni mwa mwaka 2025. Jambo la kwanza, kumwamini mtu lazima kwanza ufanye rejea. Aliyoyasema mwanzo ameyatekeleza kwa kiwango gani ndiyo tuje kumwamini katika haya aliyoyasema sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ndio shahidi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipopata madaraka haya mwaka 2021, alikuja jengo hili, alizungumza mambo katika sekta mbalimbali. Alisema katika suala zima la miundombinu ya barabara. Kipindi kile upande wa *TARURA* ilikuwa inapokea wastani wa shilingi bilioni 273 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunavyozungumza, ilipofika mwaka 2024 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan eneo hilo alilibadilisha mpaka kufika shilingi trilioni 1.09. Huyo ndiye Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyasema hayo Mheshimiwa Rais tulipokuja humu, Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ulikuwa bado sana, lakini tunaona kazi kubwa aliyoifanya. Leo hii mradi ule umeshakamilika, umeme zaidi ya *megawatt* 2,115 zimeongezeka. Sasa kiwango cha umeme *grid* ya Taifa kimeongezeka kutoka *megawatt* 1,690 zaidi sasa ya *megawatt* 3,000 *plus* kwenda *megawatt* 4,000. Nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia? *Zilongwa, zitendwa. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ndugu zangu mnakumbuka kipindi kile alipoingia madarakani, miradi mingi, wale wa umeme wanafahamu. Ndugu zangu watani zangu wale wa Sumbawanga na wengine, kazi aliyofanya mradi mkubwa wa kujenga msongo wa umeme *kilovolt* 400 kutoka pale Iringa uliopita Makambako mpaka Sumbawanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watani zangu wengine wa Tabora wanafahamu, msongo mkubwa wa umeme kutoka Tabora kupita Sikonge mpaka Katavi. Pia mradi kutoka Nyakanazi wa *kilovolt* 400 uliopita Kakonko mpaka kule Kigoma, huyo ndio Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika haya, tuna kila sababu hii aliyoileta hapa Mezani. Ama hotuba aliyoitoa hapa tunasema kwamba ni yenye kutekelezeka, na tumwombee sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti na ndugu zangu, ninaomba niwaambie, katika malengo haya siyo kila mtu atafurahi. Lazima sisi kama Wabunge tusimame imara kutekeleza mipango hii. Lazima tusonge mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais katika hotuba yake amesema mradi wa *LNG* ambao *investment* yake ni zaidi ya Dola za Kimarekani bilioni 42. Mradi ule maana yake ni nini? Mradi ule utakapotekelezeka utaenda kubadili kabisa sura ya uchumi wa nchi yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda eneo hilo, nenda katika ule mradi wa Mchuchuma na Liganga wa kuzalisha chuma. Pia akazungumza suala zima la kuunganishwa kwa reli itakayoenda mpaka Bambabay kutoka kule Mtwara, lakini itaingia tawi lingine mpaka katika mradi wa Mchuchuma na Liganga. Hii maana yake inaenda kutengeneza misingi mizuri ya uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika, ameweka malengo ya kuongeza idadi ya watalii nchini mwetu kufika milioni nane. Tukumbuke, alipokuja hapa Bungeni mwaka 2021 idadi ya watalii ilikuwa wastani wa milioni 1.7. Leo hii tunapozungumza mpaka mwishoni mwa mwaka 2025 wamefika milioni 5.4. Piga makofi kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo hili siyo la kufikirika. Idadi ya watu milioni nane maana yake kwenda kubadilisha

uchumi wa nchi yetu hii. Tumuunge mkono Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba ndugu zangu, hasa upande wa elimu, lazima tujipange miaka mitano ijayo. Tuna sera yetu ya elimu, lazima tutafakari, mwaka 2028 ambao mwaka huu 2026 kutakuwa na vijana wale wanaopaswa kwenda moja kwa moja kuanzia Kidato cha Kwanza mpaka cha Nne, tutakuwa na idadi kubwa ya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, imani yangu kubwa, Serikali tujipange kuona ni jinsi gani tuanze ujenzi wa shule mpya za sekondari kusaidia watoto hawa wote wasikose nafasi. Hii tutakuwa tumetenda haki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vijana watakuwa Darasa la Saba na wengine vijana wa Darasa la Sita, hawa wote watapaswa kwenda sekondari kwa mujibu wa sera mpya ya elimu. Katika hili ninaiomba sana Wizara ya Elimu na TAMISEMI tushirikiane kwa pamoja kuhakikisha tunafanya *resource mobilization* mapema. Utafutaji wa fedha kuhakikisha katika majimbo yetu zikajengwe shule nyingi za sekondari kuwasaidia watoto hawa ambao kipindi hiki watakuwa ni wengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, vilevile ni suala zima la ujenzi wa barabara. Mipango mizuri ipo, niwaombe, pale jimboni kwangu Kisarawe tuna barabara kubwa ya kimkakati inayotoka Kisarawe, inapita Maneromango mpaka kule Mloka, Rufiji, katika *Nyerere National Park*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la kuongeza mapato yetu, eneo lile utalii umeongezeka. Lazima niwaombe hasa kupitia Wizara ya Ujenzi tuipe kipaumbele barabara hii. Tuongeze idadi ya watalii watakaoenda katika hifadhi yetu ya Taifa na mwisho wa siku kuongeza mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ni suala zima la amani. Ndugu zangu ninawaomba, ajenda ya

amani haina mbadala. Sisi wote kama Wabunge na Watanzania kwa ujumla tuweke mbele na tuwaambie Watanzania wafahamu ajenda ya amani haina mbadala. Hili ninawaomba vijana wa Kitanzania, sisi kwa matarajio ya kawaida, tuna matarajio ya kwenda mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, ni lazima tuilinde nchi hii kwa wivu mkubwa, tusikubali hata kidogo nchi hii ikaharibika mikononi mwetu. Ninawaomba sana Watanzania wote twende tukailinde amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango yote hii mizuri ya maendeleo haiwezi ikafanikiwa endapo amani ya nchi hii itaharibika. Tukumbuke nchi nyingine ambazo zimesambaratika katika uchumi wao. Nenda Syria, Yemen na Libya pale mwanzo vijana wasiokuwa na mahari wanaozeshwa wake, lakini leo nenda kaangalie katika nchi hizo, amani imetoweka, uchumi umeharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba Watanzania tuweke wivu mkubwa katika suala zima la kulinda amani yetu, pia tumwombee Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mungu ibariki Afrika, ibariki Tanzania, bariki Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Selemani Jafo. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Khambay, Mheshimiwa Kangi Lugola na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud wajiandae.

**MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, ambaye amekuwa akiturehemu sote kwa kutujaalia afya njema na kuniwezesha mimi kusimama hapa kwa mara ya kwanza ndani ya jengo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Babati Mjini kwa kunichagua kwa kura

nyingi za kishindo na kunifanya leo niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais iliyoko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia nafasi hii pia kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Babati Mjini kwa kumpa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kura nyingi za heshima kwa 97%. Wananchi wa Jimbo la Babati Mjini wamekuwa na sababu za msingi za kumpa kura hizo nyingi za kishindo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya miaka ya minne ya utumishi wake na kwa mambo mengi mazuri aliyoyafanya katika Jimbo la Babati Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Babati Mjini, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan sisi tunaona ni kiongozi hodari na shupavu kwa yote aliyotufanyia wananchi wa Jimbo la Babati Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya elimu, katika hotuba yake Mheshimiwa Rais ameelekeza mambo gani ambayo anatamani kuyaona yanafanyika kwa maendeleo ya sekta ya elimu nchini. Katika mpango mzima wa kuhakikisha tunakuwa na kampasi za vyuo vikuu katika mikoa yote, ni dhahiri hayo yakifanyika katika maeneo yetu elimu itakwenda kuboreka na miji yetu itakwenda kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Jimbo la Babati Mjini tayari tuna kampasi ya Chuo cha Uhasibu Arusha, *IAA Campus* ambapo Serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 13 katika ujenzi wa kampasi hiyo na tunatazamia itakwenda kupokea zaidi ya watoto 10,000. Ikipokea watoto 10,000 ndani ya halmashauri yetu ya mji wa Babati ni dhahiri uchumi unakwenda kufunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta hiyo hiyo ya elimu sisi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tunamchukulia ni kiongozi hodari katika kutambua umuhimu wa elimu. Ametujengea shule mpya nane zikiwemo za msingi na sekondari. Ikiwemo shule ya sayansi ya wasichana ya *Manyara Girls* iliyotumia zaidi ya shilingi bilioni tatu, na leo tunaona vijana wanaendelea kupata elimu katika eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo katika sekta hiyo ameweza kujenga madarasa mengi katika shule zetu, ameweza kujenga matundu ya vyoo katika shule zetu, na wanafunzi wameendelea kupata elimu. Kama hiyo haitoshi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amejidhihirisha kwa kuonyesha kuwa anapenda wanafunzi wa Kitanzania waendelee kupata elimu na wasipate changamoto. Ameendelea kutoa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa mabweni katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizopo ni chache katika sekta ya elimu ikiwemo uhitaji wa shule chache mpya na uhitaji wa mabweni. Katika Kata ya Babati Mjini, shule zilizopo zote hazina mabweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaiomba Serikali kupitia Wizara ya TAMISEMI, kadri itakavyojaaliwa kupata fedha iweze kututengea fedha kwa ajili ya kupata mabweni katika Kata hiyo ya Babati na maeneo mengine ya Halmashauri ya Mji wa Babati yaliyoko na sekondari na yana uhitaji wa mabweni na shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunasubiri kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule, ni vema Serikali ikaona namna ya kutusaidia kupata mabweni kwanza ili wale watoto wanaotoka katika maeneo ya mbali waweze kuondokana na kadhia ya changamoto hiyo hususan watoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta hiyo hiyo ya elimu, Serikali imetenga fedha nyingi katika vyuo vyetu vya *VETA* na vimekuwa ni vyuo ambavyo vimekuwa na msaada mkubwa kwa vijana wetu kwa sababu vinakwenda kuwaandaa kwa ajili ya kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali yangu na Waziri mwenye dhamana husika na sisi Wabunge kama tutaweza kuafiki, bajeti ijayo, vyuo hivi vya *VETA* tuweke utaratibu wa kutambua watoto wanaohitimu katika vyuo vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuone namna ya kuwapatia vifaa vya awali watakavyokwenda kuvitumia pindi wamalizapo masomo yao ili waweze kujiajiri kuliko wamalizapo masomo yao na kwenda mtaani hawana hata zana za kuanzia kazi. Kwa hiyo, tuwabaini ili tuweze kuwapatia vifaa vya awali. Tuwajengee dhana ya kuwaamini ikiwezekana hata ikiwa ni kwa njia ya kuwakopesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta hiyo hiyo ya elimu, upande wa elimu ya juu, tunaipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuweka fedha nyingi katika ku-*support* vijana wetu kwa kuweza kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa rai kwa viongozi wanaohusika kutusaidia kuwa na dawati ambalo litatoa msaada kwa vijana ambao wanajaza fomu kwa ajili ya kuomba mikopo, kwani wengine wana sifa na wametoka kwenye familia ambazo ni duni, lakini wanakosa mikopo kwa sababu pengine ya uelewa mdogo katika ujazaji wa fomu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ninaomba Wizara ione namna ya kuwasidia vijana hao ili waweze kujaza fomu kwa ufasaha na waweze kupata mikopo nao waweze kufurahia fedha nyingi ambazo zimetengwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya maji, sisi watu wa Babati Mjini tunamshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametenga fedha nyingi katika sekta hiyo na tumeanza kuondokana na changamoto ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru zaidi kwa kuendelea kumwamini ndugu yetu Waziri husika katika dhamana hiyo, kwani watu wa Babati Mjini tulikuwa tuna changamoto kubwa ya maji. Alitupatia shilingi bilioni 17.6 kwa ajili ya mradi wa maji wa Dareda – Singu – Sigino – Bagara ambapo umesaidia kupunguza changamoto ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa shilingi bilioni 16, ameelekeza zitolewe kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji wa Mto Erri kuelekea katika mji mpya wa Maisaka Katani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri fedha hizo kwa sababu ameshatoa maekelezo ya mchakato wa kupatikana kwa mzabuni, basi mzabuni apatikanapo fedha hizo ziweze kupatikana ili mradi huo uweze kuendelea na kutatua changamoto ya maji katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kuishukuru Serikali kwa kuendelea kutupa shilingi milioni 900 kwa ajili ya chujio la maji katika Mlima Kwaraa ambapo umeendelea kupunguza changamotoo ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, changamoto kidogo iko katika maeneo ya Mkuyuni B ambapo tunaomba Serikali iweze kutupatia fedha ili kutatua changamoto katika maeneo hayo. Katika bajeti ya 2025/2026, kuna shilingi milioni 400 zilizotengwa kwa ajili ya kupeleka maji katika Kijiji cha Chemchem Kata ya Mutuka. Mheshimiwa Waziri ninakuomba zipatikane fedha hizo ili kuweza kutatua changamoto katika hayo maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ule mradi wa Dareda – Sigino – Bagara tuna uhitaji wa shilingi milioni 400 ili tuweze kukamilisha changamoto kwa ajili ya vitongoji viwili ambavyo vipo jirani na mradi huo. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametusaidia sana sisi watu wa Babati katika sekta hiyo ya maji na tunaendelea kumpongeza na kumwombea afya njema kwa sababu changamoto ya akinamama kubeba ndoo kichwani amewatua ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya umeme tunaendelea kuipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Katika sekta hii ya nishati, sisi watu wa Babati Mjini tulikuwa tuna changamoto kubwa ya umeme, lakini kwa sasa katika vitongoji 54 ni vitongoji vitano tu ndiyo vyenye uhitaji wa

umeme. Katika mitaa 35, mitaa yote ina umeme. Umeme uliohitajika ni umeme jazilishi katika maeneo machache. Vijiji vyote 13 vina umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ambayo yalikuwa na changamoto kubwa baada ya uchaguzi yamepata umeme yakiwa ni maeneo ya taasisi zetu za shule na taasisi za dini. Pia, mtaa mmoja wa Ari katika Kata ya Nangara ulikuwa una changamoto kubwa, lakini baada ya kufanya mazungumzo, na jana watu wa *TANESCO* wamenihakikishia leo nguzo zinafika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, changamoto hiyo ya wananchi ambayo ilikuwa kubwa inakwenda kutatuliwa baada tu ya uchaguzi. Pigeni makofi ya kutosha kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, malizia sentensi yako.

**MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya kilimo wananchi wa Jimbo la Babati ninajua wananiona. Tunaipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumpatia ndugu yetu Mheshimiwa Chongolo nafasi hiyo na msaidizi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tuna changamoto katika masuala ya umwagiliaji katika *round* ya kwanza, tumeweza kupata visima 12 ambavyo vitahudumia hekari zisizopungua 480. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, palikuwa na changamoto ya upatikanaji wa *solar* pamoja na pampu za maji hayo ili kuweza kuvuta maji na kuweza kuyapandisha kwenye *tanks* ili wakulima waweze kuendelea na shughuli za umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nimefanya mazungumzo na Mheshimiwa Waziri na amenihakikishia fedha hizo zipo tayari na ameshatoa maelekezo. Hivyo, wananchi wajiandae kuendelea na shughuli za kilimo cha umwagiliaji kwani baada ya muda watapokea hizo *solar* pamoja na pampu kwa ajili ya shughuli za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la afya tunaishukuru Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwani tumeweza kujengewa majengo mapya nane yaliyotumia zaidi ya shilingi bilioni 12.7 katika hospitali yetu ya Mji wa Babati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tulikuwa tuna changamoto ya Wodi ya Mama na Mtoto, lakini leo tunavyozungumza, hata vifo vya watoto na akinamama wajawazito vimepungua. Hospitali yetu imeendelea kuhudumia zaidi ya akinamama takribani 400, wanaendelea kupata huduma ya kujifungua katika hospitali yetu ile na changamoto zimeendelea kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kumpongeza Waziri mwenye dhamana husika, ndugu yangu Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa na msaidizi wake, Mheshimiwa Dkt. Samizi. Mheshimiwa Dkt. Samizi alifika katika hospitali yetu ya rufaa ya mkoa, tulikuwa na changamoto katika jengo la *ICU*; jengo la dharura na jengo la damu salama, lakini baada ya ujio wake aliweza kutoa maelekezo na fedha ambazo zilikuwa zinahitajika tulizipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunavyoongea jengo la *ICU* linafanya kazi, jengo la dharura linafanya kazi na jengo la damu salama pia. Ninaamini mpaka mwezi Machi litakuwa limekamilika na kuendelea kutoa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ninakushukuru kwa nafasi hii. Ninatumia tena fursa hii kukupongeza wewe, kumpongeza Spika wetu na Naibu Spika pamoja na Waziri Mkuu nikiamini kuwa Mawaziri wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais tutakwenda kushirikiana nao sisi Wabunge na kuhakikisha tunawasaidia wananchi wetu na wanapata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufikia hapo ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Khambay. Nilimtaja Mheshimiwa Kangi Lugola, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mheshimiwa Kafiti William Kafiti na Mheshimiwa Neema William Mgaya wajiandae.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi na ninakupongeza kwa kuukwaa uenyekiti kwa sababu ya umahiri ambao umeuonyesha kwenye Mabunge yaliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kunipa afya njema. Pia, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na Chama chetu cha Mapinduzi kwa kuniteua kuanzia kwenye kugombea Ubunge na hatimaye Wanamwibara wakaniamini wakanipa *comeback* ya kurudi Bungeni, ninawashukuru sana Wanamwibara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya tarehe 14 Novemba mwaka 2025 ambayo Mheshimiwa Rais aliitoa hapa Bungeni kuashiria kulizindua Bunge, ilikuwa ni hotuba ambayo ilijaa maono, ilikuwa ni hotuba ya uthubutu, ilikuwa ni hotuba ambayo inaonesha kwamba Tanzania mpya inakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya kupiga makofi kwa kauli ya Mama Samia kwamba Tanzania mpya inakuja, mimi ninawaomba Waheshimiwa Wabunge hebu wote tuseme, "Tanzania mpya inakuja."

**WABUNGE FULANI:** Tanzania mpya inakuja!

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita kwenye maeneo machache ya kuishauri Serikali ya Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan. Nianze kwenye sekta ya mifugo na uvuvi, lakini nitajikita kwenye uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna kipindi ambacho Mama Samia ameshtuka, kama kuna kipindi ambacho Mama Samia amekuwa na maono kwenye sekta ya uvuvi, ni pale ambapo ameliona Ziwa Victoria ambalo Tanzania tunamiliki maji 49%, Uganda 45%, na kenya wanamiliki asilimia sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mama huyu ameshtuka. Kwa nini ameshtuka? Wenzetu wa Kenya ambao wanamiliki maji asilimia sita wana uvuvi wa kufuga samaki kwa njia ya vizimba na hivi ninavyozungumza sasa, wenzetu wa Kenya kwenye Ziwa Victoria wana vizimba zaidi ya 6,000. Ili hali Tanzania ambao tunamiliki maji 49% tuna vizimba visivyozidi 900, huku ni kushtuka kwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kusema, kama kuna sekta ambayo itasaidia kutengeneza ajira kwa vijana na kwa wananchi kwa ujumla, ni sekta ya uvuvi hasa ufugaji wa samaki wa vizimba. Tunayo maziwa mengi Nyasa, Tanganyika, Rukwa na Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapofanikiwa kufuga samaki kwa vizimba, mambo yafuatayo tutanufaika nayo. Moja, kwenye upande wa ajira, tutakuwa na watu hasa vijana ambao wanalisha samaki, tutakuwa na wananchi ambao wanavuna samaki kwenye vizimba, tutakuwa na wananchi ambao ni walinzi kwenye vizimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya *multiply effect*, tutakuwa na viwanda ambavyo vitakuwa vinatengeneza chakula cha samaki lakini pia, tutakuwa na viwanda ambavyo vitakuwa vinachakata samaki. Kwa hiyo, tutakuwa tumeliletea pato kubwa sana Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sasa tunawenda kuwa na *SGR* katika miaka mitano hii inayokuja kuanzia Tanga Bandarini hadi Musoma kwa hiyo, itachochea uvuvi wa Samaki, kwa sababu sisi uvuvi wa samaki tutakapoenda kufuga kwenye vizimba, ni kuanzia Mkoa wa Kagera, Mkoa wa Geita, Mkoa wa

Mwanza, Mkoa wa Simiyu na Mkoa wa Mara. Kwa hiyo, tutakuwa na eneo kubwa sana ambalo litatuletea mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida nyingine, kumekuwa na uvuvi haramu ndani ya Ziwa Victoria. Kwa hiyo, Serikali itakapokuja na mpango mkubwa sana wa kufuga samaki majini, wavuvi hawa ambao wanavua kiharamu ndani ya maji ya Ziwa Victoria, wengi wataenda kwenye kufuga samaki kwenye vizimba kwa sababu watapata mikopo. Kwa hiyo, tutaweza kuwa na samaki ambao wataanza kuzaliana pamoja na kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwa kuwa samaki wameisha ndani ya Ziwa Victoria, Ziwa litapumua kwa sababu wavuvi wengi wataenda kwenye vizimba na hivyo kuliacha ziwa kwa muda mrefu likipumua na samaki kuendelea kuongezeka. Kwa hiyo, maono haya ya Mama Samia Suluhu Hassan ni maono ya hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda kwenye eneo lingine. Unajua ilivyotangazwa kwamba tarehe 14 Novemba Mheshimiwa Rais atalihutubia Bunge, Watanzania wote kwa makundi mbalimbali, akina mama, wazee, vijana, wafanyabiashara, na mama ntilie; kila kundi lilisubiri kwa kiu tarehe 14 Mama Samia anakwenda kusema nini atakapokuwa analihutubia Bunge?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Hotuba ya Mama Samia kuanzia ukurasa wa 1 - 40 amezungumzia mambo mengi sana kwa sekta na namna ambavyo amejipambanua, mikakati mbalimbali ya miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, makundi haya ambayo yalikuwa yanamsikiliza Mheshimiwa Rais na mimi siku hiyo nilikaa hapa nilipo, Mama Samia akiwa hapo analihutubia Bunge, nilimtazama usoni Mheshimiwa Rais nikaona dhamira yake wakati analihutubia Bunge anaongea na Watanzania. Niliona kabisa anamaanisha na ana dhamira ya dhati kututoa mahali ambapo tumefika sasa kwenda kwenye nchi ya asali na maziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, makundi mbalimbali haya yaliyokuwa yanamsikiliza, wengine kwenye luninga majumbani, wengine vibanda umiza wanamsikiliza Mama Samia kama nilivyotaja, kuna kundi moja ambalo ninataka kuliongelea ambalo nalo lilikuwa linamsikiliza Mama Samia Suluhu Hassan, na hilo kundi linapatikana ukurasa wa 37 kwenye uwajibikaji na utawala wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge tutaongea sana, tutajadili, tutatenga fedha, matrilioni kwa ajili ya miradi ya nia njema ya Mama Samia, lakini hatutafanikiwa, maono haya hatutayafikia kwa sababu Mama Samia alihitimisha kwa kusema yafuatayo, ninaomba ninukuu:

"Tumezungumzia masuala mengi ila msingi wa mafanikio yote haya ni utawala wa sheria, uadilifu, uwajibikaji katika kila ngazi kuanzia juu mpaka chini. Kwa msingi huo, na ili kuhakikisha wananchi wananufaika na rasilimali za nchi pamoja na kupata huduma wanazostahili, tutaelekeza jitihada zetu kwenye mapambano..." (ninarudia) "…kwenye mapambano dhidi ya rushwa, ufisadi, ubadhirifu, uzembe, ukosefu wa nidhamu na maadili. Ni lazima tudhibiti wachache wanaotaka kuturudisha nyuma kwa kuendekeza maslahi binafsi." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niende ukurasa wa 40, Mheshimiwa Rais alimalizia hotuba yake kwa kusema: "Ninamwomba Mungu kuwa mwisho wa utumishi wa Awamu ya Sita usipimwe tu kwa vitu, bali pia kwa tabasamu la utu litakaloachwa kwenye nyuso za Watanzania." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama Samia aliona pamoja na kwamba ana maono ya dhati ya kutupatia Tanzania mpya, lakini dhahiri aliona kwamba kuna matishio, na viashiria vinavyoweza kukwamisha Tanzania mpya kutopatikana na ndiyo maana akajipambanua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, niboreshe eneo hilo, pamoja na kwamba alibaini hivi vihatarishi, matishio haya, niboreshe eneo

moja ambalo na lenyewe tusipoliangalia, ndilo litakaloharibu mipango mizuri ya Serikali na kuendeleza ufisadi pamoja na ubadhirifu ndani ya nchi yetu, ni kundi la machawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, machawa ni kundi hatari, machawa ndimo wanamojificha mafisadi, machawa ndimo wanamojificha wabadhirifu. Bila kushughulika na machawa ambacho ni kichaka wanamojificha, kukichoma moto na kukifyekelea mbali, maono yote haya hayatafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na haya, lazima yafuatayo pia Serikali iyaangalie. La kwanza, ni kuhakikisha kwamba mihimili ya dola: Mahakama, Bunge pamoja na Serikali inakuwa ni mihimili iliyo huru. Bunge liwe huru, kwa mfano, leo tukiletewa Taarifa ya *CAG* lazima tuijadili kwa uhuru, kwa upana ili tushughulike na wabadhirifu. Ndiyo maono ya Mheshimiwa Rais yatakapofikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapoweka maazimio, lazima maazimio yale yaende yaheshimiwe na Serikali na Serikali iyatekeleze, na bila hivyo hatutafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama iwe huru, wapelekewe watu ambao wamefanya uhalifu, watendewe haki ya kuhukumiwa ili waogope fedha za Serikali. Pia, vyombo vya kiuchunguzi, vyombo vya dola na vyenyewe lazima viwe huru, lazima Mwendesha Mashtaka awe huru ili maono haya yafikiwe. Lazima Polisi wawe huru ili wachunguze watu ambao ni mafisadi papa, wapelekwe Mahakamani kuliko kupeleka vidagaa, vimjusi vidogo vidogo ndiyo vinaenda Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya iwe huru, ishughulike na mambo haya. Ninashukuru Mheshimiwa Rais ameliona jambo hili kwamba yote haya ameyasema, amejipambanua, lakini kuna kundi hili hapa linaweza kunikwamisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba, Mheshimiwa Rais alisema Bunge hili atatupa ushirikiano, na sisi tumpe ushirikiano.

Haya mambo ya kuleta masuala ambayo ni muhimu, masuala ambayo watu wamejificha kwenye uchawa, kumbe ni madalali wa rasilimali za Serikali. Wanajificha kwenye uchawa, kumbe ni wahujumu uchumi, halafu tunawabaini. Tuache mambo ya kufunika kombe mwanaharamu apite. Tusikubali mambo kama haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mama amejipambanua, anataka kumaliza Awamu ya Sita aliache tabasamu la utu kwenye macho ya Watanzania. Haya mambo ya kuitanaitana kwenye chama sijui Party Caucus kuna jambo zito, lifisadi limetikisa nchi, lakini kuna watu wengine ambao pengine wako connected na hilo lifisadi na hilo lihujumu uchumi, mnatuletea mambo kwenye Party Caucus, hiyo haitakuwepo hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo haitakuwepo hiyo na imeenda hiyo. Tunataka…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** …tumsaidie Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli kama kundi hili halitadhibitiwa kwa nguvu zote, nami niwaambie, kwetu Musoma tunasema: “vita ni vita Mura.” Lazima tupambane. Itakuwaje wananchi wa Mwibara pale tunahitaji maji na Mheshimiwa Rais maono yake anasema tutakuwa na gridi ya Taifa ya Maji halafu fedha zinaliwa na haya majamaa, Mwibara watapata wapi maji? Mwibara tunataka kupata vizimba vya kufuga Samaki, halafu haya majamaa yaendelee kula pesa. Mwibara tutapata wapi vizimba vya kufuga Samaki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwibara tunataka pembejeo, tunataka kulima, halafu haya majamaa tuyaache kwa kufunika kombe mwanaharamu apite! Hakuna hiyo. Lazima nchi hii watu wapate Tanzania mpya inayokuja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kangi Lugola, nimekuvumilia, muda umeisha.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kangi Lugola, lakini Waheshimiwa tunajua ni kinyume cha kanuni kuwaambia watu wapige makofi, lakini kwa vile alikuwa anaitamani Tanzania mpya na hata na mimi na ninyi mnaitamani, nikavumilia kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, siyo utaratibu wa kanuni, kwa hiyo, kwa leo tuvumilie kwa sababu ni jambo la kutamani kitu kizuri, utaifa ni *very exceptional*. Kwa hiyo, kwa leo tumevumilia, lakini siku nyingine tusiagize watu kupiga makofi.

Waheshimiwa Wabunge, haya, tunaendelea sasa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, baadaye atamalizia Mheshimiwa Kafiti William Kafiti na Mheshimiwa Neema William Mgaya.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa hii nafasi. Kwanza kabisa, ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa ardhi na mbingu, asiyepokea majungu, atakalo yeye huwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru wapigakura wangu walionipa imani yao na ridhaa yao na baadaye Chama changu cha Mapinduzi kikaniteua kuwa Mbunge wa Viti Maalum kuwawakilisha wanawake wa Mkoa wa Mjini kule Unguja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa pongezi kwa Viongozi Wakuu wote wa Serikali akiwemo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu mpendwa Samia Suluhu Hassan kwa umakini na umahiri wao wa kuliongoza Taifa letu hadi kufikia hii leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninauelekeza mchango wangu kwanza kwenye suala la ajira za vijana na wanawake. Kwenye

Hotuba ya Mheshimiwa Rais, ameguswa na ana uchungu na vijana wa Taifa hili kuhakikisha wanapata ajira ili waweze kujikwamua na umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais, ameunda Wizara maalumu ya vijana, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuona changamoto zao, kero zao na matatizo yao ili yafikiwe kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hilo hilo, Mheshimiwa Rais katika hotuba yake amesisitiza kwamba Tanzania itatoa vipaumbele na itatoa msukumo, mazingira wezeshi katika uwekezaji wa viwanda vya ndani. Viwanda vya ndani vitakwenda kupunguza sana tatizo la ajira kwa vijana, lakini pia tutatumia malighafi za Tanzania ili kuweza kuzalisha zaidi na wakulima wetu watapata tija na masoko kupitia viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais, amesisitiza na ana uchungu mkubwa katika kuziwezesha sekta kuu za uzalishaji ikiwemo kilimo, mifugo na uvuvi. Ni historia, hivi karibuni tu wiki chache zitakazobaki, Tanzania inakwenda kuingia kwenye uvuvi wa bahari kuu wakati jambo hilo lilikuwa ni ndoto. Tunakwenda kuzindua bandari yetu ya uvuvi pamoja na ununuzi wa meli za uvuvi katika uvuvi wa bahari kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo Mheshimiwa Rais ameonesha kwa dhati dhamira yake ya kuipeleka mbele Tanzania katika uchumi kwa wazalishaji wa ndani ya nchi lakini kupata fedha za kuinua uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ninajielekeza kwenye sekta ya kilimo na nitagusia kwenye sekta ya umwagiliaji. Mheshimiwa Rais ameona kwamba kilimo cha Mtanzania, kilimo endelevu, kilimo chenye kukabiliana na matatizo ya tabianchi ni kilimo cha umwagiliaji. Kwa maana hiyo basi, amewekeza fedha nyingi kwenye bajeti ya kilimo na tunaona mafanikio yake ikiwemo mbegu bora, viuatilifu na dawa nyingine ya kuulia wadudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijielekeza kwenye sekta hiyo ya umwagiliaji, tumeona kwa vitendo mitambo ya kuchimba visima kwa sekta hii ya umwagiliaji. Jana tu Mheshimiwa Waziri wa Kilimo amekabidhi mitambo 19 ya uchimbaji visima pamoja na magari na pikipiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mitambo ile, mitambo miwili itachimba kisima kina kirefu kinakaribia kilometa mbili kwenda chini. Haya ni mapinduzi makubwa ya kilimo kwenye sekta hii ya umwagiliaji. Mitambo ile iliyokabidhiwa jana Afrika Mashariki nzima hakuna, lakini kwa Tanzania imewezekana, huyo ndiyo Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Waswahili tunasema: "Ada ya mja kunena, uungwana ni vitendo." Tenda watu wataona, majisifu weka kando. Mheshimiwa Rais anatenda na tunaona kwenye sekta zote za uzalishaji, miundombinu, afya, na elimu anatenda na Watanzania tunaona, hatumii maneno, anatumia vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea na mchango wangu, pamoja na kilimo hicho endelevu cha umwagiliaji ninataka niseme machache; sisi wakulima kutokana na jambo hili kubwa alilotufanyia Mama Samia Suluhu Hassan tuna *slogan* yetu tunasema hivi, umwagiliaji na kilimo cha umwagiliaji ndyio mkombozi wa mkulima. Umwagiliaji ni kilimo cha uhakika, inyeshe isinyeshe tutamwagilia na hayo ndio maneno yetu sisi wakulima wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile tabasamu alilosema hapa litawezekana kwa kuwapatia wakulima mbegu bora, viuatilifu, mbolea na umwagiliaji; atawaacha Watanzania wakiwa na tabasamu. Haya yote, ili yafanikiwe ni lazima amani, upendo, utulivu na kuvumiliana tudumishe kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake amewaomba Watendaji wa Serikali wawajibike kwenye maeneo yao. Nakubaliana na wazo hilo la Mheshimiwa Rais kwamba, Watendaji wetu wa Serikali kwa ngazi zote aliowaamini

wamlipe imani aliyowapa. Wafanye kazi kwa vitendo kuwatumikia Watanzania, amewaamini kwa upendo na wao wamlipe upendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye halmashauri, vijiji, tarafa na mitaa, watendaji wote waliopo kwenye ngazi hizo wawajibike kuwasaidia wananchi kutatua changamoto zao kulekule waliko, siyo kusubiri misafara ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, wakamweleze Mheshimiwa Rais au Waziri Mkuu changamoto zao. Wale watendaji walioko chini huu ndio wajibu wao kuyatekeleza hayo na kuwapa tabasamu wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizoko chini zitatuliwe chini, zisingojee Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Wameaminiwa, kila mtu kwa ngazi na wadhifa wake alioupata, Mwenyezi Mungu amemkubalia kuupata, basi aoneshe uwezo wake, kipaji chake na weledi wake katika kuwatumikia Watanzania, kama anavyofanya Mheshimiwa Rais. Rais wetu ni shujaa, shupavu, mkomavu, mstahamilivu na mtekelezaji, sifa moja ya binadamu ni uvumilivu na ustahamilivu; Mama yetu Samia anayo, ni jasiri, mama yetu haogopi kuwatumikia Watanzania, yuko tayari atukanwe, yuko tayari abezwe, lakini Watanzania tunufaike na matunda ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia ninakushukuru sana kwa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud. Nilimtaja Mheshimiwa Kafiti William Kafiti na Mheshimiwa Neema William Mgaya atamalizia.

**MHE. KAFITI W. KAFITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nitumie nafasi hii, kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa miongoni mwa Wabunge katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile natumia nafasi hii kuwapongeza sana Wabunge wote waliomo humu ndani kwa ushindi mkubwa walioupata. Vilevile, ninapongeza ushindi wa Rais wetu mpendwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa ushindi wa kishindo. Vilevile ninatumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kuteuliwa kuwa Waziri

Mkuu wetu kwa sababu, tunaamini Mheshimiwa Rais amechagua jembe hakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninakishukuru sana chama changu, Chama Cha Mapinduzi, kwa kunipa nafasi hii na baadaye wananchi wangu wa Jimbo langu la Ilemela kwa kunichagua kwa kura nyingi. Ninawaahidi nitakuwa sauti yao nje na ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nimeomba kazi kwao na niko tayari kuifanya kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa tarehe 14 Novemba, katika Bunge hili. Uchangiaji wangu utajikita kwa yale Mheshimiwa Rais na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi iliyoyafanya, vilevile nitajikita kuangalia ni nini kilichofanyika kwa kiwango kikubwa katika Jimbo langu la Ilemela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 8(1)(b), inasema lengo la Serikali ni ustawi wa wananchi kwa hiyo, Serikali yoyote ni lazima iangalie ustawi wa wananchi wake. Ustawi huu ninaousema ni katika maeneo mbalimbali, eneo la miundombinu, eneo la afya, eneo la elimu pamoja na huduma za msingi kama vile maji na umeme; huu ndio msingi mkubwa wa ustawi wa wananchi. Kwa hiyo sisi Waheshimiwa Wabunge tuliokusanyika hapa hatuna budi kuhakikisha haya ambayo nimeyataja hapa tunayasimamia kwa kiwango kikubwa, ili kuleta mapinduzi ya kweli kwa nchi yetu na kwa wananchi wetu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ambayo nitakwenda kuyaainisha hapa, ambayo yamefanywa na Serikali ya CCM, yamefanywa na Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ninaanza na eneo la uvuvi, sisi wakazi wa Mwanza, hasa wa Jimbo la Ilemela, shughuli yetu ya kiuchumi inategemea uvuvi. Ilemela zaidi ya kilomita 1,080 sawa na 75% ya eneo letu imezungukwa na maji, maana yake ni shughuli yetu sisi wananchi wa Jimbo la Ilemela ni uvuvi na Mheshimiwa Rais ameleta mapinduzi makubwa katika eneo la uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengine ninaomba niongelee eneo la Ilemela; tunafahamu kwamba, sekta ya uvuvi imeajiri vijana wengi na katika eneo hili la uvuvi Mheshimiwa Rais ameliangalia kwa jicho la pili, kwa maana ya kuwawezesha wavuvi waweze kuwa na nyenzo bora za kuvua, kuongeza kipato chao na pato la Taifa kutokana na sekta hii ya uvuvi. Ninampongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, tarehe 23 Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja Mwanza katika Jimbo la Ilemela kuzindua mradi wa uokoaji wa kikanda. Mradi huu utakuwa msaada mkubwa kwa wavuvi wetu wa Mkoa wa Mwanza, pamoja na nchi za jirani, kwa maana ya Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo wa uokoaji wa kikanda unakwenda kusaidia wavuvi katika ziwa letu la Victoria, wavuvi sasa watakuwa salama, wao na mali zao. Vilevile uvuvi haramu kupitia kituo hiki unakwenda kukomeshwa kwa kiwango kikubwa kwa hiyo, tunashukuru sana. Wavuvi sasa wanapokwenda kuvua, kama hali ya hewa inakuwa sio nzuri, basi kituo hiki kitaweza kuwataarifu wavuvi wetu hali ya usalama katika ziwa na wavuvi hao watakuwa salama; kama hali ya mawimbi inakuwa mbaya, basi wavuvi hawa hawatoenda kuvua kwa hiyo, imekuwa ni msaada mkubwa sana kwa wavuvi wetu wa Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee eneo lingine la vijana. Nampongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametuamini vijana na hata ukiangalia Wabunge waliomo ndani humu wengi ni vijana; tumpigie makofi Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu vijana tumeaminiwa, sisi ndiyo nguvu kazi ya Taifa, nchi yoyote, ili iweze kwenda mbele ni lazima iwekeze kwa vijana. Mheshimiwa Rais kwa kulitambua hilo, pamoja na kuwa na wingi huu wa vijana ameunda Wizara ya Vijana itakayoshughulikia matatizo ya vijana, hii ni zawadi kwetu sisi vijana. Sisi Wabunge tuliomo humu ndani hatuna budi kumuunga mkono Rais wetu mpendwa, ili tuweze kuwakomboa vijana wenzetu. Tunafahamu vijana wanahitaji ajira, Mheshimiwa Rais ametoa zaidi ya shilingi bilioni 200 kwenda kusaidia vijana na akinamama. Ukiangalia katika eneo hilohilo kila halmashauri hapa ina ile 10% ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu sisi Ilemela ndani ya miaka hii minne tumepata zaidi ya shilingi bilioni nne ambayo imekwenda kwa zaidi ya vikundi 250 vya vijana. Tumpe nini Rais wetu mpendwa? Tumpigie makofi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niendelee kuelezea eneo la ukuaji wa diplomasia ya kiuchumi. Mheshimiwa Rais katika eneo hili ameendelea kufanya vizuri, diplomasi yake ya kiuchumi dhidi ya mataifa mbalimbali imeleta matunda nchini kwetu. Ukiangalia taarifa na rekodi za *TISEZA* kwa miaka hii minne, zaidi ya kampuni 915 zenye thamani ya shilingi bilioni 10.9 zimekuja kuwekeza hapa nchini. Tupige makofi kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ina maana gani? Ni kwamba sasa Tanzania imefunguka, tumekuwa na wawekezaji wengi ambao wanakuja kuwekeza nchini kwetu, lakini eneo la miundombinu ya umeme Mheshimiwa Rais ameendelea kuweka bidii. Tulikuwa tunazalisha megawati 1,600 sasa tunazalisha megawati 4,000 na ukiangalia hotuba yake, inasema kufikia 2030 tutaongeza vyanzo vya uzalishaji wa umeme. Tutakwenda kuzalisha wati 4,000 mpaka wati 8,000 kwa hiyo, unaweza ukaona mapinduzi ya miundombinu ya umeme yanaongeza uwekezaji katika nchi yetu kwa sababu, uwekezaji uweze kuwa imara hatuna budi kuwekeza kwenye miundombinu ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona juzi hapa Mheshimiwa Waziri wa Nishati, kaka yangu Deo, amezindua Miradi ya *REA* ambayo tunasema vitongojini kama mjini, ndio kauli mbiu. Sasa Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya makubwa, tuna vitongoji zaidi ya 64,000 leo vitongoji zaidi ya 39,000 vina umeme. Mheshimiwa Rais ametenga zaidi ya shilingi trilioni 1.2 kuongeza vitongoji 9,002 kwenda kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni mambo mengi ambayo Rais ameyafanya kwa sisi watu wa Mkoa wa Mwanza na watu wa Jimbo la Ilemela, kwa jumla mengi yamefanyika. Ameifungua Mwanza kwa kiwango kikubwa kila mmoja hapa ni shahidi, sisi Wanamwanza tunamshukuru. Mradi wa *SGR,* Mwanza

– Isaka, tunatamani uweze kukamilika na sisi Wanamwanza tuweze kunufaika na treni hii kukuza vipato na uwezeshwaji wa biashara katika Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna daraja la Magufuli. Kila mmoja ni shahidi wakati mama huyu anaingia walisema hawezi kulikamilisha, lakini nikuambie ninaomba Bunge hili tumshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, daraja lile limekuwa ukombozi wa uchumi wa Mkoa wa Mwanza, tumpe nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Waziri Mkuu amekuja kuzindua meli yetu mpya ya *MV-New Mwanza*. Meli hii ni moja ya vivutio, ni meli ambayo italeta mapinduzi makubwa ya kiuchumi katika Mkoa wa Mwanza. Serikali ya CCM imefanya mengi, Waheshimiwa Wabunge ninaomba tuipigie makofi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo tunaona eneo la kilimo, Serikali imeendelea kuboresha. Kila mmoja ni shahidi hapa, kilimo ndio uti wa mgongo wa nchi yetu na ukiangalia kimeajiri vijana wengi kwa hiyo, ninaomba niendelee kuipongeza Serikali yetu katika eneo la kuimarisha kilimo, imezidi kuongeza pembejeo na mbegu bora, ili wakulima wetu waweze kunufaika. Kwa hiyo, sisi kama Wabunge, hatuna budi kuhakikisha tunaiunga Serikali mkono, ili suala hili liweze kufanyika kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie katika suala la ajira. Tumeona kwamba, katika kipindi chake cha siku 100 ametoa ajira za elimu zaidi ya 7000 na ajira za afya zaidi ya 5000. Kama Mbunge wa Ilemela, nimepata vijana zaidi ya 100 katika eneo la elimu pamoja na afya, niseme nini kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan?

Mheshimiwa Mwenyekiti, palipo na mazuri ni lazima tusifie na ni namna gani Rais wetu mpendwa ameweza kulijenga Taifa letu kwa hiyo, sisi Wabunge na wananchi kwa ujumla tunaomba tumuunge mkono Rais wetu mpendwa, anayoyafanya ni makubwa. Kwa hiyo, kwa haya anayoyafanya basi tunaamini Taifa letu linakwenda kuponyeka na lile tabasamu alilolisema Mheshimiwa Rais sasa linakwenda kutimia.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. KAFITI W. KAFITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninawaomba Wabunge tuendelee kuiunga mkono Serikali ya CCM. Mungu atatubariki siku zote, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana Mheshimiwa Kafiti. Tunaendelea, Mheshimiwa Neema William Mgaya atamalizia.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Rais wetu mpendwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Awali ya yote, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi tena ya kuweza kurudi ndani ya Bunge hili Tukufu. Sambamba na kumshukuru Rais wangu mpendwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan na Kamati Kuu ya Chama changu Cha Mapinduzi ninawashukuru sana kwa kunipa nafasi kwa mara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajikita katika sekta ya afya na ya utalii; ninaanza na afya. Ninaanza kwanza kwa kumpongeza Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri ambayo ameifanya kipindi chake kilichopita katika suala zima la sekta ya afya. Amefanya kazi kubwa sana katika kuboresha na kuimarisha miundombinu ya afya, kwa maana ya kujenga zahanati nyingi sana ndani ya nchi yetu na vituo vya afya vingi, hospitali za wilaya, hospitali za mikoa, sambamba na kuweza kuimarisha upatikanaji wa vifaa tiba. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake kwa upande wa afya, Mheshimiwa Rais ana maono makubwa ya kuhakikisha kwamba, Watanzania wote wanapata bima ya afya sambamba na ongezeko la ajira za afya katika hospitali zote tuwe na watumishi wa kutosha. Vilevile ana maono ya kukamilisha vile vituo vya afya, zahanati, hospitali za wilaya na za Mkoa, ili kuhakikisha kwamba, ile dhamira yake ya kusogeza huduma kwa wananchi wa Tanzania katika sekta ya afya inakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kuendelea kuwekeza katika kuwajengea uwezo wataalam wetu wa afya kupambana na magonjwa ya milipuko vilevile na kutoa huduma za kibingwa za afya kwenye hospitali zetu. Hayo yote ni mambo ambayo Mheshimiwa Rais amejikita katika hotuba yake kuhakikisha kwamba, tunaenda kufanikisha. Mheshimiwa Rais hawezi kufanikisha haya kama watendaji wake katika Wizara hii ya afya hawatatoa mchango mkubwa wa kusukuma maono haya, ambayo Mheshimiwa Rais amepanga kuyatekeleza katika muda wake huu wa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza na bima ya afya. Bima ya afya kwa Watanzania wote, tumeona ndani ya siku 100 kumeanza programu mbalimbali za kuweza kuanza kutekeleza hili suala zima la bima ya afya kwa wote. Ushauri wangu ni katika Wizara ya afya kuna Kitengo cha Utafiti *(NIMR); NIMR* sasa waone wao wana kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba, wanafanya utafiti katika nchi mbalimbali zilizo-*practice* bima ya afya kwa wote waangalie ni mambo gani wamefanya wakaweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile si vibaya wakaangalia katika nchi ambazo hazikuweza kufanikisha suala zima la bima ya afya, kama wenzetu waliopo jirani, siwezi kuwataja. Aidha, katika kuhakikisha bima hii ya afya inatekelezeka ina maana wao ndio chachu kubwa ya kuweza kuweka mwongozo mzuri katika Wizara ya Afya na kuona kipi cha kufanya na kipi cha kuacha ili tuweze kufanikisha suala hili la bima ya afya kwa wote na Mheshimiwa Rais aweze kukamilisha yale maono yake katika suala zima la bima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwona Mheshimiwa Waziri hivi karibuni anaongea na wawekezaji wa viwanda vya dawa, ni suala jema, ni suala zuri, sambamba na kuwa, sasa tunataka kuwekeza viwanda vingi vya dawa ndani ya nchi yetu. Hii nayo ita-*support* kwa sababu, kuwa na bima ya afya na kutokuwa na uhakika wa kupata dawa itakuwa haina maana. Kwa hiyo, ninaona dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais pamoja na Wizara ya Afya ni kuhakikisha kwamba, inakwenda kufanya mapinduzi makubwa ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hilo la wawekezaji wa viwanda vya dawa ndani ya nchi yetu, sawa tutakwenda kuzalisha dawa nyingi, lakini kuna hatari pia, ya kuweza kwenda kuzalisha dawa ambazo sio bora. *TMDA* wana kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba, viwanda vitakavyozalisha dawa wanasimamia ubora wa dawa zile isije baadaye ikawa dawa zinakuja kuleta madhara kwa wananchi. Kwa hiyo, Wizara ya Afya wana kazi kubwa sana katika kuhakikisha maono ya Mheshimiwa Rais kwamba, wananchi wake wanapata dawa na wanapata bima ya afya kwa wote; wana kazi kubwa ya kuhakikisha wanamsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza hayo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kunapokuwa na uanzishwaji wa viwanda vingi ndani ya nchi kunakuwa na masuala ya *air pollution* na kuna masuala ya *water pollution*. Ndani ya hiyo hiyo Wizara ya Afya kuna Mkemia Mkuu, naye ajiandae, viwanda vitakavyokwenda kuanzishwa vya kutengeneza dawa madhara hayo katika mambo ya *water pollution* na *air pollution,* tunajua matokeo yake yanaweza yakaleta milipuko ya magonjwa mengine. Kwa hiyo, tusije tukawa tunatengeneza huku tunakwenda tunaharibu, nao wakae tayari, kwa ajili ya kuweza kukabiliana na mambo yote hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya ni jambo la msingi sana kwa sababu, kama hatutazalisha Taifa lenye afya ina maana mambo mengine yote yatasimama, kwenye utalii, kila kitu, ina maana uzalishaji utasimama. Kwa hiyo, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa maono na jitihada kubwa ambazo anaziweka katika sekta ya afya. Afya ni msingi kwetu sisi wote Watanzania katika kuhakikisha kwamba, tunaboresha na kukinga nguvukazi ya Watanzania wetu wawe na afya njema, ili kuweza kufanya vizuri uzalishaji kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la utalii. Hakuna asiyejua kwamba, Tanzania uchumi wetu mchango mkubwa unatoka katika sekta ya utalii, kuendesha Tanzania yetu. Nampongeza Mheshimiwa Rais, mwaka 2022 tulianzisha ile programu ya *royal tour* na kwa kweli, inafanya vizuri. Vilevile,

ninaamini kipindi kile, mwaka 2022, nilisema kuna nchi ambazo zime-*practice* hii programu ya *Royal Tour,* kama Ecuador, Mexico, Poland, Israel na wenzetu jirani wa Rwanda, wamefanya vizuri na leo tunaona na sisi tunafanya vizuri katika suala zima la sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba, pamoja na kwamba tunafanya vizuri, ni Mheshimiwa Rais katusaidia. Watalii wanakuja wengi nchini, ninaomba sasa tujikite katika kuhakikisha kwamba, tunatoa huduma inayostahili. Kama unavyojua, sisi Watanzania wengi katika suala zima la huduma hata nchi wenzetu tu, jirani, wanatushinda. Tujitahidi tufanye kazi vizuri katika suala la utoaji huduma katika sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile si vibaya Serikali ikaangalia sasa kupanua wigo wa kuvitangaza vivutio vingine kuelekea Nyanda za Juu Kusini. Nyanda za Juu Kusini, Njombe kuna kitu, Songwe kuna vimondo kule Mbeya, Rukwa kuna *Kalambo Water Falls*. Mheshimiwa Rais mwaka 2023 alipokuja Njombe alituahidi, Nyanda za Juu Kusini kwamba, atakuja na programu mpya, *the hidden place of Tanzania.* Kwamba, hii itajikita katika kutangaza utalii wa Nyanda za Juu Kusini na sisi kwa kweli, watu wa Nyanda za Juu Kusini, tuko tayari kutoa ushirikiano, ili kuwezesha utalii wa Nyanda za Juu Kusini. Tuna mashamba mazuri ya chai na ya miti, ambayo yanaweza yakatumika kwenye utalii wa picha kwa hiyo, tuko tayari na tumejipanga. Tunaiomba Serikali ilete chachu kubwa katika kukuza utalii wa Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Ruaha tu pale unakuta mbuga ambayo ina makundi ya simba yanayotembea kwa pamoja, makundi makubwa ya simba ambayo hakuna kwenye mbuga nyingine yoyote Tanzania. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iweze kuangalia zaidi utalii wa Nyanda za Juu Kusini, tuna mambo mengi sana ya kufanya na kuweza kuongeza kipato kuchangia katika suala zima la utalii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninampongeza Rais kwa hotuba yake nzuri na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Neema Mgaya.

Waheshimiwa Wabunge muda wetu kwa kipindi hiki cha asubuhi umefika mwisho. Nawashukuru wote na kuwapongeza kwa namna ambavyo mnatoa michango yenu katika hotuba hii ya Mheshimiwa Rais, ambayo ni dira ya miaka mitano ya Taifa letu. Kwa hiyo, katika kupongeza pia, tunashauri mambo mengi ambayo yataweza kuwa yenye tija katika kutekeleza hotuba hiyo ya Mheshimiwa Rais.

Baada ya kusema hayo, acha niwataje Wabunge ambao wataanza kuchangia jioni, ili waweze kuwahi. Tunaanza na Mheshimiwa John John Nchimbi, atafuata Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, wengine watafuata baadaye.

Baada ya kusema hayo, ninawatakia mchana mwema. Ninasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni.

*(Saa 7.03 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**29 JANUARI, 2026**

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hotuba ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa Ufunguzi Rasmi wa Bunge la Kumi na Tatu, Tarehe 14 Novemba, 2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu, tunaanza na Mheshimiwa John John Nchimbi, Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mheshimiwa Eric James Shigongo ajiandae.

**MHE. JOHN J. NCHIMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuweza katika hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu, hotuba ya ufunguzi wa Bunge ya kuonesha sasa tumemaliza uchaguzi na tunaanza utawala wa miaka mitano, safari ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwaletee salamu kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Nyasa, wanawapongeza sana. Kwa niaba yao nimezifikisha salamu hizi na wanapenda kuwahakikishia kwamba afya zao ni njema sana na wako wazima kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu ni hotuba ya dira. Nchi zote duniani katika chaguzi zote zinapomalizika nchi ambazo zinatambua umuhimu wa kuanza kipindi cha awamu mpya, huwa ni hotuba muhimu sana katika kuweka *guidelines*, kuweka namna gani tunapita kufikia kule tunakotaka kwenda. Kwa maana hiyo basi, ni hotuba ambayo kwa wenzetu kule Marekani hata katika zile chaguzi ambazo kuna wengine walikuwa wanaangalia vibaya, lakini inapofikia pale wanajua sasa ni hatima ya maisha yetu katika miaka mitano na wanao wajibu wa kujadili, kushauriana na kuangalia wapi inatusaidia ili wote tuweze kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii ni hotuba muhimu sana ambayo Bunge limechukua heshima kubwa sana kuijadili kwa niaba ya Watanzania na kuwawakilisha Watanzania kwa sababu ni hotuba ambayo itawabeba wote wa kila upande, wa kila aina na hata wageni walioko ndani ya Tanzania ni hotuba muhimu sana kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yameongelewa mambo mengi sana kuhusu tulikotoka na tulipofikia hapa na mafanikio makubwa katika Taifa hili, lakini katika hotuba ya Mheshimiwa Rais alizungumzia eneo moja muhimu sana, kwamba mikopo ya 10% iende na kuwafikia walengwa. Hii imekuwa sehemu muhimu sana katika mazungumzo ya Wabunge wengi, kwamba wanatamani ile mikopo ya 10% katika Halmashauri iwafikie watu wengi na iweze kuleta tija katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe rai kupitia hotuba hii kwamba wale ambao wanaisaidia Serikali katika kusimamia mikopo huko chini, Mheshimiwa Rais alitoa sera nzuri, alisimamisha mikopo akatengeneza sera ambayo inawawezesha kuweza kuleta miradi mizuri yenye manufaa kwa wananchi. Sasa, ninatoa rai kule chini ambako wanasimamia mikopo hii, wahakikishe kwamba inafanyiwa kazi ili iweze kuleta miradi ambayo wanasema ni endelevu *(sustainable)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka kule Mbeya waliweza kuanzisha mradi kwa wanafunzi waliomaliza vyuo vikuu wanaotafuta ajira, wakaweza kuanzisha shule yao, wale akinamama waliokuwa wanafagia na mafagio chini wakaweza kukopeshwa magari safi ya kisasa ambayo yamewawezesha wao kumudu maisha yao. Ninakumbuka kule Chunya madaktari waliokuwa wamemaliza hawana kazi waliweza kufunguliwa hospitali ndogo wakawa wanaendesha huduma, kutoa kwa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, hizi sera alizozijenga Mheshimiwa Rais ni sera ambazo zinawawezesha watumishi wa Serikali waweze kutekeleza kazi zao kwa weledi na kwa kutumia elimu yao kulifanya Taifa hili liweze kwenda mbele. Kwa hivyo

basi, ninaomba kutoa rai kwa watumishi wanaotuwakilisha huko chini wawe wabunifu, waangalie miradi endelevu itakayoweza kubadilisha maisha ya Watanzania ili yaakisi maono ya Rais wetu katika Taifa jipya analotaka kulijenga la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amezungumzia maeneo mengi ya maendeleo, katika suala hili la maendeleo lazima tukubaliane kwamba hakuna Taifa linaweza kufanya maendeleo kwa kutegemea 100% nje kwa wafadhili na kadhalika, nchi yoyote duniani, ukienda Japan, China, Marekani na kila nchi ziliendelea kwa wao kujibana mkanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi, wakati Mheshimiwa Rais wetu akizunguka huku na kule kuhangaika kupata fedha za kuwezesha miradi mbalimbali, tunaomba miradi hiyo isimamiwe vizuri kwa weledi huko chini ili kuweza kuakisi yaliyoandikwa kwenye hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona tulivyokwenda huko katika majimbo ingawa jimbo langu siyo, lakini mengi nimeyasikia wanayaongea Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna miradi ilipewa fedha na Mheshimiwa Rais, imepita muda mrefu bado haijakamilika mpaka sasa kwa sababu hela wanazo na bado miradi haiendi, sasa hii hotuba inataka maendeleo katika miradi, kwa hiyo, ninaomba nitoe rai kwa wale watu wote ambao wanasimamia miradi huko chini, waungane na sisi kumuunga mkono Rais wetu katika kuleta maendeleo katika Taifa hili kwa kwenda kusimamia hii miradi kwa uzalendo na kuhakikisha inatekelezwa ili kile ambacho anakitaka Rais wetu kiweze kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipata ahadi katika hotuba ile kwamba atatuletea watumishi na hasa watumishi wa sayansi ili kuifanya nchi yetu iweze kwenda mbele katika eneo la sayansi. Kwanza kabisa mimi binafsi ninashukuru Serikali kwa sababu nimepata walimu wa sayansi 74, ambao wamekwishafika na wamekwisha kuripoti na wamekwisha kuanza kazi, hii inaonesha dhamira ya dhati katika kubadilisha jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba sana wale ambao wamepata ajira hii na walioko kazini kule, wafanye kazi kwa bidii kufundisha watoto wetu ili tupate watoto wenye uwezo, wenye weledi watakaoakisi akili na uwezo wa Watanzania. Kuna tabia mbaya watu wakishaajiriwa wanaingia vipindi vyote na hawatoki shuleni na wakati hawalipwi mshahara, akianza kupata mshahara kila mwezi anaumwa na kila mwezi anaenda kwenye harusi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, hili si jambo zuri. Tunakuwa tunakatisha tamaa na hatuwezi kufikia malengo ambayo anayahitaji Mheshimiwa Rais wetu tuweze kufika. Watumishi walioko huko chini ambao wamepata nafasi ya ajira wakaoneshe kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto nyingine pia ambayo watumishi wanapelekwa katika maeneo ambayo yako mbali, *remote areas* zile wilaya za mbali, wanaamini wakienda kule ni kwa ajili ya kuajiriwa na baada ya hapo wanaomba uhamisho kwenda sehemu za mijini. Tunaomba Wizara zile ambazo zinamsaidia Mheshimiwa Rais aliyeleta hoja hii ya kupeleka walimu katika shule maeneo ya vijijini, wale wafanyakazi wakawatumikie Watanzania. Mahali popote walipo Watanzania wao wana wajibu kama Watanzania kwenda kuwapatia huduma na siyo kuchagua maeneo ya kukaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 21 wa hotuba ya Mheshimiwa Rais aliongelea suala la kuongeza uhifadhi wa mahindi na kuongeza ubora wa *NFRA*. Nimeona hii imekuwa ikifanyika miaka mingi, lakini ninaomba kwa kutumia hotuba hii kama dira yetu, Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Kilimo, sasa ni wakati muafaka wa kuangalia ni namna gani zao la mahindi linaenda kuwa zao la biashara pia pamoja na kwamba ni zao la chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona wenzetu wa mikoa jirani wanatumia zao hili wanakwenda sehemu mbalimbali kuuza nje mpaka huko Somalia. Tukatafute nasi masoko ili tuweze kwenda kutumia mahindi yetu kwenda kuuza huko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika ameongelea suala la mifugo katika ukurasa wa 22 kuimarisha mifugo, tunaomba pia Wizara husika ziangalie namna ya kutafuta masoko ya mifugo mingi zaidi hasa maeneo ya Mashariki ya Kati *(Middle East)*. Watu wengi wanapeleka kule vitu lakini wanapeleka kidogo kidogo sana, nchi za wenzetu zinapeleka sana nyama na kadhalika kule. Hii ni nafasi ya wao kusaidia wafugaji wetu kupata masoko katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la madini Mheshimiwa Rais aliahidi kusaidia wachimbaji wadogo na wananchi. Nimeona kama wiki mbili zilizopita imetoka notisi ya Serikali ikiongeza wigo wa wananchi kwa *local content*, yaani ni vitu gani ambavyo vitafanywa na Watanzania peke yake bila watu wa nje kuhusika. Biashara kwa ajili ya Watanzania peke yake, hili ameshalitekeleza na nimeliona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa rai kwa baadhi ya Watanzania ambao zile nafasi za *local content* wanashirikiana na watu wa nje, wanakuwa wao wamekaa na hisa ndogo wanakuwa vile wamesharudisha kwa watu wa nje wakati siyo dhamira ya Serikali. Wawe waaminifu kwa nchi yao, wahakikishe ile *local content* iliyowekwa kwa ajili ya Watanzania inafanyika kwa ajili ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa umeme, tumepata vijiji vyote umeme kwetu Nyasa, kama ambavyo Mheshimiwa Rais amesema anakwenda kwa upande wa vitongoji, wiki iliyopita pia nimeshapata mikataba imesainiwa ya vitongoji 91 na sasa vitabakia vitongoji 16, ili Nyasa yote iwake taa. Ninaamini, kama kaanza na 91 hivi 161 vitaisha ndani ya miaka miwili, Waziri wa Nishati usimwangushe Mheshimiwa Rais wetu kwenye hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa kumalizia, Mama aliongea hapa kama mama na ninaomba niongee sasa kama mtoto aliyemsikiliza mama kwa wenzangu. Tanzania yetu ndiyo nchi pekee katika Nchi za Maziwa Makuu ambayo ina uhakika wa amani na hakuna nchi nyingine yoyote yenye uhakika wa amani

kama Tanzania. Wenzetu wote wakipigwa wanakimbilia kuomba ukimbizi Tanzania. Tuna makambi ya ukimbizi Tanzania karibu mikoa mingi sana ya mpakani, sisi hatuna pa kwenda zaidi ya kisiwa cha Tanzania. Wale wanaotudanganya tukasahau amani yetu ni muhimu sana, wanakimbia lakini hawakimbilii Afrika, wanakwenda mbali kwa sababu Afrika hakuna sehemu ya kukimbilia zaidi ya Kisiwa cha Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama unataka kuuza *ice cream,* hata kama unataka kuuza mchicha, kama amani haipo hata huo mchicha hauuziki. Tuitumie mitandao ya kijamii kama wenzetu wa China kwa ajili ya biashara na siyo kwa ajili ya kuharibu amani ya Taifa letu. Wapo watu wanaosema mpaka Tanzania isipewe misaada na kuombea hilo jambo, lakini wanasahau kuna misaada mingine inayokuja Tanzania haikwepeki kutokana na teknolojia na hali ilivyokuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani mtu anayetumia dawa za kufubaza maambukizi ya UKIMWI *(ARV)*, zikisitishwa na mataifa ya magharibi, hawa ndugu zetu ina maana watarudi katika ile *HIV* ya zamani ya kubakiwa na kilo mbili. Tusiwe wabinafsi tunapoangalia maendeleo ya Tanzania na amani ya Tanzania. Tusitumie mitandao ya kijamii kuchonganisha wananchi, kuchonganisha viongozi na kutoa taarifa mbaya za watu mbalimbali na viongozi kana kwamba hiyo ni furaha. Tuibadilishe mitandao ya kijamii kuwa kwa faida ya Watanzania wote na kuwa ni sehemu ya biashara itakayoifanya Tanzania iendelee kuwa njema zaidi na Tanzania ya Mama Samia iendelee kung'aa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa John Nchimbi. Waheshimiwa Wabunge ninaomba tuzingatie muda wa dakika 10 kengele ya pili ikilia ili wenzetu waweze kupata nafasi ya kuchangia.

Tunaendelea na Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mheshimiwa Eric James Shigongo na Mheshimiwa Zuena Athman Bushiri wajiandae.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kulihutubia Taifa kutoka hapa Bungeni, kuwaeleza wananchi wa Tanzania ni kwa jinsi gani kipindi sasa kimefika cha kuhakikisha kwamba yale maendeleo ambayo tumekuwa tukiyatafuta kwa uharaka zaidi sasa yanakaribia kuweza kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hii hotuba kwa undani kabisa kuanzia ukurasa wa kwanza hadi wa mwisho, kwa wale ambao walisoma *Cuba* na wamepata *D* mbili, wataona katika hotuba hii falsafa ya Mwalimu Nyerere aliposema kwamba ili tupate maendeleo tunahitaji vitu vine, akataja watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Akaweka sharti kwamba ili hayo maendeleo yapatikane haya mambo manne shurti yawepo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua watu tupo, ardhi ipo, swali linakuja je, tunayo siasa safi? Je, tunao uongozi bora? Katika kipindi hiki cha uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu, miaka minne iliyopita amedhihirisha kwamba hakika sasa yametimia yale mambo manne kikamilifu. Tunayo siasa safi, tunao uongozi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ukisoma hii hotuba utaona kwamba kana kwamba maono ya Mwalimu Nyerere yanaishi ndani ya maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tanzania tumepata kiongozi. Tumepata kiongozi kwa sababu, ukiangalia hotuba hii, ninataka niwaambie, ninarudia, kwa wale amabao wameisoma kindakindaki, utaona kwamba hotuba hii ukichukua na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi na ukachukua maelekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo, ninaweza nikasema *documents* hizi tatu zinatosha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka mitano kama tutafanya kazi yetu kwa uadilifu kabisa na tukamsaidia Rais katika kutimiza yaliyomo katika hotuba hii, ninaweza nikaiona

ikifika miaka minne Mungu akitujaalia Tanzania tunayoitaka tunaweza tukaipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninaomba ili haya mambo ambayo Mheshimiwa Rais na maono yake yamo humu ndani, ninaomba basi tujielekeze kwenye misemo fulani. Kuna wahenga wanasema kupanga ni kuchagua na yuko Mmarekani mmoja nguli wa vipindi vya televisheni anaita Oprah Winfrey, ninafikiri wengi mnamfahamu. Alisema, *"We can not become what we need to be by remaining what we are"*. Hatuwezi kutafuta kile tunachokihitaji, tunachokitaka kwa kubakia vilevile tulivyo. Maana yake akihubiri *we have to change*; lazima tubadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, watu wote ambao kwa namna moja au nyingine wanamsaidia Mheshimiwa Rais katika kupanga mipango ya maendeleo ya nchi hii, kupanga bajeti, kuleta miradi na vitu vingine vyote, uadilifu na kadhalika, lazima tumsaidie Mheshimiwa Rais maono yake haya yaweze kusimama. Peke yake hawezi akafanya bila ya kusaidiwa. Hivyo, twendeni tukamsaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika ninapenda niwakumbushe kwa wale ambao ni wasomisomi kidogo wa vitabu, yuko Mmarekani mmoja anaitwa Frederick Douglass, huyo alikuwa ni mwanaharakati aliyepinga masuala ya utumwa, akasema kama hatupambani, yeye akatumia neno la Kiingereza. "*If there is no struggle there is no progress*"; kama hatupambani kutafuta maendeleo, maendeleo hayatakuja kamwe. Hivyo, ni kipindi cha kuhakikisha kwamba hotuba ya Mheshimiwa Rais na mipango mingine yote ambayo tunaipanga lazima tuiwekee utaratibu wa kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninaomba nishauri na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo, tunaomba kwamba mpango huu utengenezee *program and plan of action*, utuoneshe hata kama ni kwa muda gani kitu gani kinakwenda kutekelezwa, isibakie maneno tu na isibakie hotuba katika kitabu kizuri, maneno mazuri. Tuambieni, yawezekana tukija kipindi kingine tuambieni aliposema kwamba kuhusu kwa mfano kuingia katika uchumi wa

kidijitali tunakwenda kufanya nini na nani anahusika na lini tunakwenda kufanya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi mazuri yametajwa humu ndani, lakini kama tutaamua kukaa kimya na kusema kwamba, kuifanya hii hotuba ionekane ni andiko moja zuri bila kuwa na utaratibu wa utekelezaji, hatutakuwa tumemsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijielekeze kwenye ukurasa wa 34 wa hotuba ya Mheshimiwa Rais, anapozungumza kwamba angependa kuona kuna utekelezaji wa mkakati wa uchumi wa kidijitali. Huduma ya *internet* ipewe msukumo unaostahiki, amezungumza, lakini ukija hapa Tanzania kwetu *internet* inaonekana kama ni bidhaa, inaonekana ni kitu cha biashara moja kwa moja, b*undle* zinavyouzwa ni ghali sana, hata hiyo *internet penetration* tunayoizungumza inakuwa ni ngumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ninashauri na bahati nzuri namwona Waziri Mkuu yupo na Waziri anayehusika na masuala ya mawasiliano; inahitajika sasa kuwepo na utaratibu maalum wa kuweza kuangalia ni kwa jinsi gani *internet* inakuwa ni *enabler*, *internet* inakuwa ni kiwezeshi siyo biashara peke yake. *Internet* sasa hivi mifumo yote ya Serikali ya ulipaji wa kodi; kujiandikisha; sijui kitu gani; kitu gani vinategemea sana *internet*, uwepo wa *internet*. Sasa isiwe ni jambo la mjini peke yake, *internet penetration* lazima iwe katika jambo ambalo linapewa msukumo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu mijini tunafurahi sana kuona kwamba mikopo ya 10% inawafikia watu. Tunachohitaji na tunachokiomba kuwepo na mikutano mingi zaidi ya ku-*sensitize* jambo hili ili watu waweze kupata uwazi wa jinsi gani wanakwenda kukopa hizi fedha; amezitaja Mheshimiwa Rais katika hotuba yake hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni jambo ambalo linahusiana na ujenzi wa madaraja pale Kinondoni. Nikiangalia

ukurasa wa 28, Mheshimiwa Rais anazungumzia ujenzi wa barabara za juu katika Makutano ya Morocco; Mwenge na Magomeni; na kwenda kulibadilisha Jimbo la Kinondoni liwe jimbo la kisasa zaidi. Sasa hivi kunajengwa madaraja pale, Daraja la Kigogo, Daraja la Magomeni pale, Mto Msimbazi unajengwa, kuna daraja lingine la pale Mkwajuni; vyote hivi ndani ya miaka miwili mitatu Kinondoni inakwenda kubadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Wanakinondoni wamenipa salamu nizipeleke kwa Mheshimiwa Rais na ninaamini wasaidizi wake wapo; na kwa kuwa ninahutubia Taifa sasa hivi pengine ataweza kunisikia. Kinondoni tunaridhika kabisa na utendaji wake na tutaendelea kuhakikisha Mheshimiwa Rais, anakuwa salama, anafanya kazi yake ya kuwatumikia wananchi ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo wananchi wa Kinondoni wangependa sana kulisikia katika mpango huu limeelezwa juu ya kupima maeneo ambayo ni *squatters*. Tumechoka na kuwa na *squatters* katika mji ambao ni wa kisasa. Dar es Salaam ni mji wa kisasa; hivyo ninawaomba sana sana wale ambao wanahusika na mambo ya ardhi tuhakikishe kuwa tunaweka katika hiyo *program and plan of action;* kwamba, ni vipi tunakwenda kupima ardhi ambazo sasa hivi ni *squatters*. Kuna miji mingine mingi tu *squatters* zipo. Hata ukienda Ilala *squatters* zipo, ukienda Temeke *squatters* zipo. Tubadilike ili wananchi wetu wanapopimiwa ardhi zao wanavyopata hati wanaweza hata kujiendeleza kwa kwenda kukopa na kuweza kubadilisha maisha yao. Hii pengine nisiisemee tu Kinondoni, hata maeneo mengine ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, tungependa matatizo ya maji; Mheshimiwa Rais anajitahidi sana; haipendezi kwa Jiji kama la Dar es Salaam, 80% ya mapato ya Serikali yanatoka pale, mchango wetu kwa *GDP* Dar es Salaam *17%,* haipendezi jiji kama lile likose maji. Ninachoomba kuwepo na utaratibu maalum wa kuhakikisha Bwawa la Kidunda; na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikwenda pale kwenye Bwawa la Kidunda; tupeleke fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua wamelipa shilingi bilioni 24 ambazo zilikuwa zimekwama, lakini wahakikishe kila mwezi wanapeleka fedha ili bwawa lile liwe ni mwokozi kwa Jiji la Dar es Salaam. Maji sasa hivi si huduma tu, maji ni uchumi, maji ni biashara, maji ni kila kitu, maji ni uhai. Hivyo ninaomba na hili bahati nzuri viongozi wote wanaohusika wapo hapa, ninawaomba sana suala la maji walitilie maanani na walisimamie vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kulihutubia Taifa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abbas Tarimba. Nilimtaja Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela wajiandae.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipatia nafasi ya kusimama tena ndani ya Bunge hili Tukufu. Nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi (CCM) kwa kunipitisha jina langu ili niweze kugombea kwa kipindi cha pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unaniona hapa leo ina maana jina langu lilipita mbele ya macho ya Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi na akaona ya kwamba ninafaa kuendelea kuwaongoza watu wa Buchosa kwa kipindi cha pili. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mambo mema aliyoyafanya kwenye Taifa letu, mambo mema aliyoyafanya kwenye Jimbo langu la Buchosa. Tumepokea watumishi 206, tumeweza kujenga vituo vya afya vingi, zahanati nyingi, shule za sekondari na msingi nyingi. Kwa ujumla wake tumepokea shilingi bilioni 82 ndani ya miaka mitano, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeisoma hotuba hii vizuri sana; na siwezi kuongelea mambo yote ndani yake, nitaongea mambo mawili tu; ukurasa wa 26 na ukurasa wa 14. Ukurasa wa 26,

ninaomba nimnukuu Mheshimiwa Rais kwenye *paragraph* ya mwisho, amesema; "Vilevile tutaanzisha Mfuko wa Wakfu wa *Madini (Mineral Sovereign Wealth Fund)* ili fedha zitokanazo na madini zije ziwasaidie watoto wa vizazi vijavyo. Tunafanya hivyo tukitambua kuwa madini si mahindi kwamba, ukiyavuna utatenga mbegu ili uyaoteshe tena. Tunataka vizazi vyetu visikute mashimo tu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi ya leo nilikuwa ninasikiliza hotuba ya Mwalimu Nyerere ya mwaka 1961. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Wazee wenzake waliopigania uhuru wa nchi yetu walijua ya kwamba chini ya ardhi kuna almasi, chini ya ardhi kuna dhahabu, chini ya ardhi kuna gesi, chini ya ardhi kuna *uranium*, chini ya ardhi kuna makaa ya mawe lakini hawakutaka kuyauza. Mwalimu Nyerere alitamka maneno yafuatayo; ninaomba nimnukuu, alisema hivi: *"Madini hayaozi, nakataza uchimbaji hadi Watanzania"* ninaomba nirudie *"hadi Watanzania watakapokuwa na uwezo.*" Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee wetu hawa wa mwanzo mwaka 1961 walikuwa na uwezo wa kuyauza haya madini tusiyakute, lakini *spirit* yao ikawa tuwatunzie watakaokuja baada ya sisi. Vijana wa wakati huo wakiwa vijana waliokwishapata elimu ya kutosha waje wachimbe madini haya kwa ajili ya Watanzania, hawakuwa na tamaa wazee wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka 65 baadaye tumesimama hapa, wakati Mwalimu Nyerere, anatamka maneno hayo nchi yetu ilikuwa bado ipo nyuma sana, ilikuwa na chuo kikuu kimoja tu; ilikuwa na shule za msingi 3,612 tu; ilikuwa wakati ule ina umeme chini ya *megawatt* 100, lakini hakuwa na haraka, akasema atuachie sisi ili tuje tuchimbe madini hayo. Miaka 65 baadaye nimesimama ndani ya Bunge hili pamoja na ninyi, tumeyakuta madini, tumechimba tumeiendeleza nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyoongea umeme katika nchi yetu tumefikia *megawatt* 4,200. Ninavyozungumza hivi sasa chuo kikuu si kimoja tena, kuna vyuo vikuu 50 katika nchi yetu.

Ninavyozungumza hivi leo umri wa kuishi wa Mtanzania umeongezeka kutoka miaka 37 hadi miaka 67; kazi ya madini haya ambayo wazazi wetu walituachia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ambalo ninajiuliza ndani ya moyo wangu, ambalo ninataka Wabunge tujiulize, tunafanya nini sisi kwa ajili ya watoto na wajukuu zetu? Tunafanya nini mimi na wewe ili wajukuu zetu nao waje waseme kama mimi ninavyomshukuru Mwalimu Nyerere, nao wasimame waseme, ninalishukuru Bunge la Kumi na Tatu, ninamshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan na Wabunge waliokuwepo wakati ule kwa uamuzi wao wa kuhakikisha ya kwamba walinitunzia sehemu ya mapato ili mimi yanisaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi huu wa kuanzisha Mfuko huu ili tunachokipata leo tusikitumie chote, tubakize kidogo kwa ajili ya watoto wetu. Mheshimiwa Rais kwa niaba ya wajukuu zangu ahsante sana; na Waheshimiwa Wabunge ninawaombeni sana kwa moyo mkunjufu na kwa unyeyekevu, ninaomba sana tumuunge mkono Mheshimiwa Rais, kwenye jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, hatuwezi kuwa kila madini, kila *product* iwe na Mfuko wake. Mfuko huu unaoanzishwa unaitwa *Mineral Sovereign Wealth Fund*, kwa ajili ya madini peke yake; lakini mwaka 2014 kwa waliokuwepo Bungeni wakati huo walianzisha kitu kinaitwa *Natural Gas Resource Fund*, ambayo matumizi yake ni sawasawa na kilichotamkwa hapa. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ambaye sasa hivi ndiye Waziri Mkuu wetu, ninaomba sana tusiwe na Mfuko kwa kila *product*. *Natural Gas Revenue Fund* ya mwaka 2014 na sheria yake ipo iliundwa pamoja na hiki nilichozungumza hapa kiwe Mfuko mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko huu mmoja badala ya kuitwa, kwa mfano tukipata petroli leo tutahitaji kuwa na mfuko wake, tukipata *product*, tukivumbua kitu kingine kesho labda *uranium* iwe na mfuko wake. Hatuwezi kuwa na mifuko mingi, badala yake tuwe na mfuko mmoja tu na mfuko huu uitwe

*Natural Wealth Sovereign Fund*. Fedha zikusanywe pale ziwasaidie watoto wetu watakaokuja baada ya sisi. Hilo ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili lipo ukurasa wa 14. Kwenye ukurasa wa 14 hotuba ya Mheshimiwa Rais, imetamka maneno ya fuatayo; "Mwelekeo wetu ni kukua kwa pamoja kwa uchumi unaogusa maisha ya watu mmoja mmoja *(microeconomy)* na uchumi wa jumla *(macroeconomy)*." Tunataka kukuza uchumi. Tunataka kuukuza uchumi wetu *macro* na uchumi wetu *micro*. Unaposoma ripoti zetu za uchumi unakuta taarifa nzuri sana kwamba *GDP* yetu imeongezeka ni bilioni 92; *per capital income* imeongezeka ni 1,300, lakini wananchi wetu hawana fedha mfukoni. Kwenye *record* uchumi umekuwa lakini wananchi wanalalamika hawana fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini cha kufanya? Ninakubaliana na kila kitu, tufanye jambo moja muhimu sana katika Taifa letu; tu-*trickledown effect* uchumi utoke *macro* uje *micro,* uingie kwenye mifuko ya watu, watu waone fedha kwenye meza zao wapate chakula. Lengo la Mheshimiwa Rais ni kuwapa watu furaha. Nimesoma ripoti ya furaha duniani nchi yetu ni ya 129. Kuna nchi 12 tu chini. Tuna kazi kubwa sana ya kuwapa furaha watu wetu. Watu wetu wanahitaji fedha, wanahitaji maisha yao yawe rahisi ili waweze kuwa na furaha. Tufanye nini sasa? Tufanye nini? Hatuwezi kugawa fedha kwa watu wetu; tutengeneze *opportunity* za watu kutengeneza fedha wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalishukuru Bunge lako Tukufu tulikaa hapa mwaka jana tukapitisha sheria ya manunuzi, tukabadilisha Sheria ya Manunuzi, kwamba biashara yoyote ya shilingi bilioni 50 kushuka chini haifanywi na mgeni katika nchi hii. Tumefanya jambo hilo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati huo Mwigulu Nchemba, Waziri Mkuu wetu akaandika kanuni. Leo hii Tanzania hakuna mtu mgeni anafanya biashara ya bilioni 50. Ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, tupandishe *threshold* kutoka shilingi bilioni 50 kwenda shilingi bilioni 100. Biashara ya shilingi bilioni 100 isifanywe na mgeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wamechoka kuendelea kushuhudia wageni wanakuja hapa wanatajirika wao wanabaki maskini. Leo hii tuna viwanda vingi kila mahali, lakini tunafahamu ya kwamba watu hawa ni wawekezaji. Sichukii wawekezaji, sichukii wawekezaji; na ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, ameongeza mitaji ya uwekezaji katika nchi yetu kutoka dola bilioni moja hadi bilioni sita leo tunavyoongea, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Lakini wakati ninapenda wawekezaji ninawapenda watu wangu; ninataka watu wangu watajirike kwenye nchi yao. *This is our country*. Tunatakiwa sisi wenyewe tuwe na uchumi mkononi, *take the mean of the economy*. Hii ni nchi yetu sichukii wageni *I am not xenophobic,* lakini ninatamani watu wetu washikilie uchumi wa nchi. Watanzania wawe mabilionea katika nchi yao, wana nchi tajiri inakila kitu wanaweza kutajirika. Tuwasaidie tuwatengenezee fursa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Rais, ameanzisha *Samia Bond* ili kuwasaidia wakandarasi. Ninamshukuru Mheshimiwa Rais amelipa bilioni 200 ili kuwasaidia vijana wetu ili waweze kupata mikopo. Ninamshukuru Mheshimiwa Rais na Bunge lake kwa Sheria ya *Local Content* kuwasaidia Watanzania waweze kushiriki kwenye uchumi wao. Tusipowasaidia Watanzania, tukawatengenezea mazingira ya kutajirika wataendelea kuwa maskini na kuwa na chuki. Tuwasaidie ili waweze kukamata uchumi wa nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *digital Economy*, tuwasaidie kwenye *digital economy*. Leo hii vijana wetu wana *products,* wamebuni, lakini hawana mtaji, hawawezi kwenda benki wakakopeshwa. Huo ubunifu wao uwe sehemu ya mtaji waweze kupatiwa mikopo na benki. Marekani walivyoanzisha *Silicon Valey* walikuwa na *Silicon Valey Bank* kwa ajili ya kuwasaidia wabunifu wao. Tusipofanya hivyo vijana wetu watabuni *products* watakimbia nchi yao. Benjamin Fernandes alianzisha *NALA* hakupata msaada akakimbilia nchi nyingine; si jambo jema. Tuwasaidie vijana wetu ili watajilike na nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Eric James Shigongo. Nilimtaja Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri; Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela na Mheshimiwa Samira Khalifani Amour wajiandae.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais siku akifungua Bunge la Kumi na Tatu tarehe 14 Novemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kauli moja. Kuna neno moja la Kiswahili linasema "Chanda chema huvishwa pete". Watanzania wote tunaona kazi aliyoifanya Mheshimiwa Rais, kwa kipindi cha miaka minne. Rais huyu amekuwa Rais wa mfano. Ninasema chanda chema huvishwa pete kwa sababu tunahitaji Watanzania wote tumvishe pete Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. Wabunge tumejaa hapa wa Chama Cha Mapinduzi kutokana na kazi kubwa aliyoifanya katika majimbo yetu. Miradi kuanzia ngazi ya matawi mpaka mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, amezunguka nchi hii, amezunguka nchi hii akiomba kura zake na za Wabunge pamoja na Waheshimiwa Madiwani. Kwa kuwa Watanzania wameiona kazi iliyofanyika ya Chama Cha Mapinduzi hawakusita kutoa kura za ndiyo kwa Chama Cha Mapinduzi. Akinamama wamewaona wengi kipindi hiki wakirukaruka, wakichakalika, wakizunguruka kuziomba kura za Mheshimiwa Rais. Kwanza wamejisikia fahari za kupata Rais kwa mara ya kwanza mwanamke; lakini pia wamejisikia fahari kwa mwanamke huyu kujali sana shida za wanawake, mojawapo ikiwepo maji. Alileta kauli yake ya kumtua mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kuwa maji yalikuwa ni tatizo kubwa sana katika Taifa letu. Rais huyu alipoingia aliwaona wanawake jinsi wanavyoteseka kuyatafuta maji, kwa sababu sisi ndiyo walengwa wakubwa wa maji. Maji yanapokosekana nyumbani anayeulizwa ni mama wala si baba; watoto wanaposhindwa kupika wanamuuliza mama, hakuna maji, watoto wanaposhindwa kufua wanamuuliza mama, hakuna maji; watoto wanaposhindwa kuoga wanamuuliza mama, hakuna

maji. Kwa kuwa Mheshimiwa Rais huyu ni mwanamke haya yote yalimgusa na ndiyo sababu wanawake wote walitoka kumtafutia kura. Kura hizi zilikuwa ni kura za kihistoria kutokana na hali halisi aliyoichukulia Mheshimiwa Rais, hasa katika matatizo yanayomuhusu mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuishia hapo, Rais huyu alikuja kwenye suala la nishati salama. Nishati hii ya kupikia, nishati ya kupikia kwa kweli huko tulipokuwa nyuma afya zetu, mama zetu, bibi zetu hata sisi wengine tulipata matatizo ya macho kwa sababu ya moshi wa kuni. Si hilo tu, unapokuwa unatoka katika shughuli zako za kila siku ukaja nyumbani ukakuta nyumbani hakuna kuni, ukakuta nyumbani mvua imenyesha kama vile leo asubuhi ilivyonyesha Dodoma, kuni zimeloa, mama huna amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mama huyu akaangalia ni nini cha kuwasaidia akina mama, akaona ahakikishie kwamba anaisimamia nishati safi ya kupikia ili kuwasaidia akinamama. Akinamama sisi tunasema, sisi akinamama ni washawishi wakubwa sana. Kwa sababu sisi akinamama tuna mapenzi makubwa na wanaume zetu, tuna mapenzi makubwa na watoto wetu. Tunaposimama tukiongea kuhusu masuala yanayotugusa tukaziomba kura kwa waume zetu na watoto wetu lazima watupe kura. Kwa maana hiyo basi ndiyo maana watu wengi wameshangaa kwa kura za kishindo alizozipata Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi, akinamama, akinababa, watoto wetu mwangalieni Mheshimiwa Rais huyu anavyolipambania Taifa hili; siyo lake peke yake. Tanzania ni ya kwetu wote. Tunaona fahari tunapopita mitaani kuona barabara nzuri, tunaona fahari tunapopita mitaani tukiona umeme, tunaona fahari tunapopita barabarani tukiona maji, tunaona fahari tunapopita barabarani tukiona maendeleo na uchumi wa mwananchi mmoja mmoja, Watanzania tumvisheni Mheshimiwa Rais pete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamvisha pete tumpe moyo wa kuendelea kupambana tena kwa maendeleo ya Taifa hili katika miaka hii mitano. Tunatambua iko miradi iliyotekelezwa na iko miradi mingine ambayo bado inatekelezwa, tuna uhakika itakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nirudi sasa katika hotuba ya Mheshimiwa Rais. Katika ukurasa wa 17 umeongelea kuhusu maji. Maji ni uhai, bila maji hakuna maisha, bila maji hakuna maendeleo, bila maji hakuna Wizara yoyote inaweza kufanya kazi. Tumeona maendeleo makubwa katika sekta ya maji. Mwaka 2021 mijini maji yalikuwa 84% sasa hivi tuna 91.6%; vijijini yalikuwa 70.1% sasa hivi tuna 85%. Ahsante Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais hakuishia hapo, kwa kauli yake ya kumtua mwanamke ndoo kichwani aliendelea zaidi akaleta magari ya kuchimba visima katika mikoa yote ya Tanzania. Mheshimiwa Rais mpaka sasa hivi visima 900 vimechimbwa katika nchi yetu na bado kazi inaendelea, Mheshimiwa Rais hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije Kilimanjaro katika Mkoa wangu. Kilimanjaro sisi tumefaidika, tulikuwa tuna Mradi wa Maji wa Same - Mwanga – Korogwe. Mradi ule ulitusumbua sana miaka nenda rudi, tukasema jamani huu ni mfupa wa nini? Mfupa wa nguruwe au mfupa uliomshinda fisi? Hata hivyo, Mheshimiwa Rais ule mfupa uliomshinda fisi aliumaliza. Mheshimiwa Rais alipambana kiasi cha kutosha na hivi tunavyoongelea Mradi wa Same – Mwanga - Korogwe unafanya kazi tunafurahia matunda ya Mama Samia. Ahsante sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongea changamoto katika sekta ya maji. Tunatambua Serikali imefanya kazi kubwa sana katika sekta ya maji, lakini kumekuwa na changamoto ya upotevu wa maji. Changamoto hii ya upotevu wa maji inatokana na yale mabomba ya zamani. Sasa hivi mabomba haya ni ya *plastic* ni mapya zamani yalikuwepo mabomba ya chuma ambayo yameoza yametoboka, kwa maana hiyo basi maji

yanatiririka bila kuwafikia walengwa. Katika hili niiombe Serikali yangu sikivu ifuatilie suala hili kuhakikisha kwamba yale mabomba ambayo ni chakavu yanafanyiwa ukarabati ili walengwa waweze kupata maji wanayoyahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongea suala la elimu, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais na nitaongelea kuhusu vyuo vya *VETA* kila wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwa vijana wetu wengi ambao hawajapata nafasi ya kuendelea na masomo ya juu wanakuwa mitaani mara kwa mara. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwa kuliona hili na kuanzisha vyuo vya *VETA* kila wilaya. Vijana hawa sasa hivi wasipopata nafasi za kuendelea na masomo ya juu wanajiunga na *VETA* na kufanya mafunzo ambayo yanawasaidia na baadaye kujiajiri na hata kuajiri wenzao. Ahsante sana Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna elimu ya amali. Hii elimu ya amali ni elimu ambayo itawasadia sana watoto pia inaendana na elimu ya *VETA*. Katika Mkoa wa Kilimanjaro tunazo shule za amali 12. Shule hizi kwa kuwa mtoto anaanza tangu *form one* akijifunza ufundi mpaka akifika *form four* tayari ana cheti cha kumaliza ufundi na anaweza kujiajiri na hata kuajiri wenzake. Ahsante Mama Samia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Zuena.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mheshimiwa Samira Khalifani Amour, ajiandae.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikushukuru wewe kwa nafasi. Ninaomba niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Lulindi kwa kuniamini na kunirejesha tena. Kipekee kabisa ninaomba pia niwashukuru familia yangu maana yake mke wangu na vijana wangu wawili

kwani walikuwa na wakati mgumu sana kipindi cha uchaguzi kutokana na hali halisi iliyokuwepo hapo. Kwa uvumilivu wao kwa kweli ulinifanya nikaimarika na nikarudi hapa kwa kasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sauti yangu unaisikia imebadilika ni kwa sababu siko vizuri kiafya na nina mafua, lakini nimelazimika nije nichangie kwa sababu ya umuhimu au unyeti wa hotuba hii ambayo tumewekewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa nguvu na kuniamsha nikiwa hai japo ninaumwa, lakini nimshukuru pia Mheshimiwa Rais wa nchi hii mbeba maono wa nchi hii kwa kazi kubwa aliyoifanya lakini na maono yake aliyotuwekea hapa, ambayo bila shaka ninatarajia sisi kama wadau wake tuweze kuweka *input* ya kule anakotaka kuelekea kusudi tuweze kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema *essence* ya ku-*table* hotuba ya Rais hapa kwetu ni kuweza kumuwezesha kumpa maoni yetu ambayo yanaweza yakachangia chochote, lakini kuonesha jinsi gani tunaweza tukafanya hiki na kile, tuweke kile tuongoze hiki, tupunguze hiki kusudi haya yawe maono sahihi ya kutembelea kipindi hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoanza kwa kumshukuru amefanya kazi kubwa na kwa ujumla Awamu ya Sita pamoja na Baraza la Mawaziri kwa ujumla wamefanya kazi kubwa ambayo mpaka sasa hivi takribani Wabunge wote tunalo la kusema kuhusiana na pale tulipotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia amekuwa mwepesi sana wa kuelewa changamoto za wananchi na kuchukua hatua stahiki yeye mwenyewe binafsi na hii imeonekana maeneo mengi sana. Kwa mfano, tulivyotaka kwenda kusogea katika eneo la uwekezaji katika utalii alijitoa yeye mwenyewe na kuonesha njia jinsi gani tunataka tuenende kufikia maendeleo. Tulikuwa tukipata watalii takribani 500,000

huko nyuma, lakini kwa kujitoa kwake tumeweza kufikia idadi ya watalii takribani 2,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuonesha pia au kuthibitisha haya ninayoyasema kwamba yeye ni mwepesi wa kutambua changamoto na kuzitafutia jinsi ya kuzitatua, ni vile alivyoweza kukubali mzigo ambao watangulizi wake waliuanzisha kwa maana ya miradi ya kimkakati. Miradi hii mikubwa ilihitaji pesa nyingi sana na katika mazingira ambayo tumezoea ni kama utamaduni huko nyuma watangulizi wengi wamejielekeza katika malengo yao katika kipindi hicho muafaka. Kwa hiyo, tungetarajia hata yeye angekuwa na mambo mapya ya kutaka kuyaanzisha kusudi watu wayaone kwamba haya ndiyo mambo yake aliyoyaanzisha, hakufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amehakikisha kuona kila kitu kilichoanzishwa ambacho kilikuwa ni chenye kazi ya kututoa pale tulipo kuendelea mbele au ni mradi mkubwa ambao ni wenye maendeleo wenye tija alihakikisha kwamba lazima anaukamilisha kwa nguvu zote na haya ndiyo maendeleo endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwenye Mkoa wa Mtwara au kwa maana mikoa yetu ya kusini, tumeona ujenzi wa bandari kwa kiasi kikubwa cha pesa takribani shilingi bilioni 157.8. Ujenzi huu umekamilika na bandari ile imekuwa yenye tija. Sasa hivi kunaingizwa kontena nyingi sana pale kwa ajili ya kusafirisha kutoka nje, lakini imechochea uchumi katika eneo lote la Mtwara hali kadhalika Tanzania kwa ujumla imeongeza pato lake la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ujenzi wa kiwanja cha ndege takribani shilingi bilioni 73 za kitanzania na ujenzi ule unakaribia kukamilika. Ni kiwanja cha ndege bora kabisa chenye *standard* za kimataifa na kitakapokuja kutumika *fully fledge* bila shaka kitakuwa kimeongeza tija kubwa sana katika eneo lote la kusini na nchi hii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, tumeona ujenzi wa hospitali ya rufaa ya kanda takribani shilingi bilioni 15.8 na ujenzi

ule umekamilika. Ule ni ujenzi ulikuwa wenye tija kubwa, tumeona watu wengi sana kutoka hata nchi za nje wamekuja kutibiwa katika maeneo hayo. Vilevile, wananchi wa Kusini sasa hivi hawalazimiki kuja Muhimbili kutafuta huduma za kiafya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, kumekuwa na ujenzi wa Barabara ya kutoka Mnivata kuelekea Masasi kilometa 160 pesa takribani shilingi bilioni 236. Ujenzi huu unaendelea vizuri sana hususani katika *lot* ya kutoka Msanga kuelekea Masasi. Ningetaka ushauri katika eneo la kutoka Mnivata kwenda Newala kasi iongezeke. Wananchi wa maeneo yale wana tamaa lakini wana imani kubwa na ujenzi ule kuwa utakuwa umewatoa katika changamoto walizokuwa nazo huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, kumekuwa na ujenzi wa Barabara kutoka Mtwara kuelekea Masasi kupitia Mingoyo kilometa 200 na kitu takribani shilingi bilioni 401. Hali kadhalika ni ujenzi ambao utakuwa umeleta tija na kuchachusha maendeleo katika eneo hilo kuelekea hii mikoa ya kusini ya Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, kumekuwa na ujenzi wa bandari mpya (Bandari ya Mgao). Bandari hii ni bandari ya mizigo na mambo mengine (ni bandari ya uchukuzi hii), takribani shilingi bilioni 400+ bado inaendelea kuleta maendeleo katika maeneo hayo lakini ni kuonesha jinsi gani Mheshimiwa Rais amejitahidi sana kuhakikisha anafufua uchumi wa Kusini na nchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya mazuri yote ambayo nimeyasema hapa bado sisi tunalo la kuzungumza kwa lengo la kutaka kusogea mbele. Kuna maeneo ambayo bado hayajafanyiwa mchakato wa kimaendeleo wa kutosha. Kwa mfano, kwa upande wa Kusini katika eneo la utalii kuna maeneo mengi sana ya utalii yapo vijijini bado hayajaweza kutumika. Kwenye mbuga ya Lukwika kwa mfano, ni miongoni mwa mbuga ambayo na yenyewe ni bora kabisa katika mbuga za wanyama zilizoko katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika tukizungumzia katika masuala ya maendeleo katika kilimo, eneo la kusini kwa ujumla wake ni eneo muhimu sana katika uzalishaji wa chakula hususan katika mahindi, lakini eneo hili ni eneo pia ambalo ni la uzalishaji wa mazao ya biashara hususan korosho. Korosho imekuwa ni zao moja muhimu kabisa la biashara katika nchi hii linaloingizia pesa nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, muhula uliopita takribani dola milioni 580 za kigeni sawasawa na takribani ya shilingi trilioni 1.4 hivi, zilitokana na uzalishaji wa korosho. Pesa hizi ni nyingi sana ambazo zimechachua uchumi katika eneo la Mkoa wa Mtwara na maeneo mengine ya Kusini, hali kadhalika nchi kwa ujumla kwa sababu tukizungumza katika pato la kigeni ilichangiwa pesa nyingi kama nilivyosema hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kutokana na jitihada hizo hizo ambazo tungetamani Mheshimiwa Rais azifanye angezifanya katika maeneo mengine pia ya kufufua kile kilichoitwa wakati ule *Mtwara Corridor.* Hii ilikuwa ni *development plan* ambayo ilikuwa ni muhimu sana katika kuongeza uchumi wa nchi hii hususan katika kuchachua eneo zima la kanda ya Kusini kwa maana ya Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Njombe na kadhalika...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Issa Mchungahela.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Samira Khalifani Amour, Mheshimiwa Adonis Alfred Bitegeko na Mheshimiwa Khalid Mussa Nsekela, wajiandae.

**MHE. SAMIRA K. AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuweza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Ninaomba nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunijalia kuweza

kusimama hapa katika Bunge lako Tukufu (Bunge la Kumi na Tatu). Ninapenda kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Kagera kwa imani waliyonipa. Ninaomba niwaahidi mbele yako kwamba nitawatumikia kwa moyo wangu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Rais wetu, jemedari Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ushindi wa kishindo, ushindi wa kihistoria ushindi wa 97%. Hii ni imani tosha kwa Watanzania kwamba wanaridhika na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Niendelee kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi uliotukuka na kwa mapenzi anayoyaonesha kwa Watanzania; anatenda kwa vitendo. Ninajivunia kuwa na kiongozi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Serikali yake kwa kuendelea kutoa mikopo ya 10% kwa wanawake, vijana na walemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sote ni mashahidi tunaona Tanzania nzima mikopo inaendelea kutolewa hususan katika Mkoa wangu wa Kagera. Wanawake wa Mkoa wa Kagera wanashukuru sana. Sasa hivi wanawake wa Kagera tunajituma, mikopo hii imekuwa ni tija imeleta furaha katika familia zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Serikali yake katika kuboresha usafiri wa anga katika Tanzania yetu. Sisi sote ni mashahidi tunaona usafiri wa anga kwa sasa tunasafiri bila wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wangu wa Kagera, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameona kilio cha wananchi wa Kagera na akaamuua kutufuta machozi, hivi sasa tunategemea kupata ujenzi wa uwanja wa Omukajunguti katika Wilaya ya Misenyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja huu upo tayari kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ninachoomba Serikali yangu ianze utekelezaji wa uwanja huu kwani ni tegemezi katika Mkoa wetu wa Kagera. Tunategemea kukuza uchumi wa mkoa wetu kwa kupitia uwanja huu pindi utakapokamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kagera ni wakulima lakini tunazo bidhaa tunazoweza kusafirisha kupeleka nje ya nchi, endapo uwanja huu utakamilika tutafanya biashara nje ya nchi, tutapeleka ndizi, samaki, dagaa. Lakini itoshe kusema, Mkoa wa Kagera tuna hifadhi ya Burigi - Chato, lakini pia kuna hifadhi ya Ibanda, uwanja huu utakapokamilika tunategemea tutapata wageni wengi katika Mkoa wetu wa Kagera na tutaweza kufanya biashara na wanawake wa Mkoa wa Kagera wataweza kufanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake katika miundombinu ya maji, amemtua mwanamama ndoo kichwani. Maji vijijini kwa sasa kwa uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa Tanzania yetu yanapatikana kwa 85%. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anajituma, amedhamiria kweli kweli na tayari amemtua mwanamama ndoo kichwani. Lakini katika Mkoa wangu wa Kagera upatikanaji wa maji vijijini kwa sasa yanapatikana kwa 73%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wangu wa Kagera kuna miradi mikubwa 28 ya maji vijijini inaendelea ambayo imegharimu takribani bilioni 52 nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan? Itoshe kusema ninampongeza sana Waziri mwenye wizara hii Mheshimiwa Aweso, kaka yangu anajituma sana na niombe aendelee kujituma hivi hivi kumsaidia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi anavyoendelea kuwatumikia Watanzania, lakini nimshukuru sana kwa kuweza kumteua Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ili kuweza kumsaidia, hakika sote tunaona, anaweza na anafaa. Hata hivyo,

itoshe kusema, nimshukuru sana kwa kuweza kuteua Mawaziri wengine na Manaibu Waziri, wote tunaona sasa hivi ni 2026, wote wana kasi ya 5G. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itoshe kusema, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Samira Khalfan Amour, nilimtaja Mheshimiwa Adonis Alfred Bitegeko, Mheshimiwa Khalid Mussa Nsekela na Mheshimiwa Dkt. Charles Sungura ajiandae.

**MHE. ADONIS A. BITEGEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuweza kunifikisha hapa leo na nikisimama kwa mara ya kwanza Bungeni kama Mbunge nikiwakilisha wananchi wa Jimbo la Muleba Kaskazini Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Muleba Kaskazini ambao wameweza kunipa kura nyingi za kishindo na leo nimeweza kuaminiwa na chama changu chini ya Jemedari wetu Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Mbunge wa Jimbo la Muleba Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze viongozi wote wa Bunge waliochaguliwa, Spika na Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, lakini pia nimpongeze Waziri Mkuu kwa kuteuliwa na kuaminiwa na Rais kuwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita hasa katika maeneo mawili. Kwa vile ni mjumbe wa Kamati ya Afya na Mmasuala ya UKIMWI nitagusia eneo la sekta ya afya, lakini pia nitazungumzia kuhusiana na miaka mitano iliyopita ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alivyoweza kutuletea mafanikio katika Jimbo la Muleba Kaskazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaelezea pia matarajio yetu makubwa kutokana na hotuba ya Rais aliyotoa wakati anazindua Bunge hili la Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutambua ndani ya sekta ya afya kumekuwa na uwekezaji mkubwa umefanyika wa rasilimali watu ambao umesababisha ongezeko la watumishi. Tunatambua kwamba ndani ya siku 100 Mheshimiwa Rais alitoa kipaumbele kikubwa kwa sekta ya afya na tukapata wataalam 5,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza pia kwenye upande wa Wilaya ya Muleba tumepokea watumishi 34 katika sekta ya afya, tunashukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hao tu ni moja ya watumishi 157 ambao tumepokea katika Wilaya ya Muleba, pongezi sana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi alivyowekeza katika watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hilo, ni matarajio baada tu ya kupokea watumishi hawa na kuwagawanya katika vituo vya kutolea huduma za afya ni matarajio kwamba bado tutaendelea na watumishi wengine siku za usoni hasa katika maeneo ya watumishi wa maabara, wataalam wa mionzi na dawa za usingizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa huduma bobezi na za kibigwa, tumeona ongezeko la wataalam katika huduma za kibigwa na bobezi na kufikia wataalam 1,420 kutoka wataalam 768 katika miaka mitano iliyopita. Tumeona pia upande wa huduma za afya ya uzazi mama na mtoto, kumekuwa na ongezeko la uboreshaji wa miundombinu, pamoja na vifaa saidizi vya upasuaji ambavyo vimesababisha huduma hiyo kuimarika na sasa tunaona kwamba kiwango cha vifo vya akinamama vimeweza kupungua kutoka 556 mpaka 104 kwa vizazi hai 100,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa

sana na hii imesababisha kutambuliwa na taasisi za kimataifa za *The Gates Foundation* na amepewa *award* ambayo inatambulika kimataifa. Katika *award* hii amekuwa ni Rais wa kwanza katika Afrika kupata hii *award,* lakini pia duniani kwa mchango wake mkubwa katika kuimarisha huduma za afya ya uzazi wa mama na mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha mafanikio hayo ambayo tumeyaona ya uongozi uthabiti wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, pia kumekuwa na ongezeko la viwanda vya dawa ambavyo vimefikia 19 na viwanda vya afya tiba 141. Hili ni ongezeko kubwa sana ambalo kusema kweli linaendana na matarajio ya Rais katika miaka mitano ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la msingi ambalo ni mafanikio makubwa ambayo tumeyaona ni kwamba kupitia Wizara ya Afya tumeona kwamba Taasisi ya Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba *(TMDA)* imeweza kufikia viwango vikubwa vya umahiri katika ngazi za kimataifa ambazo zinatambuliwa na Shirika la Afya Duniani *(WHO)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonesha kwamba Serikali imewekeza vya kutosha katika uthibiti wa dawa na mpaka sasa hivi *TMDA* inatambulika kama taasisi kiongozi katika uthibiti wa huduma za dawa katika Afrika. Pongezi sana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo ya Wizara ya Afya, ninaomba pia nijikite katika mafanikio katika Jimbo la Muleba Kaskazini. Ukiangalia kwenye sekta ya afya pia sisi Muleba Kaskazini tumefaidika kwa kupokea bilioni 2.4 za ujenzi, ukarabati na upanuzi wa vituo vya kutolea huduma za afya 19 vikiwemo ujenzi wa zahanati nne na kituo kimoja cha afya ambacho kinakwenda kujengwa katika Kata ya Ngenge. Tunashukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa elimu pia tumeona mabadiliko makubwa sana na mafanikio makubwa

ambayo hayajawahi kuonekana siku za nyuma. Kwa mfano kwenye upande wa elimu Jimbo la Muleba Kaskazini tumejengewa madarasa mapya ya shule za msingi 14 na sekondari 13. Ukiacha hivyo tumeona pia ukamilishaji wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha *VETA* kilichopo Kata ya Kamachumu katika Jimbo la Muleba Kaskazini. Kwa ujumla Kagera tumefaidika na uwepo au kuanzishwa kwa Kampasi ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam katika Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio makubwa kwamba hii itaweka historia na kuwezesha wataalam wa kutosha wa kusaidia katika kushauri ukuaji wa uchumi katika Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho ni cha mafanikio makubwa ambacho tumekiona katika Mkoa wa Kagera ni suala la usambazaji wa huduma za umeme. Ni kwamba usambazaji wa huduma za umeme umeongezeka na ukiangalia kimsingi umeendana na vile vipaumbele ambavyo Mheshimiwa Rais katika hotuba yake alizungumzia katika ukurasa wa 29 wa hotuba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi katika Jimbo la Muleba Kaskazini tumefanikiwa, huduma za umeme zimefika katika vijiji 56 kati ya vijiji 64. Matarajio yetu ni kwamba katika miaka mitano ijayo basi tutapata ongezeko kufikishwa kwa umeme katika vijiji nane ambavyo vimebaki. Pia katika kipindi hiki cha miaka mitano iliyopita umeme umeweza kufika katika vitongoji 185, kati ya vitongoji 284 vya Jimbo la Muleba Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kikubwa cha kujivunia ni miaka mitano iliyopita, Serikali kupitia Halmashauri ya Muleba imeweza kuelekeza katika shamba la Mfano lililopo katika Kata ya Ruanga katika Kitongoji cha Makongoramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shamba hilo limewezesha vikundi nane vya vijana 57 ambapo shamba hilo lilianzishwa na Serikali pia limewezeshwa mbolea viuatilifu. Matarajio ni kwamba Wizara ya Vijana pamoja na Kilimo watashirikiana ili kuwezesha vijana zaidi kufaidika na shamba hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwamba kupitia uwezeshaji wake tumeweza kujenga barabara kilometa 164 kwa kupitia *TARURA* katika Jimbo la Muleba Kaskazini. Matarajio ni kwamba katika miaka mitano ijayo basi tutaendelea kusambaza zaidi mtandao wa barabara. Pia tunashukuru kwamba katika miaka mitano iliyopita Mheshimiwa Rais ametuwezesha kutenga kiasi cha shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa mwalo uliopo huku kwenye Kata ya Izigo katika eneo la Kiyamkwiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio hayo ni makubwa na Muleba Kaskazini tunajivunia sana. Ni matarajio yetu kwamba tutashirikiana na Mheshimiwa Rais kuona tunawezesha wananchi kiuchumi, ustawi wa jamii na kufikia malengo makubwa ya matarajio. Sisi Wanamuleba Kaskazini tunaendelea kumuunga mkono Rais na tunamwamini kwamba ni kiongozi shupavu na mwenye weledi na kiongozi ambaye anajali sana maridhiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Adonis Alfed Bitegeko, Mheshimiwa Khalid Mussa Nsekela, Mheshimiwa Dkt. Charles Sungura, Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando ajiandae.

**MHE. KHALID M. NSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia afya na uhai…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba samahani kwa sababu wachangiaji bado ni wengi tunapunguza muda kidogo. Kwa hiyo, jitahidini kwenda kwa muda, tutaweka dakika sita.

**MHE. KHALID M. NSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Ninaomba nichukue nafasi hii kushukuru Chama changu Cha Mapinduzi kikiongozwa na Mwenyekiti wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniteua mpaka nikawa mgombea

sasa nipo Mbunge wa Jimbo la Kyerwa. Niwashukuru pia wananchi wenzangu wa Jimbo la Kyerwa kwa kuniamini na kunituma niwe mwakilishi wao kwenye Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge la Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tuna muda maalum ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa mambo matatu; jambo la kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana, kura ambazo zilionyesha imani waliyonayo kwake lakini juu ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba nzuri aliyoitoa, hotuba ambayo ilijaa maono na dira na mwelekeo wa nchi yetu ya Tanzania ya kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Rais siyo tu kwa miradi mikubwa ikiwemo *SGR*, madaraja, miradi mingi sana, lakini ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa jinsi alivyorudisha imani na ndoto ya Watanzania wa hali ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatokea Jimbo la Kyerwa, kila nikizunguka nikikutana na mama ntilie wa vijijini kule Businde, vijana wajasiriamali wadogo wadogo bodaboda wa kule Kaishu Isingiro, kila nikikaa nao unaona kabisa na wale wafanyakazi wa kawaida unaona ni jinsi gani wameanza kuamini kwamba kesho yao ina nafasi katika Taifa lao la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na wenzangu wameongea mengi mazuri ambayo yamefanyika chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni mengi huwezi kurudia kuyaongea yote, lakini naomba niongee machache kwa Jimbo langu la Kyerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kyerwa sisi nguvu yetu ni kilimo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake ameweka sera nzuri, mifumo mizuri katika kilimo hasa kile ambacho kimegusa kahawa. Wakati hajaingia kahawa yetu ilikuwa inauzwa shilingi 1,000, lakini sasa tunavyoongea kahawa

inauzwa shilingi 5,000 mpaka 6,000 - 7,000, tunamshukuru sana. Ni kiongozi anayeahidi na kutenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ukienda kwenye barabara ni kilio cha muda mrefu cha wananchi wa Kyerwa na sasa tunavyoongea Barabara ya kutoka Rwemkorongo – Mkwenda – Itera – Murushaka kilometa 50 inajengwa kwa kiwango cha lami. Ingawa tunapenda na tunafurahi na tunatarajia kwamba Barabara itakayotoka Rwemkorongo – Isingiro – Kaisho – Kibisho – Mrongo kuunganisha Kyerwa na Uganda itapata lami katika uongozi huu unaofuata wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itatusaidia sisi kama wananchi wa Kyerwa kufungua biashara ya mpaka, biashara ya usafirishaji na kunyanyua uchumi wa Kyerwa. Tukienda kwenye afya, tumeshuhudia Mheshimiwa Rais akituletea hospitali ya Wilaya kubwa ambayo ina huduma nzuri na vifaa vya kutosha ingawa kwa sababu Kyerwa ina jiografia pana na kilometa zipo nyingi kati ya kituo na kituo tungetamani na tutafurahi kuona Kituo cha Nkwenda ambacho kimeanza kazi toka mwaka 1974 kinahudumia takribani wagonjwa 7,000 kwa mwezi kipandishwe hadhi kuwa Hospitali ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yapo mengi sana, tumeona miradi mingi karibia miradi 22 imekuja Kyerwa, miradi ya maji kuwatua ndoo kichwani akinamama wa Kyerwa. Ninashukuru kaka yangu Mheshimiwa Awesso anafanya kazi kubwa sana na ameshaniahidi kwamba awamu inayokuja hii tunaenda kumaliza tatizo la maji Kyerwa, tuna matarajio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukisoma hotuba imejaa maono, dira nzuri na mwelekeo. Kwa hiyo, tunaamini kwa sababu tumeshuhudia yale mazuri ambayo tumeyaona yametendeka na tunaamini aliyoahidi kwenye hotuba yote yanaenda kutendeka bila kuacha chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sababu ya muda ninaomba nichangie kidogo kwenye hotuba nzuri kabisa ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ninachangia eneo moja linalohusu vijana. Kama kijana mwenzao, ukisoma hotuba hii ukurasa wa 13, ninanukuu "Kwa matamshi yake na kwa kutambua takwimu amesema Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba, kwa kuwa zaidi ya 60% ya watu wa nchi hii ni vijana, tutaweka kipaumbele kwenye sera na *program* zitakazopanua fursa za kiuchumi, kutengeneza kazi na ajira, kuongeza wigo wa hifadhi ya jamii za kuwajengea kesho iliyokuwa bora zaidi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka kwenye hii nukuu nami ninajifunza kwamba Rais na ninampongeza ni kwamba ana masilahi mapana na kesho ya Tanzania hii hasa kesho ya vijana. Vijana katika Taifa hili ni rasilimali kama nyingine, ni kundi kubwa. Tunafurahi tuna nchi ambayo imejaa rasilimali kama madini, ardhi, sijui dhahabu, gesi. Kundi kubwa la vijana ni utajiri kama wanavyoona dhahabu, kama wanavyoona gesi, pale utakapokuwa umetumia kundi hilo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapo Mheshimiwa Rais anaonesha kabisa maslahi mapana aliyonayo juu ya kundi hili la vijana kwa sababu tunaamini kesho yetu imekaa mikononi mwa vijana na Taifa letu la kesho lipo mikononi mwa vijana. Kwa hiyo, nami kama kijana nikaona nitoe rai kwamba ni muda muafaka sasa ili twende vizuri na maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika hotuba yake na kulingana na dira ya Taifa, yote yaliyomo ni muda muafaka sasa kwamba kila wizara, taasisi na idara zifungamanishe na vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, kwa maono haya tukifungamanisha na vijana kwa kila taasisi, kila Wizara na kila idara hapa tunaweka uwekezaji wa kimkakati wa kulinda Taifa letu la kesho na si uwekezaji holela. Rafiki yangu, Mheshimiwa Profesa Muhongo ametoa takwimu nyingi sana 2030 inavyoonekana 40% ya vijana duniani itakuwa iko Afrika, hebu fikiria ushindani ambao tutakuwa nao kama vijana wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo hili tulichukue kimkakati na ukiniruhusu lisiwe jambo la hiari la kufungamanisha vijana na idara hizi, bali kiwe ni kigezo cha utendaji kwamba kila hoja ya sera au bajeti ijibu swali kwamba je, tunatengeneza ajira ngapi za vijana? Ni kandarasi ngapi zinaenda kwa vijana? Ni biashara ngapi za vijana zinaenda kwenye mnyororo wa thamani wa kazi za Serikali na biashara ya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Charles Sungura, Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando, Mheshimiwa Haiderali Hussein Gulamali na Mheshimiwa Masanja Kadogosa wajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES J. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ameniwezesha leo kusimama mbele yako hapa. Pili, nimshukuru sana na nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana na wananchi wangu wa Wilaya ya Handeni. Jambo la tatu, ninawashukuru sana wananchi wa Wilaya ya Handeni kwa upendo wao mkubwa wa kunichagua mimi kama mwakilishi wao, lakini niwaambie kwamba nitawahudumia na nitawapigania sana kwa moyo wangu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikichangia moja kwa moja katika hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ukienda ukurasa namba 24 ninaomba ninukuu maneno yake, amesema: "Tunapoanza safari ya muhula wa pili wa miaka mitano ya awamu ya sita, tumejipanga kuweka kongani ya viwanda katika kila wilaya ili kuongeza thamani ya mazao."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikupe taarifa kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alikuwa mbele ya muda; tayari kongani ya viwanda imeanza katika Jimbo langu la Handeni. Jimbo la Handeni tuna wakulima wa mkonge takribani 6,120, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amewaona hawa

wakulima hivyo aliwaahidi kuwaletea viwanda vitatu vya kuchakata mkonge (Viwanda vya Korona). Ninaomba nikwambie mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba, tayari kiwanda kimoja kimeshajengwa na kinakabidhiwa mwezi ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda hicho kina thamani ya shilingi bilioni 1.3, lakini pia kina uwezo wa kuchakata mkonge *cubic meters* 390 kwa siku. Kiwanda hiki kitawanufaisha sana wananchi wa Kwedizinga, Kata ya Segera, Kata ya Kabuku, Kata ya Mgambo, Kata ya Kwamgwe, Kata ya Ndolwa na Kata ya Kwamkonga. Vilevile, hajaishia hapo tu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tayari ameshatuletea shilingi bilioni nne kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vingine viwili vya mkonge. Viwanda hivi ni vikubwa kwa sababu vitaweza kuchakata *cubic meters* za majani 450 kwa siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha kwanza kitajengwa Kata ya Kwamatuku. Kiwanda hiki kitanufaisha wananchi wa Kata ya Kang'ata, Kata ya Kiva, Kata ya Magamba, Kata ya Kwa Honje, Kata ya Misima na Kata ya Sindeni. Mwaka huu wa fedha michakato imeshaanza ya ujenzi wa kiwanda hiki. Kiwanda cha mwisho cha tatu ambacho ndiyo mahitaji ya Jimbo la Handeni, ni kiwanda ambacho kitajengwa katika Kata ya Mkata. Kiwanda hiki kina thamani ya shilingi bilioni mbili nacho kina uwezo wa kuchakata *cubic meters* za majani ya mkonge 450 kwa siku. Nacho kitanufaisha wananchi wa Kata ya Kwachaga, Mazingara, Mkata, Sunga, Kwamsisi na Kitumbi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni bingwa sana, hajaishia hapo tayari tarehe 4 Desemba, 2025 ametukabidhi kiwanda kipya cha kuchakata mihogo. Kiwanda hiki kina uwezo wa kuchakata kwa siku tani 12 na *output* yake ambayo ni unga wa muhogo, ni tani tatu. Hivyo, tayari sasa hivi anatafutwa mwekezaji wa kuweza *ku-run* kiwanda kile. Kwa hiyo, tumshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa hiyo, jumla ya viwanda vyote hivi vinne, viwili ambavyo vimeshakamilika na hivi vingine viwili ambavyo vipo kwenye mchakato wa kujengwa; vitaajiri takribani ajira za moja kwa moja 800 mpaka 1,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na *radius* na umbali wa kiwanda kutoka kwa wakulima ni takribani kilometa moja mpaka kilometa 50, kwa maana hiyo hata upelekaji wa mazao yao katika viwanda utakuwa ni wa bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ombi moja la kuomba kiwanda cha machungwa katika Kata ya Mkumburu na Kata ya Mzundu. Kata hizi mbili zina wakulima wenye hekta za machungwa takribani 17,876, lakini kwa mwaka tarafa hizi mbili zinazalisha tani 591,000 za machungwa. Hivyo, ninadhani kuna haja wananchi hawa kufikiriwa kwa kuwekwa kiwanda cha kuchakata machungwa ili tuendane na azma ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kwamba tunaongeza thamani ya mazao yanayozalishwa na wakulima hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lingine niombe vijana wetu walioko katika Jimbo la Handeni, wapewe ardhi ambayo ina hati moja kwa moja ili waweze kunufaika na viwanda hivi ambavyo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anaendelea kuvijenga katika Jimbo la Handeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lingine, ukiangalia ukurasa wa 20, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema: "Tutaanzisha vituo vya kukodisha zana za kilimo." Ninaomba Wizara ya Kilimo muanzishe kituo cha kukodisha zana za kilimo katika Jimbo la Handeni, ili vijana wetu waweze kunufaika na watumie gharama ndogo katika kilimo chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea katika upande wa umwagiliaji katika ukurasa namba 20 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema: "Tutaongeza eneo la umwagiliaji kutoka ekari 3.4 milioni mpaka milioni tano." Ninaomba niwaambie kwamba Jimbo la Handeni na sisi tumo katika mchakato huu; kwa sababu tayari mipango ya ujenzi wa *skim* 11 za umwagiliaji tayari upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo *skim* ambazo zimegawanyika katika makundi matatu. Kundi la kwanza, ni *skim*

zinazotegemea maji ya Mto Pangani na Mto Mnyusi. *Skim* hii ina ukubwa wa hekta 500 na ipo katika eneo la Masatu (Segela), ina thamani ya shilingi bilioni 28 na mpaka dakika hii mwaka 2024 *feasibility study* na *design* tayari imeshafanyika. Hivyo, niombe Wizara ya Kilimo itusaidie kutangaza *tender* kwa haraka ili wananchi hawa waweze kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la pili ni *skim* ambazo zinatokana na uchimbaji wa mabwawa. Tayari shilingi bilioni 1.2 zimeshatolewa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kwamba *feasibility study, design* na *topographic survey* inafanyika. Ninavyozunguza hapa tayari imeshafanyika hivyo, maeneo ya Magamba, Kwengoma, Kale na Kibaya-Misima tayari watafaidika na *skim* hii ya mambwawa. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu anaupiga mwingi Jimbo la Handeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la tatu ni *skim* zinazotegemea visima virefu, tayari mitambo 19 imeshanunuliwa kwa upande wa Kaskazini na sasa hivi ina *operate* Arusha. Tumeambiwa kuanzia mwezi Mei mitambo hii, itahamia Mkoa wa Tanga na hatimaye Jimbo la Handeni. Kwa hiyo, maeneo kama Mungwi, maeneo kama Kwenkwale, Mandela pamoja na Kwanyanje Kata ya Kwasunga, watanufaika na visima virefu kama *skim* za umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ninaomba niseme kwamba, Jimbo la Handeni sisi ni wafugaji. Ni wafugaji wazuri wa ngo'mbe, mbuzi, pia na kondoo. Tunao ng'ombe 140,473, tuna mbuzi 200,939 pamoja na kondoo 38,755. Ukisoma *page* namba 22 katika hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema kwamba: *"Tutoke kwenye kumtazama ng'ombe na mlio wake, lakini tumtazame na uzito wa nyama, tumtazame na ladha ya nyama, lakini pia tutazame na wingi wa maziwa."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Charles. Tunaendelea na Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando, Mheshimiwa Haiderali Hussein Gulamali ajiandae.

**MHE. SALEHE M. MHANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninaomba nishukuru kupata nafasi hii niweze kuwa mchangiaji katika hotuba ya Mheshimiwa Rais. Ninamshukuru Mwenyezi sana Mungu kwa kunipa baraka hii na kibali hiki. Ninaomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama chetu Chama Cha Mapinduzi, kwa kuweza kunipa imani na mimi kuweza kuniteua na kugombea katika Jimbo la Kilindi, Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii na kwa unyenyekevu mkubwa niweze kuwashukuru sana wapigakura wa Jimbo la Kilindi kwa imani kubwa waliyoonesha kwangu, nami ninaomba niwaahidi nitafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kwamba ninakwenda kukidhi matarajio ya Wanakilindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kuungana na Wabunge wenzangu kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita kwa miaka minne. Kazi alizofanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa Wanakilindi ambao ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeelezwa kwa kirefu kabisa na wachangiaji wengine Wabunge wenzangu katika majimbo mbalimbali hapa nchini. Hata hivyo, ninaomba niseme Wanakilindi wanashukuru sana kwa wema waliotendewa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika sekta mbalimbali katika Jimbo letu la Kilindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, tuwe wa kweli na Watanzania ninaomba wanisikilize. Katika wakati ambao Taifa letu limepata baraka ni kupitia kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ni miujiza imejitokeza, huwa siyo rahisi sana kutekeleza miradi ya kimkakati kwa kiwango ambacho kimefanyika, lakini wakati huohuo inatekelezwa miradi katika sekta za uzalishaji kwa

kiwango ambacho hakijawai kutarajiwa. Pia, wakati huohuo inatekelezwa sekta za kutoa huduma za kijamii, elimu, maji na afya kwa wakati mmoja. Ninawaomba wanataaluma tutafakari na kuangalia kiwango cha uwezo wa hali ya juu cha uongozi alichonacho Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakwenda kuona katika kipindi cha miaka mitano ikiwemo katika Jimbo la Kilindi, wananchi wanakwenda kupata huduma mpaka watoto wadogo wanaimba Mama Samia. Ukiona mahali popote kiongozi katika ngazi yako unaimbiwa na watoto, wewe una baraka za Mwenyezi Mungu na unatenda mema kwenye jamii yako. Tunakushukuru sana kwa miradi ya maji, Mradi wa Diburuma bilioni 22.9 unaokwenda kutatua tatizo la maji katika kata sita, katika Jimbo la Kilindi kwenye Tarafa ya Kwekivu, bilioni 6.9 katika Mradi wa Kwamaligwa Kata ya Kibirashi, vijiji sita na maeneo mengine kadha wakadha. Kwa sababu ya muda ninaomba niishie hapo itoshe kusema, tunamwombea kila la heri katika miaka hii mitano Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ili afanye yale aliyodhamiria na aende akaandikwe kwa wino wa dhahabu kwenye Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ninaomba nirudi kwenye hotuba ya Rais aliyoitoa katika Bunge letu la Kumi na Tatu mwezi Novemba. Ninaomba nianze kwa kutanguliza kabisa kuunga mkono hoja hotuba hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ninaunga mkono kwa sababu ukurasa wa 28 kwa Wanakilindi unakwenda kuleta tabasamu, amesema na amekazia anataka anapomaliza mwaka 2030, makao makuu ya wilaya zote yaunganishwe kwa kiwango cha lami na makao makuu ya mikoa. Eneo hili ni mojawapo linalokwenda kuwagusa wananchi wa Jimbo la Kilindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee tunamshukuru kwa sababu alishaanza dhamira hii. Tayari kilometa 20 kutoka Handeni Mafuleta mkandarasi ameanza kazi, tayari kuna mkataba umesainiwa wa mkandarasi kutoka Mafuleta kwenda Kileguru kilometa 30, safari ya kwenda kilometa 113 hadi Makao Makuu ya

Wilaya, Songe yameanza kwa dhamira ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Niiombe Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Ujenzi, tufanye jitihada kuhakikisha kwamba tunatoa fedha, wakandarasi wale warudi *site*, kazi iendelee. Kazi na utu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iende ikawafikie wananchi wa Jimbo la Kilindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 24 na hili ninaomba niliwekee uzito, kwa maana kwamba nayashuhudia mapinduzi ya kilimo katika nchi hii kupitia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa mikakati hii na malengo na dhamira ya Dkt. Samia Suluhu Hassan tunakwenda kushuhudia mapinduzi makubwa katika sekta ya mifugo na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe rai Wizara hizi za kisekta ziende zikasomane vizuri na hapa ninaomba niongezee hasahasa Wizara ya Viwanda na Biashara, baada ya mapinduzi ya kilimo, kinachopokea ni mapinduzi ya viwanda. Kwa hiyo, lazima sasa hivi sekta ya viwanda iende ikajipange na sisi tupo tayari kule kwenye majimbo yetu kuandaa maeneo ya kongani za viwanda ili kusudi sasa mazao ya wakulima yachakatwe kule kule kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapochakata mahindi badala ya kuuza mahindi ghafi, unatoa mpaka pumba maana yake unazorotesha sekta ya mifugo. Tunataka kwenda kwenye ufugaji kibiashara kwa unenepeshaji wa mifugo. Moja ya eneo linalochangia kunenepesha mifugo ni upatikanaji wa pumba za mahindi. Ukisafirisha mahindi umezorotesha lengo la uboreshaji wa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, suala la uchakataji wa mazao ya mpunga, ukisafirisha mpunga umeondoa pumba inaenda kunufaisha mataifa mengine, kunenepesha mifugo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Mawaziri wa kisekta ninaomba twende tukatafsiri uanzishwaji wa viwanda vidogovidogo, viwanda vya kati kwenye maeneo ya uzalishaji ili kujenga mnyororo wa thamani na kuweka uhakika wa masoko kwa wakulima wetu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. SALEHE M. MHANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa sababu ya muda, ninaomba kuunga mkono hoja. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Salehe Mhando. Nilimtaja Mheshimiwa Haiderali Hussein Gulamali, Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa na Mheshimiwa Zeyana Abdallah Hamid wajiandae.

**MHE. HAIDERALI H. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nianzie kwa kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa kama Mwenyekiti wetu. Pia, nichukue nafasi hiyo kukupa pole sana pamoja na Wabunge wote waliopo hapa kwa kuondokewa na Wabunge wenzetu ambao wametangulia mbele ya haki, tuna kila sababu ya kuwaombea Mungu awaweke mahali pema peponi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi kuchangia hotuba ya Rais. Ninaona watu wengi kuanzia asubuhi, toka siku tumeanza kila mmoja anazungumzia maono ya Rais, mafanikio ambayo ametuletea, dira ambayo anayo na dhima ambayo anayo kwa ajili ya Watanzania. Hakika Mheshimiwa Rais anatuletea haki sawa kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema hivo haki sawa kwa kila Mtanzania, ukiangalia kwamba katika sekta yoyote ile tunapotaka kulipa kitu chochote kuna *control number,* hiyo *control number* inakupa haki ya kwako wewe kulipia na zile fedha zinaingia moja kwa moja katika Mfuko wa Serikali bila kupitia njia ambazo hazitakiwi. Kwa hilo, kwa kweli tuwapongeze ni kazi kubwa sana ambayo Serikali wamebuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake Mheshimiwa Rais alizungumza kati ya Wabunge 393, Wabunge 223 ni Wabunge wapya na wanawake ni zaidi ya 40.5%. Kwa hiyo,

Mama kwa kweli amewapendelea sana, kwa hiyo niwapongeze kwamba hii ndiyo demokrasia ambayo Tanzania imetuletea. Hata hivyo, hapahapa tukiangalia Mawaziri ambao wamepata uteuzi ni wale ambao hawajaangaliwa kwenye uzoefu wao tu, lakini wamengaliwa kuwezo wao. Mawaziri wengi na Naibu Mawaziri wengi tunaona wengi ni wapya na kwa pamoja tunaona wameanza wanachapa kazi vizuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kuteuliwa katika nafasi hiyo hakika Singida tunajivunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia Nchi yetu ya Tanzania ilimepiga hatua katika kila sekta. Ninakumbuka kwamba, Awamu ya Sita kipindi cha kwanza mama alivyopokea hii nchi alisema, sasa anaenda kuifungua nchi na kweli, ameifungua kwa vitendo siyo kwa maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina kila sababu ya kujivunia kwamba, nchi yetu imepiga hatua na tukitaka kuona kwa vitendo tuangalie mapato yalivyokusanywa, ni mengi na yameongezeka. Kariakoo ambayo wafanyabiashara walikuwa wanasema kwamba, imefungwa kwa sababu moja au nyingine, leo imefunguliwa. Ukiangalia kila wakati uchumi wa nchi unakua, nenda ukaangalie viwanda vya *cement* kama vinafanya kazi au laah! Ukipita kila kona utaona vijana wanafyatua matofali, hii inadhihirisha nini? Kwamba, uchumi unakua, watu wanajenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kipindi ilifika kwamba, wajenzi walikuwa wanapumzika hawaendelezi majengo kwa namna moja au nyingine, lakini mama aliposhika nchi ile dira ilibadilika kabisa. Sasa hivi watu wanakosa muda, wanapiga kazi kwa hiyo, nina kila sababu ya kumpongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia Sekta ya Usafirishaji, Tanzania tulikuwa tuna ndoto ya kupata treni ya umeme, leo saa tatu tu tunafika Bungeni; haya yote yanatokana na nini, yanatokana na kazi nzuri, lakini akiwa mama. Nikisema mama

moja na nusu, nitakuwa sijakosea. Nina kila sababu ya kutamka *what a man couldn't do a woman could do better* kwa sababu, kazi ambayo hayati John Pombe Magufuli alipoachia, watu walikuwa wana mashaka kwamba, huyu mama kweli ataweza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mama ameonesha kwa vitendo; miradi yote, yale ambayo Mheshimiwa John Pombe Magufuli alianzisha ameyakamilisha kwa nguvu zote na kwa kipindi cha miaka minne tu. Watanzania wana akili zao, Watanzania wamekomaa kisiasa, Watanzania wana elimu ya kutosha, kama wanaenda kutoa asilimia 98 kwa Mheshimiwa Rais na Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi wana uhakika kwamba, kazi yao wameiona kwa vitendo na siyo kwa maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisizungumzie mengi kwa sababu, waliopita wameshachangia na mimi nitakuwa nachangia hayohayo. Kwa hiyo, ninajaribu kuzungumzia yale machache ambayo hayajazungumzwa na Wabunge wenzangu waliotutangualia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia leo Sekta ya Madini, juzi tumemwona Mheshimiwa Mavunde anatangaza shilingi trilioni zimekusanywa, lakini Wachimbaji Wadogo ambao ni vijana kwa ujumla, kama kuna sehemu au kuna kipindi wamefanikiwa ni kipindi cha mama Samia Suluhu Hassan. Hakuna kipindi ambacho imetokea, katika awamu zote, Wachimbaji Wadogo ndiyo wamepata kibali na leseni ya kuchimba madini, lakini wamepata na wamepiga hatua. Hii inadhihirisha kwamba, mama anapiga vita umaskini kwa vitendo siyo kwa maneno. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haiderali, ahsante sana. Muda wako umekwisha.

**MHE. HAIDERALI H. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa, Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid ajiandae.

**MHE. MASANJA K. KADOGOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa fursa hii. Kwanza ninaanza kwa kuunga mkono hoja kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na kutuwezesha kuwa katika jumba hili. Tatu, ninakishukuru chama changu, chini ya Mwenyekiti wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kunipa fursa ya kupeperusha bendera Bariadi Vijijini na hatimaye wananchi wenzangu kuona ninafaa kuwawakilisha katika jumba hili, katika Bunge hili, la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninakushukuru wewe, Kiti chako, kwa kunipa hii fursa ya kusimama humu. Tunajadili hotuba ya Mheshimiwa Rais, kwa vigezo vyovyote vile hii ni hotuba muhimu sana katika Taifa letu; kwanza, ni hotuba ambayo inatupa *roadmap* au inatuanzisha kutekeleza Dira ya 2025 – 2050, lakini la pili, ni hotuba ambayo inatueleza tulikotoka, tulipo, tunaenda wapi na tunafikajefikaje huko tunakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii imejaa maono. Kazi ya kwanza ya kiongozi kwenye jamii au Taifa ni kutoa maono na unajua kwamba, vitabu vya Mwenyezi Mungu vinasema pasipo maono watu huangamia. Kwa maana nyingine ni pasipo maono Taifa linaangamia kwa hiyo, hotuba hii ina maono, kwa Kisukuma *Vision* na itaishi kwa miaka mingine pengine 25 na zaidi inayokuja. Kama ambavyo mpaka sasahivi tunamzungumzia Mheshimiwa, Hayati Benjamin Mkapa, Rais wetu wa Tatu kwa sababu, ndiyo dira ambayo tunaizungumzia mpaka sasahivi na utekelezaji wake na hii itakuwa hivyohivyo katika Bunge hili miaka 25 inayokuja tutakuwa tunamzungumzia Samia hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mengi ambayo yamefanyika, kutokana na muda labda nianze kwa upande wa Jimbo la Bariadi Vijijini, wakati tupo Bariadi kwa maana ya jimbo moja, lakini kwa Bariadi Vijijini peke yake tumepata zaidi ya shilingi bilioni 82 ambazo zimeenda katika shughuli mbalimbali. Sasa kwa vijijini tuna shughuli mbili tu, sisi ni wakulima na wafugaji kwa hiyo,

kuna ruzuku, pesa zile zimeenda kwenye ruzuku na nyingine zimeenda kwenye chanjo, shule, zahanati na barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunamshukuru sana Mheshimwia Rais kwa maono haya ambayo amekuja nayo kwamba, ataongeza malisho kwa sisi wafugaji kutoka ekari milioni 3.4 mpaka ekari milioni sita, hiyo ni neema kwetu. La pili, ni kuongeza ekari za umwagiliaji kutoka ekari milioni 3.4 mpaka milioni tano. Ninapenda kuona kwamba, katika shemu hii tufike mahali, kama Taifa kwamba, utegemezi wetu wa chakula cha kutosheleza utokane na kilimo cha umwagiliaji, hapo tutakuwa tumefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda katika mambo ya Kitaifa. Yamefanyika mambo mengi sana, wenzangu wamezungumza hapa nisingependa kuyarudia, lakini ukiangalia katika Sekta ya Usafiri na Usafirishaji yapo mengi sana yamefanyika; kuna upanuzi wa bandari, ujenzi wa barabara, ujenzi wa reli, *SGR,* ambapo pesa nyingi sana imeenda huko na kuna mipango ya kuiendeleza, hii *SGR,* ifike Kigoma – Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mkongo wa Taifa na vilevile kuimarisha Shirika letu la Ndege. Hivi vitu ni muhimu sana katika Taifa tunaposema kwamba, miundombinu ya usafirishaji ni kama mishipa iliyopo kwa binadamu ina maana hiyo hiyo katika uchumi. Tunapokuwa na miundombinu imara tunaweza kujenga viwanda, tunaweza kufanya kilimo chetu kiwe cha kibiashara na tunaweza kufanya sekta nyingine, kama madini, kuwa na tija zaidi katika Taifa. Vilevile Mheshimiwa Rais katika maono yake anaongeza nishati ya umeme wetu kutoka megawati 4,000 mpaka 8,000 kwa maana ya mpaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni katika uchumi ambao tunataka kuujenga, kwa maono ya Mheshimiwa Rais wa dola trilioni moja mwaka 2050 ni kwamba, katika uchumi kama huu tutahitaji siyo chini ya megawati 70,000. Kwa maana nyingine ni kama tuna-*double* 2025 - 2030 maana yake ni tukiendelea ku-*double* mpaka tunapofika 2045 tutakuwa na megawati takribani 60 *plus*. Hiyo itatufanya sisi, kama Taifa, tuweze kwenda vizuri kwa

sababu, bila kuwa na nishati inayotosheleza, hayo maendeleo tunayoyatarajia hayawezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimalizie na suala la kisera zaidi; ukiangalia *Public (Public Finance)* na *Private Sector* zinashabihiana, yaani huwezi ukawa na *Public Sector* ambayo iko *strong* bila kuwa na *Private Sector* ambayo ipo *strong*. Ina maana gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba, *Public Sector* ina-*unlock potential* ya *Private Sector* kwa maana ya uwekezaji kibajeti, lakini kuna kutunga sheria au kuondoa sheria ambazo zinaleta matatizo kwenye *Private Sector*. Kuna kubadilisha kanuni na kuweka sera ambazo zinawezesha *Private Sector* kuweza ku-*flourish,* kwa uchumi ambao tunauendea sasa, *one trillion,* ambao tunautegemea sasa, *growth* ni lazima iwe *somewhere above 10%* na pengine wakati mwingine iende kwenye *15 plus* kwa sababu, haiwezekani kila mwaka tukaenda *constant*. Kuna mwaka tutaenda chini, kuna mwaka tutaenda juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tuweze ku-*sustain* ni lazima tuwe na malengo ya kukua kwa asilimia 13/13 katika miaka mingine. Sasa hiyo ina maana gani, maana yake ni tutahitaji mabadiliko makubwa ya kisera katika *Private Sector* na mabadiliko haya tusiyaone katika jicho la kitaasisi kwa sababu, ni rahisi sana kusema kwamba, tunataka kubadilisha mashirika yafanye hivi, hiyo ni *efficiency*. Lazima tuangalie Wizara, Sera, Sheria na Kanuni zilizopo kwa sababu, unaweza ukakuta pengine wanasema uchukuzi wana maono makubwa sana ya kwenda mpaka nje ya nchi, lakini ukakuta tatizo linatokea Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, pengine Sheria za *Immigration* zina matatizo au unaweza ukakuta kuna Sheria za Kikodi ambazo zinafanya uchukuzi wasiweze kufikia malengo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoweza kusema hapa ni kwamba, tutahitaji mabadiliko makubwa. Uchumi wa trilioni moja mpaka sasa hivi ni nchi 22 tu duniani zimeweza

kuufikia. Ili tuweze kufikia huko, kama Taifa, ni lazima tuwe kitu kingine kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, ninakushukuru sana. Ninajua umenivumilia, unataka kuniambia nimemaliza muda wangu. Ninakushukuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa, ahsante sana.

Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid na Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu. Mheshimiwa Bazilio Kapunda Mbwilo ajiandae.

**MHE. ZEYANA ABDALLAH HAMID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa nasi wote hapa katika Bunge nikiwa ninalihutubia kwa mara ya kwanza. Binafsi ninamshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kunichagua kupitia Kamati Kuu ya CCM na kuniamini kwamba, nina uwezo na nia thabiti ya kuja kuzisemea na kuzisaidia taasisi zetu za vyuo na vyuo vikuu, hususan vijana wetu ambao wametawanyika Tanzania nzima wakitafuta maendeleo. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshatuonesha mwanga huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru Wabunge wenzetu, kwanza tujipongeze kwa kuwepo hapa hii leo, kwamba, haukuwa uchaguzi mwepesi, lakini tumeunga mkono juhudi za Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumezisemea kinagaubaga, tumeamini kwamba, hapa tutavuka na kazi iendelee. Pia, ninashukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuwekea viongozi bora katika Serikali hii, Mawaziri wetu waliochaguliwa wakiongozwa na Dkt. Emmanuel Nchimbi pamoja na Dkt. Mwigulu Nchemba na pia, kwako wewe kwa kuweza kuwa Mwenyekiti siku hii ya leo na katika awamu hii kuwa Mwenyekiti wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niende kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyohutubia tarehe 14 Novemba, 2025, ambayo ilifungamanisha dira, maono na utekelezaji

uliotukuka wa Ilani na kuweza kututayarisha Watanzania kwenye yanayokuja katika awamu hii. Mimi ni mdau wa elimu na ninaomba kuanza moja kwa moja kwenye niliyoyaona na yaliyonigusa kwenye elimu, ndani ya hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amejikita kuleta mapinduzi ya elimu hasa kwa kuwekeza kwenye *STEM* (Sayansi, Teknolojia na Hisabati). Uwekezaji huu mkubwa unaitayarisha Tanzania kutumia sayansi na kusomesha data sayansi, akiliunde, teknolojia ya viwanda ambapo Tanzania imeshapiga hatua katika miaka minne/mitano hii iliyopita na *Vision* ya 2050 inatuonesha kule ambako tunahitaji kufika. Tukidhani kwamba, dunia ndiyo iliyokuwa inaenda kasi kwenye kubadilisha elimu kutoka *content* kwenda kwenye *competence,* lakini katika hotuba hii tumeona nalo hilo limepewa kipaumbele, kutoa vijana ambao siyo tu wanakuwa wasomi wa nadharia bali wasomi wa teknolojia wakiwa na *skills* muhimu zinazohitajika hivisasa kwenye sekta na kwenye maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiiangalia kwa kina hotuba ya Mheshimiwa Rais siyo shida kuona kwamba, alizunguka kote duniani kukokoa yale yote ambayo tunadhani hayawezekani kwa Tanzania kwa wakati huu, lakini aliyotuletea yanatuhitaji sana sisi kwa sababu, yeye kazi yake ya kutuletea mlangoni ameshamaliza. Ni sisi Wabunge, kupitia Serikali, tunaohitajika kuyafikisha kwa wananchi, tunahitajika kuyachakata kwa vijana, inawezekana sana hawajapata bado kuona kwa ndani Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amedhamiria nini kwa Tanzania. Nikiangalia hotuba hii ninaona moja kwa moja hii ndiyo awamu tuliyoagana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye elimu. Ukiangalia uwekezaji kwenye miundombinu Tanzania hii leo inakwenda kujivunia chuo kikuu katika kila mkoa, tunakwenda kujivunia vyuo vya kati vya *VETA* katika kila Wilaya, lakini siyo tu miundombinu ya vyuo hivi, Dkt. Samia Suluhu Hassan ametutayarisha kwamba, vitawekwa vifaa vya usomeshaji vya kidigitaji na zitamiminika ajira za vyuo; na tayari ajira zimeendelea kutangazwa. Katika kila chuo kwa hivisasa Tanzania tunahitimisha wanafunzi 300,000 wanafunzi

hawa wanakuja katika ajira ambazo tayari zinawasubiri na zimewezeshwa kwa viwango vikubwa vya fedha na katika mapinduzi makubwa ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Samia Scholarship.* Hili ni kapu ambalo Watanzania wanaendelea kunufaika sana, watoto wetu takribani 1,051 wamekuwa wanufaika wa *scholarship* hizi ambazo zimejikita kwenda kuleta mapinduzi ya sayansi na teknolojia katika kila Sekta. Tumeona wataalam wa kisasa wa ndani na nje wakishirikiana na vyuo vyetu na hata wanaosafiri kwenda nje na kurudi nyumbani wamekuwa pia, ni fursa ya kumwongezea nguvu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba, anayoyadhania na anayoyaona kwa Tanzania, Watanzania wenyewe wapo tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewaona vijana wakishiriki kwa namna tofauti katika *innovation,* lakini pia, wametumika katika njia ambazo sizo tulizokusudia, hata hivyo ninaichukulia *positively.* Tumejifunza umahiri wa vijana hawa, tutaendelea kuwatumia katika uzalishaji, katika ubadilishaji wa Taifa letu na katika kushiriki katika kunyanyua uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa rai kwa sote ambao tuko hapa tunaoshiriki miradi tofauti ya mendeleo na hasa Wizara zinazohusika kwenye uwekezaji. Vijana wetu wa Tanzania wana kila haki ya kufungamanishwa na kuambatanishwa na sayansi ambayo tunaipata kutokana na *investment* zinazokuja ndani ya Tanzania, inawezekana ndiyo nia ya kila mtendaji, lakini uwepo wa *frameworks* ambazo zinahakikisha ku-*monitor* kwa namba, kuweza kuwafuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona katika mipango ya Wizara ya Elimu kuna takribani fursa laki tatu za kuwahusisha vijana kwenye *internships au apprenticeship*, lakini inawezekana sana ikiwekewa mafungu mahsusi ya kuona mchango wao umeingia vipi katika hii sayansi na teknolojia. Hapa kuna fursa katika uvuvi, kuna fursa katika viwanda katika kilimo na fursa hizi ndizo zitakazoleta hamasa hata wale ambao walijihesabu wameshatoka katika njia rasmi za elimu watake kurudi kwa sababu zitakuwa ni fursa za wazi kwa wazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid.

**MHE. ZEYANA ABDALLAH HAMID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nitaomba kesho kuongezea kwenye afya kwa vile mimi nimo kwenye Kamati ya Afya, lakini ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu, Mheshimiwa Bazilio Kapunda Mbwilo, Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, ajiandae.

**MHE. DOTTO J. BAHEMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili kuchangia katika hotuba nzuri ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Rais wetu wakati akilifungua Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwanza kwa kukishukuru chama changu Chama Cha Mapinduzi kwa kukubali kuniteua kupeperusha bendera kugombea nafasi ya Ubunge katika Jimbo letu la Ngara. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ndiye alikuwa Kiongozi wa vikao vyote vikubwa ambavyo vilifanya maamuzi ya kuweza kuniteua mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba vilevile niwashukuru sana wananchi wenzangu wa Jimbo la Ngara ambao waliona kabisa ninatosha na wakanichagua kwa kura nyingi kuweza kuwa Mbunge wa Jimbo la Ngara. Ninaomba niendelee kuwaahidi kama nilivyowaahidi katika kampeni kwamba nitakuwa mtumishi wao, siku zote nitafanya kazi kwa kuweza kuzingatia maslahi mapana ya wananchi wa Jimbo la Ngara. Hata Mheshimiwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa kampeni alivyokuja kunikabidhi Ilani aliniambia, mwanangu nenda kawatumikie watu wa Ngara wana imani kubwa sana na wewe. Ile sauti ya Mheshimiwa Rais imekuwa ikinirudia mara kwa mara, kwa hiyo, ninaomba niwaahidi kwamba, hicho ndicho nitakwenda kukifanya katika Jimbo letu la Ngara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze sana Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ushindi mkubwa sana wa kishindo alioupata katika uchaguzi wetu uliopita wa mwaka 2025. Sisi watu wa Ngara tulikuwa tumejipanga na Chama changu Cha Mapinduzi tukiamini kwamba tunakwenda kuvunja rekodi ya kumpa kura nyingi Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini haikuwa hivyo kwa sababu, kumbe mengi ambayo ameyafanya katika Jimbo letu la Ngara ameyafanya nchi nzima, kwa hiyo Majimbo mengi yamempigia kura nyingi Dkt. Samia Suluhu Hassan, nasi tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri miongoni mwa sifa za kupiga kura ni uwe na umri wa kuanzia miaka 18, sasa watu waliopiga kura wakiwa na umri wa miaka 18 wengi wana akili ya kuweza kujua yale ambayo amefanya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha miaka minne iliyopita ndiyo maana amepata ushindi wa kishindo Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba vilevile nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa uteuzi wa viongozi alioufanya hivi karibuni, kwanza kwa kuteua Mawaziri ambao wanachapa kazi, Mawaziri wanyenyekevu, Mawaziri ambao ni wasikivu, kila siku tukizunguka huku na kule Mawaziri wapo kazini wanasikiliza shida za wananchi, wanatatua kero za wananchi, hasa wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ambaye kwa muda mfupi ametuonesha kwamba ni kwa namna gani ambavyo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amepata msaidizi mzuri katika nafasi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri nimepata nafasi ya kukaa na Waziri Mkuu katika vikao kadhaa, ukimsikiliza anavyoongea, ukisikiliza maono yake, ukisikiliza *thinking* yake unasema kweli Tanzania sasa tuna Waziri Mkuu ambaye atakwenda kutuvusha katika hiki kipindi. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na viongozi wengine. Katika Jimbo letu la Ngara tunao wasaidizi ambao wanawasaidia Mawaziri, tunaye Mkuu wetu wa Wilaya Kanali Mathias Kahabi ambaye ametusaidia kuituliza Wilaya yetu ya Ngara, vilevile tunaye

Mkurugenzi wetu Solomon Kimilike ambaye naye amekuwa akisimamia vizuri fedha zinazoletwa na Mheshimiwa Rais kwa ajili ya miradi. Ninamwomba Waziri Mkuu kama Mkurugenzi wetu hawana mpango wa kumpandisha cheo basi watuachie palepale Ngara sisi watu wa Ngara tuna kazi naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimempongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, nimempongeza kwa sababu sisi katika Jimbo letu la Ngara wakati Mheshimiwa Rais Dkt. Samia anaingia madarakani kuna mambo mengi sana ambayo yamebadilika katika kipindi hiki cha miaka minne peke yake. Mathalani wakati anaingia kuanzia mwaka 2021 mpaka sasa hivi mwaka 2025, ameshatupatia zaidi ya shilingi bilioni 81.2 ambazo zimetekeleza miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya maji, ikiwemo miradi ya elimu, ikiwemo miradi ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwenye afya wakati Mheshimiwa Rais Dkt. Samia anaingia madarakani katika Jimbo la Ngara tulikuwa tuna hospitali moja tu ya Serikali ambayo ina hadhi ya Wilaya, lakini leo tunavyozungumza ndani ya kipindi chake cha muda mfupi, sasa hivi Wilaya ya Ngara ina hospitali mbili ambazo zina hadhi ya Wilaya, moja hospitali mpya ni ya Mbuba ambayo imejengwa kwa zaidi ya shilingi bilioni mbili tayari zimeshatumika kwa ajili ya ujenzi wa ile hospitali. Kwa hiyo, sasa hivi watu waliokuwa wanasafiri zaidi ya kilometa 200 kwenda katika Hospitali ya Nyamihanga kupata huduma za afya sasa hivi wanaenda kupata katika Hospitali ya Mbuba ambayo ipo pale karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la afya hakuishia hapo, wakati anaingia Dkt. Samia tulikuwa tuna vituo vya kutolea huduma za afya vilikuwa vipo 53, sasa hivi tunavyozungumza vituo vya kutolea huduma za afya viko 69, ambapo tuna hospitali tatu za Wilaya, tuna vituo vya afya vitano pamoja na zahanati 45. Hivi sasa uhakika wa kupata huduma za afya ni 85.6% kutoka kwenye 70.2% ya mwaka 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika elimu wakati Mheshimiwa Dkt. Samia anaingia madarakani, katika Jimbo la Ngara tulikuwa

tuna shule za msingi 120, sasa hivi tunavyozungumza 2026 ziko shule 127, shule za sekondari zilikuwa 25 sasa hivi ziko shule za sekondari 32. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la maji wakati Mheshimiwa Dkt. Samia anaingia madarakani, upatikanaji wa maji ulikuwa ni 52% na leo tunavyozungumza ni 74.6% ambapo zaidi ya shilingi bilioni 2.6 zimeletwa na Mheshimiwa Dkt. Samia katika kipindi chake cha miaka minne. Vijijini sasa hivi upatikanaji wa maji ni 72.8%, ambapo tumepokea zaidi ya shilingi bilioni 7.9 ndani ya kipindi cha miaka minne ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la nishati wakati Mheshimiwa Dkt. Samia anaingia madarakani tulikuwa na vitongoji ambavyo vilikuwa vina umeme ni 154 peke yake, lakini sasa hivi viko 191 vijiji vyote vina umeme na juzi tumepata vitongoji vingine 54 ambavyo vitakwenda kuongeza huduma hii ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mawili makubwa katika Jimbo letu la Ngara, Ngara tuna Mradi wa Kabanga *nickel*, sasa hivi unaitwa *Tembo Nickel*, tangu tukiwa wadogo tulikuwa tukiona shughuli mbalimbali zinafanyika katika ule mradi, lakini ule mradi ulikuwa haujaanza rasmi. Leo hii tunavyozungumza ndani ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan sasa hivi tuna uhakika kwamba ule mradi unakwenda kuanza na utakwenda kuingiza mabilioni kwa watu wa Ngara watakaokwenda kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika huu Mradi wa *Tembo Nickel* anaenda kuacha *legacy* katika Jimbo letu la Ngara kwa sababu ni mradi ambao ndani ya kipindi cha muda mrefu ulikuwa haujaanza, lakini sasa unakwenda kuanza rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ilani ya Uchaguzi 2025 - 2030 ya Chama Cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametuahidi kutujengea Barabara ya Nyakahura, Rulenge mpaka

Murugarama kwa kiwango cha lami. Hata juzi nimeuliza swali hapa Bungeni Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu kwamba mkandarasi amepatikana na fedha zimepatikana bado kwenda kumlipa malipo ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitu na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi yuko hapa, ni Kaka yangu mimi na amekuwa akinisaidia katika vitu vingi sana, hiki kitu Mheshimiwa Ulega kama watakwenda kujenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka Nyakahura kupita Rulenge mpaka Mulugarama watakuwa wamemsaidia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuacha *legacy* katika Jimbo la Ngara, pamoja na mambo mengi ambayo ameyafanya, lakini hili nalo ni miongoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezunguka nchi nzima hii mara tatu nikiangalia mambo mbalimbali ambayo yamefanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, haya nimezungumza katika Jimbo la Ngara, lakini yapo mengi ambayo yamefanyika katika ngazi ya Taifa. Katika eneo la maji kuna miradi mingi imefanyika, katika eneo la elimu kuna miradi mingi imefanyika, hayo nikueleze tu kwa uchache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamezungumza, kwa kumalizia tu katika eneo la Habari, mimi ni mwanahabari kwa taaluma na ndiyo ajira yangu ya mwisho, kabla ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuingia madarakani vyombo vya habari vilikuwa vina wakati mgumu sana. Kuna wakati walikuwa wakiitwa *TCRA* kwenda kwenye Kamati ya Maudhui, wakienda wanajua wanaenda kufungiwa, leo *TCRA* wanakuita, mnaenda mnakaa wanakuambia tumekufuatilia umefanya mazuri haya, umefanya mazuri haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tumemsikia Mheshimiwa Waziri Makonda amezungumza kwamba anakwenda kufanya mpango wa *Online Media* wapate mikopo ya vitendeakazi waende kujiendeleza. Nyuma kumiliki *Online Media* ilikuwa ni kama mhalifu, lakini leo tunazungumza kwenda kuwawezesha kwa ajili ya kupata vitendeakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dotto Jasson, tunaendelea na Mheshimiwa Bazilio Kapunda Mbwilo, Mheshimiwa Haran Nyakisa, Mheshimiwa Latifa Juwakali ajiandae.

**MHE. BAZILIO K. MBWILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, vilevile ningependa kukishukuru sana chama changu cha *ACT* Wazalendo kwa kuniruhusu niweze kuwa mgombea wa Ubunge Jimbo la Nkasi Kaskazini na hatimaye nikaibuka mshindi, nakishukuru sana chama changu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kutokana na muda, hotuba nzima ya Mheshimiwa Rais ni *road map* nzuri sana kwa Taifa letu, napenda kupongeza sana katika hilo. Sasa ili hiyo hotuba iweze kuwa ya manufaa nimeona ni jukumu langu kuongezea, kuonesha pale ambapo endapo watendaji wetu watayatekeleza basi hotuba hiyo itakidhi kama alivyosema mmoja ya wachangiaji kwamba *we have to walk the talk*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na eneo la kilimo, niipongeze sana Serikali kwa mpango wake mzuri wa ruzuku za pembejeo kwa wakulima. Huu mpango umekuwa mzuri sana na nataka niliambie Bunge lako kwamba, kwa mwaka huu Jimbo letu la Nkasi Kaskazini tunatarajia kuwa na *bumper harvest* hasa kwa mazao yanayolimwa zaidi kule ya mahindi. Niombe sana, mpango huu uendelee kipindi chote cha awamu hii utasaidia sana hata kuongeza akiba ya chakula kwenye hifadhi yetu ya Taifa. Ninashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niruhusu nipongeze benki zetu ambazo zimefanya kazi nzuri sana kuhakikisha kwamba wakulima wamepata pesa za mkopo kwa ajili ya pembejeo kwa wakati. Nizitaje benki mbili za *NMB* na *Coop Bank*, zimefanya kazi nzuri sana, wahusika ninaomba wapokee shukrani hizo za wakulima wa Nkasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uzuri huo, kuna changamoto imejitokeza ya mbolea feki, nimepewa taarifa kutoka Jimboni kwamba leo hii Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkoa wa Rukwa kimeitisha mkutano na *AMCOS* ambazo wakulima wake wamepewa *DAP* ambayo wenyewe wakulima wanasema kwamba ni feki. Sasa niombe mamlaka husika Mheshimiwa Waziri atumie vyombo vyake kucheki kama ni kweli suala hili na ikithibitishwa, niombe hatua za kisheria zichukuliwe mapema, kwani hawa watakuwa wanafifiza jitihada za Serikali katika kukuza kilimo hasa cha mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye eneo la afya, ninaishukuru sana Serikali, ninayo hospitali moja jimboni kwangu ya ngazi ya Wilaya, hiyo hospitali ni nzuri kwelikweli ninaomba nitoe pongezi, ni safi kweli na watumishi wako *attentive* masaa 24. Siyo hiyo tu, ninavyo vituo vitatu vya afya ndani ya Jimbo lenye kata 17. Kituo cha Nkomoro, Kituo cha Kirando pamoja na Kituo cha Kabwe ambacho hakijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kauli ya Mheshimiwa Rais kwamba anataka huduma ziwafuate watu, niombe sana kwa unyenyekevu Waziri awaonee huruma Kata zifuatazo: Kata ya Mkwamba ambayo ina zaidi ya kilometa 70 kufika Wilayani haina kabisa kituo cha afya, vilevile Kata tatu zilizofuatana za Paramawe, Mtenga pamoja na Mashete. Hizo Kata tatu hazina kituo cha afya, ningeomba, ninajua kwamba *resources* ziko *scarce,* lakini walau tungejenga kati ya hizo Kata tatu maana zimefuatana. Tukijenga Kata ya Mtenga, Kijiji cha Mwai walau ni katikati itahudumia Kata ya Mtenga, Kata ya Mashete pamoja na Kata ya Paramawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi, wakati Mheshimiwa Rais anasema atahakikisha lami inakuwepo kutoka Makao ya Wilaya hadi Makao ya Mkoa, tayari kwa Jimbo langu ipo, Wilaya yangu ya Nkasi ipo, lakini kuna barabara ambazo Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni alituahidi wananchi wa Nkasi, tunaomba sana sasa katika bajeti ya safari hii, barabara hizo ziingizwe nazo ni zile za kutoka Namanyere kwenda Kipili Bandarini na Kirando, Barabara ya pili ni kutoka Lyazumbi kwenda Kabwe. Maeneo

yote niliyoyataja yana bandari, ambapo endapo hizo barabara zitakuwa kwa kiwango cha lami, basi zitasaidia sana kuvutia mizigo inayoelekea Congo iweze kupitia maeneo hayo na kuongeza pato la nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa suala la utalii. Ninadhani kuna eneo ambalo kama tukiliangalia linaweza likatusaidia sana nalo ni Ziwa Tanganyika. Ninadhani Ziwa Tanganyika peke yake ni utalii tosha, kwa sifa yake ya kuwa na kina kirefu kuliko Maziwa mengi Barani Afrika hata na duniani kwa ujumla. Kitu pekee ambacho kimekosekana katika utalii wa Ziwa Tanganyika ni kutokuwa na meli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Nkasi wamenituma niiombe Serikali iturudishie Meli yetu ya Liemba, hiyo ni meli ya kihistoria. Wanaomba sana wasiipeleke kwenye chuma chakavu, meli ya Liemba irudi. Inayo historia kubwa sana meli ya *MV* Liemba, ukitafuta jina lake pamoja na Tanganyika, vina uhusiano mkubwa sana, kwa hiyo wahusika ninaomba sana meli yetu ya Liemba iweze kuelea tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa muda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bazilio. Tunaendelea na Mheshimwa Haran Nyakisa Sanga, Mheshimiwa Latifa khamis Juwakali na Mheshimiwa Pascal Lucas Lutandula ajiandae.

**MHE. HARAN N. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu leo nimesimama kwa mara ya kwanza, ninaomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujalia afya, ulinzi na hatimaye tuko hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi chama chetu, chini ya Halmashauri Kuu ya CCM na Kamati Kuu kwa kujenga imani na hakika kuweza kuteua jina langu kuwa mgombea wa Jimbo la

Kigamboni na leo niko Bungeni hapa ninawakilisha wananchi wa Kigamboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuwashukuru sana kwa dhati ya moyo wangu wananchi wa Kigamboni kwa kutoa kura za kishindo 94% kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na 93.5% kwa mimi mwakilishi wao ambaye leo niko hapa ninawakilisha shida zao, ninawashukuru sana wananchi wa Kigamboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa sehemu kuu mbili, sehemu ya kwanza nitajikita katika kuelezea mafanikio yaliyopatikana katika uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mwaka 2021- 2025, lakini pia nitachagiza kwenye hotuba iliyojaa maono na mwendelezo wa miradi mbalimbali ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani mwaka 2021 - 2025 Wilaya yetu ya Kigamboni ilifanikiwa kupokea jumla ya shilingi bilioni 368 katika kufanikisha miradi mbalimbali ambayo hapa nitaenda kuitaja. Halmashauri ya Wilaya ya Kigamboni kwa sekta ya viwanda, kabla ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan tulishakuwa na viwanda 20, lakini baada ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan mwaka 2021- 2025 tumefikisha viwanda 319 ikiwa viwanda vikubwa ni 32, viwanda vya Kati ni 14 na viwanda vidogovidogo 298, jamani haya ni maajabu ambayo yametokana na uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wananchi wa Kigamboni wanamshukuru sana kwa dhati ya moyo wao na ndiyo maana hata walionyesha imani katika uchaguzi uliyofanyika kwa kumpa kura za kishindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika idara hii ya afya vituo vya afya vilivyojengwa wakati wa uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan vilikuwa vituo 11 kutoka vituo 23 hadi vituo 32, likiwa ni ongezeko la vituo 11. Wilaya ya Kigamboni ina kata tisa, kwa hiyo ukisema vituo 11 ina maana kwamba kila kata imepata kituo cha afya. Hivyo, tunampongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, katika suala zima la elimu idadi ya shule za sekondari zilizojengwa wakati wa uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan zimefikia shule za sekondari 15 hadi sasa tunavyoongea. Idadi hii ni kubwa na itawasaidia sana wananchi wa Kigamboni, hasa katika kupata elimu na kuweza kujikimu katika shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme tu kuhusiana na nishati. Wilaya ya Kigamboni sisi wote tunaelewa kwamba ni wilaya ya kimkakati. Wilaya hii ya kimkakati inahitaji nishati bora na yenye nguvu, hasa katika kuhakikisha uendeshaji wa viwanda vilivyoimarishwa katika Wilaya ya Kigamboni kama nilivyotaja hapa vinafanya shughuli zao za uzalishaji bila mkwamo wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kipekee, katika uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan Kigamboni tumefanikiwa kupata Barabara ya lami kilomita 41.5 za kutoka Kibada, Mwasonga, Tundu – Songani *junction* mpaka Kimbiji. Hatua hii ni kubwa sana katika harakati za kuchochea maendeleo katika Jimbo letu la Kigamboni. Ninaomba nitoe nitoe pongezi sana shukrani za dhati ya moto kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan; aendelee, bado wananchi wa Kigamboni wana uhitaji mkubwa sana wa miundombinu ya barabara ili kuhakikisha wanachochea maendeleo ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zingine ninazitoa kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kulingana na maono yake. Wote ni mashahidi kwamba wakati anaingia kulikuwa na taasisi inaitwa *Tanzania Investment Centre,* kukawa na taasisi inaitwa *Economical Processing Zone Authority*. Sasa, huyu Rais, ili kujua kwamba ni mtu mwenye maono, ni mtu ambaye anaangalia mbali ameziunganisha hizi taasisi na kujenga taasisi moja bora ambayo inaweza sasa kusimamia mchango wa sekta binafsi katika kukuza pato letu la Taifa ambayo ipo katika dira yetu ya 2025 mpaka 50. Kwamba, inapofika 2050 lazima Serikali iwe inachangia bajeti kwa 30%, lakini sekta binafsi iweze kuchangia 70%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo tunapongeza sana kwa sababu ni maono makubwa ambayo yenye tija katika Taifa letu la Tanzania…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haran Nyakisa, ahsante sana.

**MHE. HARAN N. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niunge mkono hoja, lakini nilikuwa nina michango miwili ya muhimu kidogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, hutaendelea kwa sababu ya muda. Ahsante sana.

Tunaendelea Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mheshimiwa Pascal Lucas Lutandula na Mheshimiwa Haji Amour Haji wajiandae.

**MHE. LATIFA K. JUWAKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa miongoni mwa wachangia wa Hotuba hii ya Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niungane na wenzangu waliotangulia kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kibali hiki cha kutujalia kuwa wazima na uhai. Kwa dhati ya moyo wangu, ninaomba nirejee tena kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kunipendekeza kuwa miongoni mwa Wabunge wanaogombea katika kundi la vijana. Pia ninawashukuru sana vijana wa nchi hii kwa imani kubwa waliyonipatia na kunipa imani kunirejesha tena ndani ya Bunge hili kwa awamu hii ya pili; ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda ninaomba nijielekeze katika mchango wangu. Mimi binafsi ninapomwona Dkt. Samia Suluhu Hassan ndani ya moyo wangu ninauona utulivu na maono makubwa ya maslahi ya nchi hii. Kwa nini niyaseme

haya; kwa sababu bahati nzuri sana nilikuwepo katika Bunge lililopita, kila tulichokileta hapa sisi Wabunge wa Vijana na Waheshimiwa Wabunge wote ndani ya Bunge hii basi Mheshimiwa Rais alikuwa analichukua na kulichakata na kuleta *output* ndani ya Bunge hili. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niseme, kwamba vijana wa nchi hii wanahitaji mambo makuu matatu. Jambo la kwanza wanahitaji elimu na ujuzi, jambo la pili vijana wa nchi hii wanahitaji ajira na uwezeshwaji, jambo la tatu vijana wa nchi hii wanahitaji kusikilizwa kwa sauti zao, lakini pia kufanyiwa maboresho ya mambo mbalimbali katika mambo wanayoyahitaji na kushiriki na kushirikishwa katika shughuli zote zinazoleta maendeleo kwa ajili ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini nimeanza kwa kuyasema haya; nitaanza katika suala la elimu. Tulivyoingia katika kipindi cha 2020/2021, katika masuala ya elimu sisi Waheshimiwa Wabunge tulikuja hapa katika Bunge hili tukaiomba Serikali ikiwemo suala la bodi ya mikopo. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021, elimu ya juu walitengewa fedha si zaidi ya bilioni 400.6. Tukaja katika Bunge hili tukamwomba Mheshimiwa Rais, lakini sasa tunavyozungumza kiwango cha mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi wa Tanzania kimepanda hadi bilioni 900.1, tunamshukuru sana. Tumekuja katika Bunge lililopita tulimwomba Mheshimiwa Rais tufanyiwe mabadiliko ya Sera ya Elimu na kwa sababu tulikuwa tunaona mitaala yetu ya elimu haiendani na uboreshaji na matarajio ya vijana. Lile lilifanyika, hivyo tunamshukuru Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao ushauri mmoja kwa wenzetu wa Wizara ya Elimu. Nchi zote duniani kupitia vyuo vyetu hivi vya Tanzania, ninataka niwashauri na hawa wenzetu wa vyuo vikuu, tumebadilisha mitaala katika ngazi ya chini kabisa. Sasa, ili tuweze kufikia katika lengo lile ambalo tumekusudia ni lazima ita-*take so long*. Ninataka niwashauri wenzetu wa elimu ya juu wawe na mpango maalum. Huko wenzetu nchi za duniani kuna kitu wanaita *demand driving course*. Hizi *demand driving course* ni kozi ambazo zinatengwa kutokana na mahitaji ya kidunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyoelewa sasa hivi tunaweza tukaangalia; tunaona kwamba kuna masuala ya *cybercrime* na kuna masuala ya *artificial intelligence*. Kwa hiyo wenzetu wa vyuo vikuu lazima wawe *active* na macho yawe yanaangalia dunia, kwamba dunia inataka nini. Wakiona dunia kwa sasa inahitaji kitu gani na wao waweze kuandaa kozi ambazo zinaweza kuendana na mahitaji ya dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakwenda kwenye suala la ajira na uwezeshaji. Hapa Mheshimiwa Rais ametupa moyo, ametupa ari mpya vijana wa Tanzania. Ninataka nitumie nafasi hii kuwaomba sana kwa unyeyekevu mkubwa vijana wenzangu wa nchi hii; mama huyu anatupenda sana vijana wa nchi hii. Katika kutupenda kwake amedhihirisha katika Hotuba yake Mheshimiwa Rais alivyokuja kuzindua Bunge hii. Ninaomba nimnukuu, Mheshimiwa Rais alisema; "Kwa kuwa zaidi ya 60% ya watu wa nchi hii ni vijana tunaweka vipaumbele kwenye sera na programu zitakazopanua fursa za kiuchumi kutengeneza kazi na ajira, kuongeza wigo na hifadhi za jamii na kuwajengea kesho iliyo bora zaidi." Mheshimiwa Rais hakuishia hapo akaendelea kusema: "Ili kuhakikisha vijana wanapata nafasi ya kushiriki katika kujenga mustakabari mwema wa Taifa letu tutaweka kipaumbele kwenye ushirikishwaji." Ninaomba nirejee tena; "kwenye ushirikishwaji wa vijana katika masuala ya maendeleo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nilikuwa ninaomba nichukue nafasi hii kumwomba sana, *with due respect* Mheshimiwa Waziri wa Vijana, vijana wana matumaini makubwa sana na sisi wasaidizi wao tuna matumaini makubwa sana. Kwenye suala hili la uwezeshaji tunaomba tushiriki na tushirikishwe *from the scratch,* kuanzia chini. Hii itaweza kuonesha ule uhitaji na malengo ya vijana, lakini pia ili kuweza kuleta *output* kwa vijana na kuweza kufikia matarajio ya Mheshimiwa Rais ambayo anayatarajia kwa vijana wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda kama ikiwezekana unaweza kuniruhusu nimalizie la mwisho. Suala langu la mwisho nimesema ni ushirikishwaji wa vijana, hapo nimemaliza. Kwenye suala hili inaonyesha wazi kuteuliwa kwake Mheshimiwa

Waziri wa Vijana inaleta sura kwamba Mheshimiwa Rais anayo imani na kuleta mabadiliko kwa vijana. Kuteuliwa kwa wakuu wa wikoa wa nchi hii walio vijana, kuteuliwa kwa wakuu wa wilaya hii walio vijana, kuteuliwa kwa wakurugenzi wa nchi hii walio vijana, kila mmoja akisimama kwenye nafasi yake tutakuwa tunauimba wimbo mmoja wa kuleta mabadiliko chanya kwa ajili ya vijana wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais na sisi vijana asituchoke. Kama ni mama ni mlezi na kama mzazi akiwa mlezi vijana wakikosa anawapona kwa sababu ya kuwaletea maendeleo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Latifa kwa ujumbe mzuri kwa vijana, vijana ndiyo nguvu kazi ya Taifa letu. Tunaendelea na Mheshimiwa Pascal, Mheshimiwa Haji Amour Haji na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma wajiandae.

**MHE. PASCAL L. LUTANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nianze kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walionitangulia katika kuchangia hotuba nzuri ya Mheshimiwa Dkt. Samia. Awali ya yote mimi ni mara yangu ya kwanza kusimama katika hili Bunge lako Tukufu, hivyo, nianze kwa kumkumbuka babu yangu, mjomba wake mama yangu, Ndugu Ezekiel Madila aliyekuwa Mheshimiwa Mbunge kuanzia mwaka 1975 hadi mwaka 1977. Familia yetu na ukoo wetu imetuchukua takribani miaka 48, nimerejea mimi mtoto wa mamantilie, Pascal Lucas Lutandula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge wenzangu mnaonisikiliza; ukiingia humu ukachomoka, kurudi ni bahati. Kwa sababu ya muda niwashukuru viongozi wangu wa dini wakiongozwa na Pastor Luguli Askofu wetu wa Kanisa la Waadiventista Wasabato kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuniombea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana kwa upekee na kwa unyeyekevu mkubwa watu wa Jimbo la Chato Kusini, watu wema, watu waungwana, watu wanaompenda Mungu

waliokubali niwe sauti yao. Mungu wa Mbinguni awabariki sana Watu wa Chato Kusini. Ninataka niwaahidi, nilikwishawambia; nia yangu ni moja na nia yangu ni kuwatumikia; katika maisha yangu yote nitakuwa sauti yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mambo mengi ya kuchangia; nitachangia sehemu moja tu ya wachimbaji wadogowadogo. Mimi niliyesimama hapa ndiye mchimbaji mdogo kuliko wengine wote wanaozungumzia wachimbaji humu ndani. Mimi ndiye mchimbaji ninayeshika moko, mimi ndiye mchimbaji ninayeweza nikaingia duarani mita 60 mpaka 80 kwenda chini. Kwa hiyo, mimi ndiye sauti wa wachimbaji wa Tanzania, hata wasiponipigia makofi ipo siku watanipigia makofi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nianze kwa kusema, kwamba, sisi wachimbaji huwa tunapima uongozi na mafanikio ya kiongozi kwa namna tofauti na ninyi wengine. Sisi kiongozi akiteuliwa huwa tunasubiri kinatokea nini, jpya gani litatokea. Alipoteuliwa Mheshimiwa John Pombe Magufuli 2015 kwa sisi wachimbaji migodi mingi ilitokea dhahabu; na Mheshimiwa Rais Samia alikuwa ni Makamu. Tuliona kuwa huyu ndiyo Mheshimiwa Rais anayetupeleka sisi wachimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan yametokea maajabu hamjawahi kuyaona. Alipoteuliwa tu awamu yake hii ya pili Mgodi wa Msasa, mgodi mkubwa kule Bukombe unatoa dhahabu haijawahi kuonekana. Ninavyozungumza hivi wauza magari kule Dar es Salaam wamemaliza magari yote, yananunuliwa na wachimbaji. Ninataka niwaambie ukweli Watanzania waelewa; na nikuombe dakika zangu 10 zibaki palepale kwa sababu ninazungumzia sekta kubwa ambayo mimi ndiyo mwakilishi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mama Dkt. Samia ametupa heshima wachimbaji. Kipindi ninaanza kuchimba ulikuwa huwezi ukapeleka hata posa ukakubaliwa kwenye familia za wafugaji; leo wachimbaji tunakwenda kuchimba na *V8*, jamani Mama Samia! Ni nani kama Mama Samia? Unakwenda kuchimba na

moko umeiweka kwenye *V8*, unaulizwa huyo ni Mheshimiwa Waziri au ni Mheshimiwa Mbunge? Kumbe ni mchimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nikwambie, alipoingia madarakani Mheshimiwa Dkt. Samia Tanzania nzima tulikuwa na leseni za wachimbaji wa moko 903; tunavyozungumza leo Mheshimiwa Dkt. Samia tunamiliki leseni 9,774. Hata kama Waheshimiwa Marais waliopita ukawagawia leseni 1000, 1000 bado zinabaki. Ni nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nikwambie, Mheshimiwa Rais kipindi anahutubia hili Bunge alisema, ninanukuu: "*Wachimbaji wadogo wataendelea kuwa nguzo ya kutegemewa.*" Ninataka nimwambie kama kama alitutambua sisi tutabaki kumtambua kama nguzo na mchimbaji namba moja Tanzania; na hii ninataka nitoe ilani, wameniambia wachimbaji, walinituma, wakasema na wewe tumekutuma ukifika huko tena utusahau. Ninataka nimwambie Mheshimiwa Waziri Mkuu nitamsumbua asubuhi na mchana. Ninamwamini kwa sababu wachimbaji wanataka kuendelea kuchimba wala siyo kupiga maneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto, ni ndogo sana, ambazo nitampelekea Mheshimiwa Waziri Mkuu mezani kwake, wala sipigi kelele. Sisi wachimbaji tunataka kuchimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwaambie ukweli, wakati Mheshimiwa Dkt. Samia anaingia madarakani viwanda vidogo vidogo vya wachimbaji katika nchi hii tulikuwa navyo 1,015. Leo tu kwa muda mfupi wa miaka minne ameongeza viwanda vingine 542. Tumeajiri zaidi ya vijana hawa, wanaosemwa vijana hawana ajira, zaidi ya 1,000, vijana 62,000 wameajiriwa. Ninataka niwaambie vijana wenzangu Tanzania, kwamba sisi kwenye upande wa dhahabu kumekucha. Tunavyozungumza leo Mheshimiwa Dkt. Samia anaingia madarakani dhahabu ilikuwa inanunuliwa Tanzania kwa *gram* moja shilingi 240,000, tunavyozungumza leo dhahabu *gram* moja ni mara mbili yake; inayonunuliwa leo, Mheshimiwa Waziri wa Madini ni shahidi, 450,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wachimbaji, vijana wa Tanzania na watani zangu wagogo acheni *propaganda* twendeni tukachimbe. *(Makofi)*

**MHE. MUSA G. MBUGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa inatoka wapi?

**TAARIFA**

**MHE. MUSA G. MBUGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimpe taarifa anaeongea kwamba dhahabu sasa hivi inanunuliwa kwa zaidi ya shilingi 400,000. Amesema 450,000? Inanunuliwa kwa shilingi 500,000 sasa hivi.

**MHE. PASCAL L. LUTANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea, lakini sio mchimbaji huyo ananipotezea muda. Dhahabu kwa soko la leo inanunuliwa kwa shilingi 450,000 kwa gramu moja. Leo ukiwa na kilogramu 10 za dhahabu tayari una shilingi 4,500,000,000. *(Hapa Mheshimiwa aliongea Kisukuma) (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nitoe maombi yangu. Kwanza kwa unyenyekevu mkubwa ninataka nimwambie Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Daktari mama yangu Samia tunampenda. Sisi wachimbaji tutaendelea kumlinda na bado tutamuombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayupo Rais mwingine mwenye moyo wa upendo wa kuwajali wachimbaji kama Mheshimiwa Dkt. Samia. Ninataka nimuahidi na sisi wachimbaji tumuahidi, Biblia inasema katika Wafalme, "Mfalme Ezekia alimlilia Mungu na Mungu akabadilisha aliyokuwa akiyawaza". Sisi wachimbaji tutamlilia Mungu mpaka Mungu akubali Tanzania Mama aivushe kufika Kanaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa sababu ya muda nitoe sasa mapendekezo yangu niliyotumwa matatu na wachimbaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji wamenituma mambo matatu tu mafupi ambayo nimpelekee moja kwa moja Waziri Mkuu na Waziri wa Madini. Moja wamenituma ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ninaomba nikupe dakika mbili tu umalizie kwa sababu muda wako ulishaisha.

**MHE. PASCAL L. LUTANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza wamenituma Waziri Mkuu ninaomba anisikilize vizuri namwaamini kabisa Waziri Mkuu kaka yangu nampenda mno; wameniambia wanaomba wakutane naye. Kuna jambo la wawekezaji limekuja Tanzania na linaitwa *Technical Support* linaweza kutuporomosha. Ninaomba akutane na sisi, azungumze na sisi, awasikilize wachimbaji. Muda wowote wako tayari wachimbaji hawana maneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine wanalotaka waje wazungumze na wao, hizi leseni wanazozifuta katika mgawanyiko wake wa kuzigawa, sekta hii wachimbaji wengi wameipenda. Vijana wameongezeka na wamekubali sasa kufanya kazi ya uchimbaji; mgawanyo wao ukoje? Wanataka sasa waweke mipango kama leseni zinaporudishwa kutolewa kwa wawekezaji wakubwa, hawa wachimbaji wadogo wadogo waaanze kupata wao, wapewe kipaumbele kwenye nchi hii kwa sababu mama amewatambua, ninaomba sasa wapewe kipaumbele. Hayo maombi yangu mawili matatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni kwa wapigakura wangu wa Chato Kusini hawa sitowasahau. Nao wamenituma ukikutana na Waziri Mkuu mwambie kuwa ombi lao ni moja, wanataka wakachimbe walipofanya utafiti pale Kanyindo. Waendelee kuchimba na hawana maneno mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo niseme tutaendelea kumwombea Mheshimiwa Dkt. Samia. Sisi tuko pamoja naye akisema kesho tuje kuchangia maendeleo ya nchi

hii hela tunazo tutachangia, tuko tayari wachimbaji mama ametupa pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nimeunga hoja na Mungu wa Mbinguni awabariki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pascal Lucas Lutandula, ahsante sana na ninaamini wachimbaji madini Tanzania nzima wamekuelewa kabisa.

Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge itabidi niongeze muda hadi tumalize wachangiaji wanne waliobaki. Tunaendelea na Mheshimiwa Haji Amour Haji, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma, Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe na Mheshimiwa Haidary Hemed Sumry atakuwa wa mwisho.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nikupongeze wewe kwa kuchaguliwa tena kuwa Mwenyekiti katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pili, nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anavyofanya kazi zake na kutuwajibishia sisi wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Pangawe kwa kuweza kunichagua tena kuja kuwatumikia katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani kwamba katika hotuba yetu hii ambayo iliyoletwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo tunayoijadili hivi leo. Hotuba yetu hii imekuja na mambo mawili ambayo ni makuu katika kitabu hiki ambacho cha hotuba na kila mmoja ambaye anayesimama utakutia anaingia katika hizo alama mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha mwanzo, ni kumzungumza Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba ana uthubutu kwa sababu kitu cha mwanzo ni lazima kwamba tukubali Rais wetu

mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika moja ambalo kitu alichokuwa nacho ni uthubutu. Uthubutu huu aliuanza mara tu baada ya kuapishwa na kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pale aliposema "Kazi Iendelee" na kwa kweli Mheshimiwa Rais alionesha kweli uthubutu wake kwa ile miradi ambayo imeachwa na mtangulizi wake niseme tu kwamba miradi ile kama ni mtu ambae ni mwepesi kwa wakati ule maana yake tungekuwa sasa hivi tunazungumza jambo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe kama ni shuhuda wakati ambapo mtangulizi wake anafariki kipindi kile tulielekea safari ya kwenda Mwanza tukapita kwenye Daraja lile la Busisi pale. Daraja lile tumepita pale ikiwa kama tunapita kwenye mabati, tumepita juu ya mabati ninaweza kusema kwamba ilikuwa ni watu wa mwanzo wa basi la Wabunge kupita katika Daraja la Kigongo - Busisi likiwa lile daraja ndio kwanza linaanza na bahati mbaya sana siku ya pili yake tuko Mwanza pale mtangulizi wake yule akafariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukawa tunajiuliza; je, miradi ile itaweza kuendelea kama ilivyo? Bahati nzuri baada ya miaka miwili tena tukaja tukapita tena Kigongo - Busisi daraja lile likawa tayari linaendelea mpaka mwaka jana maana yake Daraja lile limemalizika. Siyo tu kwa Kigongo – Busisi, ni miradi mingi ambayo ameishikilia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan miradi ile yote kwa kiasi kikubwa tutasema kwamba imemalizika au iko karibu sana kumalizika. Sasa niseme tu kwamba Dkt. Samia Suluhu Hassan ana uthubutu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kisha kitu cha pili niweze kumzungumza Dkt. Samia Suluhu Hassan kutokana na hotuba hii kwamba Dkt. Samia Suluhu Hassan ana dhamira ya kweli. Nikizungumzia suala la dhamira maana yake kwa namna ambavyo alivyoileta hotuba hii na hotuba hii kaileta kwa kuakisi tena jina lingine la kusema kwamba Kazi na Utu. Tukizungumzia suala la kazi na utu maana yake kwamba kwa namna zile taasisi ambavyo zilivyoelekezwa na namna ambavyo zilivyokuwa na maelekezo yake na zilivyokuwa na maono ambayo ameyaonesha maana yake ni kweli kwamba Mheshimiwa Dkt.

Samia Suluhu Hassan lile neno la Kazi na Utu linaakisi juhudi zake na maono yake kupitia kwa kila sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tukija katika Sekta ya Afya maana yake kaleta maelekezo mengi pale na maono yake na ile kuangalia suala la utu kusema kwamba kwa sasa hivi maana yake tujaribu kuangalia, si dawa lakini ni bora ya tiba kuliko kinga. Maana yake ni bora tutibu kwanza, ni kitu cha muhimu zaidi, lakini ni bora kinga kuliko tiba. Maana yake tukinge kwanza ndiyo kisha baadaye tufuatilie tiba ambayo ninasema kwamba ni maono ambayo kayazungumza kwenye kitabu chake hiki ambacho kipo kama hotuba ambayo aliyoieleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika masuala ya elimu, kuna maono mengi sana kuhusiana na elimu za vijana hasa kwenye masomo ya amali. Nitasema kwamba kwa upande wa masomo ya amali, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa upande wa vijana kwa maono yake kayazungumza kwenye hotuba, lakini kuna vitendo ambavyo tayari vimeshaanza kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni vijana karibu 1,500 sasa hivi wanapelekwa kwenye mafunzo ya amali na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itagharamia bure. Nimemsikia Mheshimiwa Naibu Waziri akitangaza juu ya suala hilo na hiyo kwamba ni dhamira yake. Ninasema kwamba ni dhamira kwamba kuhakikisha kwamba vijana wa Tanzania wanapata elimu ya amali na vilevile kupata ule ujuzi utakaoweza kuwasaidia aidha kwa kujiajiri au kwa kuweza kuajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo niweze kumpongeza pia Waziri wa Vijana ambaye naye kwa jitihada kubwa sana ambayo anaifanya kupitia vijana wake kwa namna ambavyo alivyokuwa kaichukua ile Wizara na kajikubalisha hasa kutokana na ule uono wake. Nilikuwa ninamwangalia wakati huo kabla hajawa Waziri alikuwa ni mtu wa karibu sana kuwaasa vijana na zile mada zake nilikuwa nazipitia mara kwa mara ninaweza kusema kwamba Dkt. Samia Suluhu Hassan Waziri huyu nadhani kwamba kam-*target* hasa na kwamba anafanya kazi vizuri.

Niseme tu kwamba anafanya kazi kwa namna ambavyo inatakiwa kwamba kapewa Wizara yake na Wizara hiyo imepewa washauri juu ya vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kitabu chetu hiki nije kwenye suala la amani. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alitupa nasaha katika kitabu chetu hiki tukiangalia kwamba kuna mambo matatu. Jambo la kwanza kuna nasaha, jambo la pili katika kitabu chetu hiki kuna maelekezo au mwelekeo na lingine kuna ahadi ambazo ameahidi katika kitabu chetu hiki cha hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija suala la nasaha. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kama ni mama maana yake ametuasa. Ninasema kwamba kawaasa vijana pale aliposema kwamba katika kukaa kwetu tusije tukakata tawi la mti ambao tumeukalia. Kwa wazee zamani niseme kwamba tusije tukafanya kazi ya uabunuwasi. Uabunuwasi ni kufanya kitu cha kinyume chake. Kufanya kitu kinyume chake maana yake kule ambacho kitu kinyume chake ndicho unachokifanya wewe mwisho wake inakuwa ni athari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze tu katika katika kutuasa kwetu huku maana yake nizungumzie suala la amani kwamba bila ya yote hayo na haya tunayoyazungumza yote haya bila ya amani maana yake hakuna chochote ambacho kitakachoweza kufanikiwa. Tukubali tu amani ndio kila kitu na amani ndiyo msingi wa maendeleo ya Taifa letu na amani ndio uhai wa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndugu zangu viongozi wangu ningeshauri kwamba kwa kila mmoja ambaye anayekwenda kwenye jimbo anayewatumikia wananchi suala la amani liwe ni kitu ambacho cha msingi kuliko masuala yote. Wanapozungumza, wanapokaa, maana yake bila ya amani maana yake hatuwezi tukafikia haya yote ambayo tunayoyazungumza. Bila amani hakuna maendeleo na bila amani hakuna uhai. Kwa hiyo, neno hili nalo kama viongozi maana yake

ningeshauri maana yake kwamba tuliwekee mkazo katika shughuli zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, baada ya kuangalia hii hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo alivyotoa maelekezo na namna ambavyo ilivyo, niseme kwamba kwa kila Wizara au kwa kila taasisi ambayo imeguswa juu ya hotuba hii maana yake ni vizuri zaidi tukawa na mpango mkakati maalum. Ikiwa ni afya maana yake tukawa na mpango maalum kwa upande wa afya unaotokana na hotuba hii, kama ni elimu tukawa na mpango maalum unaozungumza juu ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumza haya kwa sababu gani? Lengo maana yake tuone matokeo ya haya ambayo yaliyosemwa na Mheshimiwa Rais na mwisho wa siku nchi yetu hii kwa namna ya maono yetu tufikie katika lile lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwenye Kamati zetu pamoja na kwamba tunalizungumza suala hili kama ni hotuba kwenye Bunge la Jamhuri, lakini pia kila wakati kwenye zile Kamati zetu kwa taasisi zilizoguswa tuwe na maono ya kuiangalia hii hotuba kwa kila sekta. Kama ni elimu; je, imeguswa kwa upande gani juu ya ile hotuba ambayo ilikuwepo. Kama ni afya, utalii, au miundombinu ili mwisho wa siku tutakuja kujikutia kama tutakwenda kwa namna ambavyo ilivyozungumza hiyo hotuba hivyo nchi yetu itakuja kuwa ni nchi ya asali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nishukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi hii na niwapongeze Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao. Hii inaonyesha dhahiri katika Bunge ambalo limesheheni wataalam, ni Bunge la Kumi na Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo nizungumze dhahiri na ninazungumza hivi kwa sababu kila anayechangia utahisi hasa huyu katoka kwenye kundi fulani. Kama ni vijana maana yake anazungumza hasa, kama ni mwalimu unajua yule ni mtu wa vijana, kama ni mtu wa *NGO* ambaye nilikuwa namsikiliza dada

yangu Mheshimiwa Jamila pale unajua kwamba yule ni mtaalam wa *NGO,* kama ni mwalimu unajua kwamba ni mwalimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niwapongeze Waheshimiwa Wabunge kwa namna ambavyo tunachangia Hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. Ninaomba sana tuendelee kuwa na umoja, tuendelee kulisaidia taifa letu; umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haji Amour ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma, ajiandae Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja ambayo iko mezani ambayo ni Hotuba ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akifungua au kuzindua Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba ya Rais ni maelekezo, si ushauri ni maelekezo ambayo tunabidi tuitekeleze ili kulisogeza Taifa letu kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisoma hii hotuba nikairudia. Ina mambo mengi ambayo tukiyatekeleza tutawatumikia wananchi na ninatumaini kauli ya Mheshimiwa Rais kwamba ifikapo 2030, nchi iwe inatabasamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwapongeza Wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini kwa kura zao nyingi walizonipa mimi kama mbunge wao, lakini walizompatia Mheshimiwa Rais. Wanayo ari ya kufanya kazi kumuunga mkono na kama kauli mbiu ilivyo kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Muleba kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kazi kubwa imefanyika. Mambo ambayo yalishindikana kipindi cha nyuma yamefanyika kwa kipindi cha miaka mitano. Nimwombe Waziri wa TAMISEMI,

tunajenga hospitali kubwa pale Muleba zaidi ya shilingi bilioni tatu zimeletwa pale. Ninamwomba aje atutembelee aangalie kazi inayoendelea pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miundombinu ninaishukuru Serikali yetu. Ninamwomba Waziri wa Ujenzi ndugu yangu Mheshimiwa Ulega aje akatutembelee aangalie daraja la mfano linalojengwa pale Muleba na sisi watu Muleba tunaita Busisi ndogo. Kazi kubwa imefanyika pale Mto Ngono (sasa msicheke ninapoongelea Mto Ngono), ni Daraja la Kamishango lakini kwetu unaposema Mto Ngono wengine wanafikiria mambo mengine, lakini kazi kubwa imefanyika pale. Ninamwomba Waziri wa Ujenzi aje akazindue lile daraja muda ukitimia tukaongee maneno na kushukuru kazi iliyofanywa kwa kipindi cha miaka mitano kwani ni daraja la mfano na ni daraja la kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa kuwa Mkoa wa Kagera Chuo Kikuu - Kampasi ya Kagera inajengwa pale Kagera ambayo ni ya kwanza. Nimshukuru Rais wetu, elimu imerejeshwa nyumbani. Wakati tunaweka jiwe la msingi pale Mzee Wetu Rais Mstaafu Kikwete alisema Wahaya pamoja na kuitwa *Nshomile* lakini hamkuwa na Chuo Kikuu, kakileta Mama Samia; ninaomba tumpe maua yake. Tulikipigania kwa muda mrefu. Nishukuru na niiombe Wizara ya Elimu ikaharakishe kukamilisha ujenzi wa chuo chicho ili elimu tukairejeshe nyumbani ilikotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Vyuo Vikuu unaoendelea ni kazi nzuri, lakini ninaomba nitoe ushauri. Ujenzi wa vyuo vikuu kazi nzuri tunajenga miundombinu lakini tuangalie na *aspect* ya kuongeza idadi ya maprofesa ambao wanakwenda kufundisha kwenye hivyo vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mwakilishi wa Wasomi wa Vyuo Vikuu; kazi tuliyonayo kwa sasa tunao upungufu mkubwa wa maprofesa. Kuna sehemu nadhani tulijisahau tukaliacha, lakini sasa ni muda muafaka wa kuongeza idadi ya maprofesa ili vyuo tunavyovijenga vikapate watendakazi ambao ni mahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niwashukuru Mawaziri ambao baada ya kuteuliwa mmekuja Muleba. Ninaanza kumshukuru ndugu yangu, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Bashiru ambaye amepewa dhamana ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Niiombe Serikali na niishauri, Mheshimiwa Waziri aliona yaliyoendelea kwenye Ziwa letu la Victoria. Tunazo changamoto kubwa kwa wavuvi na uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sasa kwa kuwa amepewa hili jukumu tuhakikishe tunaokoa Ziwa letu la Victoria tuondokane na uvuvi haramu katika Ziwa Victoria ili uweze kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi vinginevyo tutabaki na Ziwa halina samaki lakini tuna maji yasiyo na samaki, hiyo haitufai. Tunataka Ziwa Victoria likaongeze chachu ya maendeleo kwa watu wanaozunguka hilo Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali waharakishe kutengeneza Mamlaka ya Udhibiti wa maziwa yetu, tuondokane na dhana ya Serikali kufanya kazi kupitia vyombo mbalimbali ambavyo ni vingi ambavyo havina *coordination* tuwe na chombo kimoja cha kudhibiti uvuvi haramu Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji, namwona ndugu yangu Waziri Aweso. Mheshimiwa Rais akiwa Muleba wakati wa kampeni alituahidi nasikia watu Bunge wanaongelea 70%, sijui asilimia tisini na ngani wanapata maji ya salama na hakika. Ninashukuru Serikali tumejenga miradi mingi sana lakini pale kwangu Muleba kutokana na jiografia na mabadiliko ya tabianchi tumechimba visima inapokuja kipindi cha kiangazi tunapata shida Mheshimiwa Aweso, Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mkubwa wa kukomboa watu wa Muleba kutokana na adha ya maji Mheshimiwa Rais alisema natumaini na Waziri wa Maji upo hapo utatekeleza na Waziri Mkuu yupo hapa, alituahidi mradi mkubwa wa kutoa maji Ziwa Victoria. Tumezungukwa na maji, lakini hatuna maji na wewe Mheshimiwa Waziri wa Maji upo tunamwomba atembee Muleba atusaidie kutatua hili tatizo la maji watu wa Muleba tupate maji kutoka Ziwa

Victoria ndiyo Suluhu pekee ya Wilaya ya Muleba kupata maji kata zote 43.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa imefanyika miradi mingine inaendelea kujengwa, lakini tunaomba tupate maji kutoka Ziwa Victoria tukamalize tatizo la watu wa Muleba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa Mkoa wa Kagera kwenye hotuba ya Rais ukurasa wa 33 ameongelea ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kyabajwa. Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kyabajwa ambao utasaidia kuchochea mazao yetu ya Mkoa wa Kagera. Ukienda nchi jirani pale kwa babu yetu wanasafirisha ndizi kutoka nchi Jirani wanazipeleka *London* lakini zetu zilikuwa zinashindwa kufika kwenye masoko ya kimataifa kwa sababu hatukuwa na uwanja wa kimataifa, uwanja wenye hadhi ya kutua ndege kubwa na kubeba ndizi zetu, kubeba maparachichi kuyapeleka soko la kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe wizara husika ambayo inajenga Kiwanja cha Ndege cha Kyabajwa sasa, kwa kuwa Rais ametamka, sasa tukachangamke tukaukomboe Mkoa wa Kagera tukaongeze kipato cha wananchi. Hii ndiyo dhana halisi tunaposema uchumi jumuishi, uchumi ambao unahusisha watu wengi, kama ni wavuvi wakavue, kama ni wakulima wakachangamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la kahawa limechangamka Kagera tuombe Wizara ya Kilimo, wapeleke miche bora kwa wakulima ili wapande, tuvune tukashindane na nchi Jirani. Babu asiwe anatuzidi mauzo kwenye zao la kahawa na Wilaya ya Muleba inaongoza uzalishaji wa kahawa Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, nikutakie kazi njema, niitakie Serikali yetu kila la kheri tunapoanza muhula mpya wa miaka mitano. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Dkt. Oscar Ishengoma. Tunamalizia na Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe na Mheshimiwa Haidary Hemed Sumry ajiandae.

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nitumie nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi. La pili, nitumie nafasi hii kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama kwenye Bunge lako Tukufu kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa tarehe 14 Novemba, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nami nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, haikuwa kazi rahisi katika miaka yangu yote ambayo nimekuwa nikifanya siasa kufikia hatua hii ya kuingia kwenye Bunge hili Tukufu katika nchi yetu. Pia nitumie nafasi hii kukishukuru sana chama changu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kunipa fursa ya kuwa mgombea na hatimaye kuwa Mbunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nitumie nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wenzangu wa Chato Kaskazini ambao kwa heshima kubwa walinipigia kura za kutosha nikiongozwa na Mheshimiwa Rais aliyepata kura 98% katika uchaguzi, Jimbo letu la Chato Kaskazini nami nikapata 97%, ninawashukuru sana wananchi wa Chato kwa kunipigia kura hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii ambayo sasa iko mbele yetu tunaijadili karibu Wabunge wote tumesimama kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais aliyoyafanya kwa Watanzania wakiwemo Watanzania wa Chato Kaskazini tunapaswa tumpe nguvu na *support* kubwa ya kuendelea kulitumikia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii nimesoma kuanzia ukurasa wa kwanza mpaka ukurasa wa mwisho nikaona Mheshimiwa Rais amezungumza katika maeneo makubwa 11, lakini katika maeneo haya 11 nami nitajikita katika maeneo makubwa mawili. Eneo la kwanza ni la kuonyesha kwa nini

wananchi wa Chato Kaskazini walitoa kura za kishindo kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza, sisi watu wa Chato ilipofika wakati wa kupiga kura wananchi wengi walijitokeza kumpigia Rais kwa kazi njema na nzuri aliyoifanya kwa wananchi wa Chato. Ukiangalia iko miradi mikubwa ya kimkakati ambayo ilianzishwa kule Chato, lakini katika miaka minne ya utawala wa Mheshimiwa Rais mambo yaliyofanywa ni mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza katika Wilaya yetu ya Chato kulianzishwa ujenzi mkubwa wa hospitali ya kanda ambayo hospitali ile wakati anachukua madaraka Mheshimiwa Rais Dkt. Samia ilikuwa imefikia 40%, lakini mpaka sasa tunavyozungumza tunakwenda kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka uliopita 2025, hospitali ile ilikuwa imekamilika kwa 100% na tayari ilikuwa inafanya kazi. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa wananchi wa Chato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anachukua nchi hii Chato kama Chato tulikuwa na vituo vya afya vinne, lakini katika miaka minne ya utawala wake Chato iliongezeka tukawa na vituo vya afya 11 ambayo ni sawa na ongezeko la vituo saba vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mweyekiti, haikuishia hapo tu zahanati tulizokuwa nazo kwa kipindi kile tulikuwa na zahanati 26 kwa wilaya nzima katika kata 23, lakini Mheshimiwa Rais katika miaka yake minne zahanati zilitoka kuwa 26 mpaka 33 ambapo ziliongezeka zahanati zaidi wakati wa utawala wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka ukienda kwenye elimu hapa ndipo alipofanya maajabu yake hapa. Kwanza vyumba vya madarasa tu vilivyojengwa katika kipindi cha miaka minne vilikuwa ni vyumba vya madarasa 340 kwa watoto wetu, lakini pia matundu ya vyoo yalijengwa zaidi ya matundi 897, nyumba za walimu katika shule za msingi zilijengwa 11, lakini kwa sekondari zilijengwa nyumba za walimu zaidi ya 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa machache tu yale ambayo ameyafanya Mheshimiwa Rais kwa kipindi cha miaka minne palikuwa na sababu kubwa ya kupiga kura na kupata 98% katika uchaguzi uliopita 2025. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa ninapitia kitabu hiki cha hotuba nilipofika ukurasa wa 12 nikakutana na kitu ambacho Mheshimiwa Rais ile falsafa yake aliyokuja nayo ya *R4*. Katika falsafa ile ukiisoma moja baada ya nyingine zile *R4* utagundua kwamba Mheshimiwa Rais alichokuwa anatamani kukifanya hapa ni kuleta usawa wa wananchi wake katika Taifa hili. Cha kwanza usawa ambao ninaweza nikauzungumzia wa kwanza ambao nimeuona ameondoa matabaka kati ya Kundi moja na Kundi jingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma tumepitia katika tawala mbalimbali, kulikuwa na matabaka ambayo yanaonekana ya wazi kwamba ukizaliwa kijijini na mwingine akazaliwa mjini ni lazima kuwe na utofauti mkubwa. Leo Mheshimiwa Dkt. Samia alipochukua nchi yetu ameleta msawazisho mkubwa sana katika Tanzania yetu hii. hapa kila Mbunge aliyekuwa anasimama hapo nikiwemo nami tunazungumzia suala la madarasa aliyoyaweka kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda madarasa yaliyowekwa vijijini mtoto wa kijijini anayeingia darasani anasoma kwenye chumba kilicho sawa sawa na chuba ambacho kimejengwa katika miji mingine katika nchi yetu. Kwa hiyo, utaona mama huyu amekuja na upendo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata kwenye jamii yetu, leo katika Bunge lako hili tukija kuangalia karibu 50% kwa 50 ni vijana kwa wazee. Kwa hiyo, wote wale vijana wameletwa katika Bunge hili lakini wamewekwa katika nafasi mbalimbali za kimamlaka za kutumikia Taifa hili. Nitumie nafasi hii kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuendelea kuwatumikia Watanzania kwa namna ambayo anaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niende kuangalia katika uundaji wa Serikali ambayo ameiunda Mheshimiwa Rais, ukiangalia katika Baraza letu la Mawaziri kwa kweli Mawaziri walioteuliwa katika kipindi hiki wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kweli Mheshimiwa Dkt. Samia amefanya kazi iliyotukuka kwa sababu ni Mawaziri wanaofanya kazi vizuri tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema pamoja na Wanachato kutengenezewa haya mambo ambayo nimeyasema bado Wanachato wana imani kubwa kwamba Mheshimiwa Rais sasa kwa sababu anataka kuona Watanzania kwa kila maeneo wanaishi vizuri. Niombe Wizara ya Uchukuzi sisi tuna uwanja wetu wa ndege pale Chato, uwanja ule umekuwepo siku nyingi na ndege zilikuwa zinatua pale na ulikuwa unafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tukiangalia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais tumeona ametuongezea ndege nyingine amenunua. Leo Tanzania tunazungumza zaidi ya ndege 16 tunazo, hapo mwanzo yawezekana ndege zilikuwa zimepungua za kutua katika uwanja wetu wa Chato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki nimwombe sana Mheshimiwa Waziri katika sekta hii ahakikishe angalau uwanja wetu utumike hata ndege zije pale mara mbili kwa wiki angalau itakuwa imesaidia wananchi wa Chato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe pia Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, tunayo Barabara kubwa ya kutoka Nyamirembe kupitia Ichwankima kwenda Kasenga mpaka Biharamulo. Barabara ile ni barabara ya kimkakati ambayo inaweza ikawafanya wananchi wa ukanda ule wakajipatia maendeleo vizuri kwa sababu inaunganisha na nchi iirani ikiwemo Nchi za Kongo, Burundi, Rwanda pamoja na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hivyo Mheshimiwa Rais katika kipindi chake cha miaka minne ameweza kujenga Bandari kubwa pale Nyamirembe alipeleka zaidi ya bilioni sita ambazo zimewekwa pale na ile bandari imeshakamilika kwa muda wa

miaka mitatu sasa, lakini haifanyi kazi na kufanya kazi kwake kunategemea ujenzi wa ile barabara ili Nchi jirani kutoka *DRC* Kongo, Burundi pamoja na Rwanda waweze kuja kuchukua mizigo kwenye Bandari ya Nyamirembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana Wizara ya Ujenzi pamoja na uchukuzi itakapofika wakati wa utekelezaji niwaombe sana katika Bunge hili wakati tunaendelea na Bunge hili basi Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi twende nao tufike Nyamirembe tuione ile Barabara, lakini tukaione na ile bandari iweze kuingia katika utaratibu wa kuweza kuendelea kufanya kazi ili iweze kuleta maendeleo katika eneo la Wilaya ya Chato. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umepita zaidi ya ule, mara mbili.

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nami nikushukuru sana kwa nafasi, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe. Tunamalizia na Mheshimiwa Haidary Hemed Sumry.

**MHE. HAIDARY H. SUMRY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kama Wabunge wengine waliotangulia kusema niendelee kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai, lakini kwa kuniwezesha kuingia katika Bunge hili ambacho ni chombo muhimu cha kutunga sheria na cha kupeleka maendeleo kwa wananchi kwenye nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo kwa Mwenyezi Mungu nikishukuru chama changu Chama Cha Mapinduzi (CCM) na vikao vyake vyote kwa kuniteua na kwenda kupeperusha bendera kwenye Jimbo la Mpanda Mjini kuwakilisha wananchi wa Jimbo la Mpanda Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani nyingine ziende kwa viongozi wa chama changu ngazi ya mkoa, lakini viongozi wa chama ngazi ya wilaya tumepambana nao usiku na mchana kuhakikisha tunapata ushindi wa kishindo kwa Rais wetu mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini kwa mimi Mbunge wa Jimbo la Mpanda Mjini na kwa Madiwani wote ambao wametokana na Chama Cha Mapinduzi, tunawashukuru sana viongozi wetu wa chama ngazi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru viongozi wa ngazi ya Kata na Matawi kwa sababu huko ndiko kulikuwa na kazi kubwa ya kampeni na wao walifanya kazi kubwa. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwashukuru viongozi wangu wa chama ninaomba niwashukuru wananchi wa Jimbo la Mpanda Mjini walifanya kazi kubwa, walinipa kura nyingi, lakini wakamheshimisha sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kura nyingi za kishindo, ahadi yangu kwao nitawatumikia kwa moyo wangu wote. Nilipita kwenye kampeni nikielezea ahadi mbalimbali za ilani ya CCM niko hapa bungeni kufuatilia ahadi zile za ilani ya CCM na yale tuliyoahidi tutahakikisha yote yanafika kwenye jimbo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani niende kwenye pongezi. Nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa ushindi mkubwa alioupata, ushindi ule umetafsiri yale ambayo yalifanyika katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wake, lakini baada ya kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais nimpongeze pia Mheshimiwa Makamu wa Rais Dkt. Emmanuel Nchimbi kwa sababu naye alikuwa pamoja kwenye *ballot paper* ya Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, tunaamini Makamu wa Rais alikuwa mtu sahihi na Mgombea Urais alikuwa mtu sahihi ndiyo maana tukapata ushindi mkubwa wa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri mkuu kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuteuliwa, lakini na kwa kupitishwa na Bunge lako Tukufu. Niwapongeze pia Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa

kuteuliwa na kuchaguliwa kuwa Spika na Naibu Spika. Kwa namna ya pekee nikupongeze wewe na Wenyeviti wengine kwa kupata nafasi hiyo mliyoipata, ninaamini kwa uzoefu ulionao utaendelea kutuongoza vizuri katika Bunge hili la Kumi na Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye mchango wangu na utajielekeza kuanzia ukurasa wa 17 mpaka ukurasa wa 24 na kwanza kabisa kwa kweli nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan nikianzia kwenye sekta ya maji. Jimbo langu la Mpanda Mjini kwa sasa linazalisha lita milioni sita za maji na kuwahudumia wananchi wa Mpanda Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu gani? Tunao Mradi wa Miji 28 ambao utakwenda kuongeza upatikanaji wa maji kwenye Jimbo la Mpanda Mjini kutoka lita milioni sita za sasa mpaka kufikia lita milioni 18, tunaamini zitatusaidia sana kuondoa changamoto ya maji kwenye Mji wetu wa Mpanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Katikati tukikaribia kwenye kampeni Mheshimiwa Rais alionyesha upendo wa dhati kwa wananchi wa Jimbo la Mpanda Mjini na akatuongezea mradi wa kuongeza lita milioni mbili, mradi wa kutoka kwenye vyanzo vya maji ya mserereko vinavyotoka kwenye eneo la Kanoge miradi hii ikikamilika, tutakuwa na uwezo wa kuzalisha lita milioni 20 kutoka milioni sita za sasa. Tafsiri yake ni nini? Unaona kabisa kwamba tutakuwa na maji ongezeko la karibu mara tatu au mara mbili na nusu zaidi ya yale ambayo tunayapata sasa tunaamini changamoto ya maji kwenye Mji wa Mpanda inaweza ikaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili ninaomba sana ndugu yangu Waziri wa Maji, kaka yangu Aweso. Sisi watu wa Mkoa wa Katavi tulikuwa na mambo matatu makubwa ambayo tulikuwa tunayaomba kwenye Serikali hii toka kipindi Mheshimiwa Dkt. Samia anaingia madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mawili makubwa yamefanyika tulikuwa hatuna Gridi ya Taifa, Gridi ya Taifa imefika kwenye Mkoa wetu wa Katavi, lakini changamoto iliyobaki ni maji ya uhakika na katika hotuba ya Mheshimiwa Rais kitu ambacho kilinifurahisha ni kwamba kuna Gridi ya Maji ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Aweso tusaidie sana kwenye huu Mradi wa Taifa wa Gridi ya Maji, mradi huu uende ukaanzie Ziwa Tanganyika na tulishakwenda na wewe mpaka Karema ukaenda ukakagua eneo la chanzo Ziwa Tanganyika. Kwa hiyo, niombe sana tuhakikishe mradi huu wa Ziwa Tanganyika unafika kwenye Mji wetu wa Mpanda, lakini utoke kwenye Mji wa Mpanda na kwenda kwenye maeneo mengine ya nchi hii ili kwenda kuwasaidia watu ambao hawana maji ya uhakika ili nchi nzima imwagike maji na hilo tunaamini mama yetu Samia Suluhu Hassan analiweza tuna imani na yeye tunamwomba Mheshimiwa Waziri apambane kuhakikisha kwamba mradi huu unatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoke kwenye hilo eneo la maji niende kwenye eneo la afya na sisi watu wa Katavi kwenye eneo la afya tunatoa shukrani nyingi, nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais samia. Kipindi Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan anaenda kuchukua nchi hii Hospitali ya Mkoa wa Katavi ilikuwa kwenye eneo la msingi na mradi ule ulikuwa umesimama kwa karibu miezi nane hautekelezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru baada ya Mheshimiwa Dkt. Samia kuingia madarakani alifanya mabadiliko ndani ya chama akamteua Katibu Mkuu Chongolo na Katibu Mkuu alivyokuja kwenye ziara yake viongozi wa Mkoa wa Katavi wakamwomba Katibu Mkuu wa Chama amfikishie salamu Mheshimiwa Dkt. Samia na aje aukwamue ule Mradi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru tunavyoongea sasa hivi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi inahudumia wananchi wa Mkoa wa Katavi. Kubwa zaidi kwenye eneo hilo alikamilisha jengo la *OPD* na sasa hivi linajengwa jengo la *wing B* ambalo

litahudumia mama na mtoto. Katika jengo hili la *wing B* tumepata shilingi bilioni nne na linahitaji bilioni 10. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana viongozi wa Wizara ya Afya watusaidie kwenda kumalizia hili jengo ambalo litakuwa linahudumia akinamama na watoto wa Mkoa wa Katavi. Tunaamini tukiwahudumia akinamama na watoto vizuri itakuwa pia ni baraka kwa Rais wetu, lakini itakuwa pia ni baraka kwa Serikali yetu, hii ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais Mama yangu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hilo hilo la Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi tulipata bahati ya kumwomba Mheshimiwa Rais pale Katavi wagonjwa ambao walikuwa wanasumbuliwa na maradhi ya figo, walikuwa wanasafiri na umbali mrefu kwenda Mwanza, Mbeya ama kuja hapa Dodoma ili kufanyiwa matibabu kwa maana ya kuchuja damu *(dialysis)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi yale yalivyofika kwa Mheshimiwa Rais alituletea pesa shilingi milioni 227 ambazo zilijenga jengo kwa ajili ya kufanyia haya mambo ya uchujaji wa damu kwa maana ya *dialysis* na leo hii ninavyosimama hapa Bungeni kuongea Mkoa wa Katavi sasa hivi mambo ya *dialysis* yanafanyika kwenye Mkoa wetu wa Katavi. Kwa hiyo, tunampongeza sana na kumshukuru Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Haidary Sumry, muda wetu umekwisha.

**MHE. HAIDARY H. SUMRY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge ninawashukuru sana kwa kuwajibika ipasavyo tokea asubuhi. Ninajua wengi mnatamani kuongea zaidi na kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais ambayo ni dira ya miaka mitano katika Taifa letu, lakini kwa mujibu wa kanuni zetu hatuwezi kuongea bila

mipaka. Kwa hiyo, leo tumevumiliana sana kwa sababu ni mambo mengi na muhimu mmeyasema kwa faida ya Taifa letu na Waheshimiwa Mawaziri wanasikiliza kwa sababu ninyi michango yenu ndiyo inaenda kusababisha utekelezaji mzuri wa dira hii ambayo Mheshimiwa Rais ameitoa kupitia hotuba yake.

Tutaendelea kuvumiliana, kwa muda mfupi baadaye itabidi tufuate kanuni zetu kwa sababu ukipewa dakika tano inabidi uji-*tune* kwenye dakika tano, ukipewa dakika 10 inabidi uji-*tune* kwenye dakika 10. Kwa hiyo tunaomba sana tuzingatie muda wakati tunatoa michango yetu.

Ninaamini tutaendelea kujifunza taratibu na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu muda bado ni mrefu akitujali uzima na uhai na tunamwomba basi tutaweza kutoa michango yetu mizuri kwa Serikali yetu na kuweza kulisaidia Taifa letu.

Baada ya kusema hayo niwatakie jioni njema, ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 2.24 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 30 Januari, 2026, Saa Tatu Asubuhi)*